ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 18 Aprili, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe: Waziri wa Nchi (OR) Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuweka mezani hotuba ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na pia hutuba za Wizara nyengine zote za SMZ ya kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Omar Shehe (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika *PAC*): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 85

Uchakavu wa Afisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali

Mhe. Saleh Nassor Juma: Aliuliza:-

Mpiga chapa Mkuu wa serikali ni taasisi muhimu sana katika kuchapisha mambo muhimu sana na nyeti ya serikali. Kwa hivyo, ni taasisi inayohitaji kutunzwa, kuthaminiwa na kuwezeshwa katika kufanya shughuli zake za kila siku. Kwa kuwa kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kimo katika mazingira magumu na ya hatari ikiwemo kuvuja na kupitisha maji pale msimu wa mvua unapowadia.

(a) Je, serikali inayo taarifa hiyo.
(b) Kama inayo ni hatua gani za dharura zimechukuliwa, ili kuinusuru hali iliyopo sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.85 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali inatambua kuwa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ni taasisi muhimu sana na ndio maana inachukua hatua mbali mbali za kuimarisha taasisi hii. Aidha inaelewa matatizo inayoikabili taasisi hii.

(b) Mhe. Naibu Spika, zipo hatua mbali mbali zinazochukuliwa na serikali katika kukinusuru na kukiendeleza kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali zikiwemo hatua za muda mfupi na muda mrefu.

Mhe. Spika, katika jitihada za muda mfupi serikali imefanya ukarabati wa jengo kwa kuziba paa na kusafisha mitaro iliopo pembezoni mwa jengo hilo, ili mvua zinaponyesha maji yasituame yaende moja kwa moja katika msingi mkuu wa Saateni unaomwaga maji yake baharini.

Mhe. Naibu Spika, aidha katika hatua za muda mrefu serikali imefanya maamuzi ya kukihamisha kiwanda hicho katika eneo la Saateni kwenda Maruhubi katika baadhi ya majengo ya kilichokuwa Kiwanda cha Sigara. Kazi kubwa ya ukarabati wa majengo haya imeshafanyika na inaendelea na tayari mashine za kisasa za aina ya *digital* zimeshaagizwa na zinatarajiwa kuwasili na kuanza kufungwa mwanzoni mwa mwezi wa Mei.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya ndugu yangu Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa amesema kwamba kuna hatua za muda mfupi na muda mrefu. Vile vile kwa kuwa keshokutwa tunategemea mawingu makubwa sana ya mvua za Masika. Pia kwa kuwa ndani ya kiwanda kile kuna *documents* muhimu za nchi je, anaweza kutueleza hizi za muda mfupi zimefikia wapo, kusudi tuweze kufahamu mvua hazitokuja hazitaharibu zaidi pale.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali kwamba na yeye atakubaliana nami kwamba kiwanda

kwa mazingira kilipo sasa hakipendezi kwa shughuli zetu za uchapishaji. Ndio maana serikali ikafanya uwamuzi wa kukiondosha kiwanda kile pale kwa sababu kubwa ya kuingia maji wakati wa mvua kubwa zinaponyesha.

Kwa msingi huo basi watendaji katika taasisi ile wanatakiwa kuelewa umuhimu wa zile nyaraka muhimu kuziweka mahala pazuri, ili maji yanapoingia ndani ya kiwanda zisiharibike. Kwa kweli wamekuwa wakichukua jitihada hizi na tutaendelea kuwahimiza wahakikishe kwamba pale mvua inapokuwa kubwa, basi mpango wao wa mle ndani ya kiwanda wahakikishe kwamba nyaraka muhimu haziharibiki.

Lakini kubwa na hili tunalolifanya la uwamuzi wa kuondoka pale, ili tuepukane na tatizo lakujaa kwa maji katika eneo lile la Saateni kutokana na hali halisi ya bonde iliopo katika kiwanda kile.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amesema kiwanda kile kimehamishwa kupelekwa eneo la Maruhubi, sijui wamefanya utafiti gani kupeleka eneo lile la Maruhubi ukizingatia pale kuna kiwanda cha Bohari Kuu na kupeleka pale wakati huduma ya maji haipo, serikali imejipanga vipi kupeleka huduma ya maji pale kwa muda huu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, bahati nzuri eneo la Maruhubi ambao uwamuzi umefanywa kuweka kiwanda hichi ni lile eneo walilopewa Kiwanda cha Sigara. Pale palikuwa nje magodauni mengi ya Kiwanda cha Sigara. Eneo lililotumiwa na Bohari Kuu ni sehemu ya sehemu nyingi zilizokuwepo pale ndani, tutahamia sisi, watahamia taasisi *Bureau Standard* ya Zanzibar na wengine, kwa sababu yapo majengo mengi.

Utaratibu tulionao tumeshirikiana kwanza kwa kuwa na umeme wa kusholeza mahitaji ya pale hali hiyo ni nzuri. Lakini suala la maji kwa sasa yapo maji ambayo yanaweza kukidhi haja ya shughuli zetu na ikiwa kuna uhitaji wa kuongeza maji zaidi basi tutafanya hivyo kuhakikisha kwamba tunapata maji zaidi, maana pale tunaweza kuchimba hata kisima na tukapata maji. Kwa ufupi maji ambayo yapo sasa yanaweza kukidhi haja ya shughuli yetu ya kiwanda ambacho tumekusudia kukiweka.

Nam. 103

Ujenzi wa Skuli ya Mizingani

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imewashajihisha wananchi kujenga mabanda ya skuli, ili kupunguza tatizo la makaazi skulini, wazee wa Shehia ya Mizingani kwa kushirikiana na walimu waliuitikia wito huo toka mwaka 2004 na kuwekwa jiwe la msingi na Mhe. Rais Mstaafu Dkt. Amani Abeid Karume tarehe 31/3/2010, ambapo lilikuwa limeshamaliza kujengwa kwa hatua zote za kuta. Kwa kuwa banda hilo hivi sasa limeanza kuanguka matofali. Na kwa kuwa Waziri wa Elimu wa wakati ule alikuwa Mhe. Haroun Ali Suleiman aliahidi mbele ya kadamnasi kuwa wizara italiezeka na kulimaliza.

(a) Kwa nini hadi leo hii banda lile halijaezekwa.

(b) Ni lini basi wananchi wa skuli ya Mizingani wataezekewa banda lao.

Mhe. Naibu Waziri Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 103 lenye (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu naomba kwanza nitoe utangulizi kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba serikali imeshajihisha wananchi kujenga majengo ya skuli kwa dhamira ya kuhakikisha kwamba watoto wote wanaofika umri wa kwenda skuli wanapata nafasi ya kwenda skuli. Wananchi katika sehemu mbali mbali ya nchi yetu wameitikia vyema wito huo pamoja na wananchi wa Shehia ya Mzingani ambao wamejenga madarasa manne.

Mhe. Spika, hadi hivi sasa jumla ya madarasa 288 na ofisi 44 na ghala 18 yamefikia hatua ya kuezekwa na wizara imekabidhiwa rasmi na wananchi. Pia ni kweli kwamba jengo hili liliweka jiwe la msingi na Rais Mstaafu wa awamu ya sita Dkt. Amani Abeid Karume na hadi hii leo halijakamilika.

Baada ya maelezo haya napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

(a) Jengo hilo halijakamilika kutokana na wizara kuwa na majengo mengi ya kukamilisha ukilinganisha na uwezo wake wa fedha. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, wizara ilitenga jumla ya 800,000,000/= kwa ajili ya mradi wa kuimarishaji elimu ya msingi, hadi Machi 2013

Wizara ya Elimu tumepata 347,000,000/= sawa na asilimia 43.4, kiasi hichi cha fedha ni kidogo ukilinganisha na idadi kubwa ya madarasa yanayohitaji kukamilishwa. Kwa msingi huo baadhi ya majengo hayawezi kukamilishwa kwa wakati ambao tulipanga.

(b) Napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kazi ya kukamilisha ujenzi wa jengo hilo zinatarajia kuanza katika kipindi cha hivi karibuni na baada ya kupata fedha kutoka kwa wahisani wetu. Hivi sasa taratibu za ununuzi wa vifaa zinaendelea mara tu zitakapokamilika kazi hii itaanza na ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi wa Novemba 2013.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mzuri ya Mhe. Naibu Waziri. Lakini kwa kuwa banda hili ni kongwe, limeanza kujengwa tokea mwaka 2004 na kuwekewa jiwe la msingi mwaka 2010. Na kwa kuwa Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Elimu wa wakati ule Mhe. Haroun Ali Suleiman alizungumza kwenye kadamnasi wakati Rais wa Zanzibar mstaafu yupo na wananchi wote wa Mzingani wapo kwamba banda hili litaezekwa kwa sababu wizara imeshalibeba.

(a) Je, kuchelewa kuezekwa kwa banda hili na hatua ya kuanguka tofali moja moja hivi sasa hatuoni kwamba tumeipuuza kauli ya Mhe. Haroun Ali Suleiman.

(b) Kuchelewa kuezekwa kwa banda hili na kumalizika na uhaba wa mabanda yaliyopo katika Skuli ya Mzingani hatuoni kwamba tunawapa matatizo na msongamano mkubwa wa wanafunzi katika Skuli ya Mzingani na kuwasumbua walimu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kupangani kuchagua, Mhe. Muhammed Mbwana ndani ya jimbo lake anazo skuli karibu tano kwa nane. Karibuni tu mwaka jana tumemlazia skuli yake moja ya Jambangome, yenye madarasa manne, ambapo watoto wa Jambangome walikuwa wakati wa mvua au jua basi ni lazima waje Mzingani. Kwa hivyo, tukaona pale kipaumbele ni ile skuli kwanza ya Jambangome.

Kwa hivyo, sio kama tumeidharau hii ahadi ambayo imewekwa na Mhe. Rais mstaafu, lakini pia na Waziri wa Elimu aliyepita, tunaikubali na ndio maana tukamwambia kwamba tutajenga katika mwaka huu, pesa ambayo tutapata kwa wafadhili wetu wa *SIDA*. Kupanga ni kuchagua Mheshimiwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri naomba kwa upole sana nimuulize swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa katika jibu lake la msingi Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba huu mradi wa uwezeshaji wa Elimu ya Msingi ulitengewa 800,000,000/= lakini hadi kufikia Machi mwaka huu zimepatikana 347,000,000/= sawa na asilimia 43.4. Kwa kuwa mabanda yaliyokuwepo ni mengi yanahitaji kumaliziwa na Wizara ya Elimu yaani yapo Unguja na Pemba. Na kwa kuwa kuna mabanda ya zamani sana kwa mfano mabanda yaliyokuwepo Skuli ya Ng'ambwa katika Jimbo la Wawi lipo limemaliza tangu mwaka 1998 na hadi leo hii Wizara ya Elimu haijatia mkono pale kumalizia katika Skuli ya Ng'ambwa katika Jimbo langu la Wawi.

Je, ni fomula gani inayotumika ili kuona kila sehemu kwa kiwango hichi hichi kidogo cha fedha kila eneo la nchi hii Wizara ya Elimu inatia mkono wake na sio kuelekeza pahali pamoja tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amani: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama alivyozungumza Mhe. Mjumbe kwamba bajeti, ambayo tulitenga ni 800,000,000/= na ambayo tumepata ni 347,000,000/= na asilimia 43.4. majengo ambayo tunayo ni mengi lakini nilisema hapo mwanzo kama kupanga ni kuchagua na nilimuahidi Mhe. Saleh Nassor kipindi kilichopita katika mabanda ambayo tumeyaweka kipaumbele ni ya zamani na Skuli yake ya Ngambwa imo. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi, muhimu ni kupatikana hizi pesa ambazo tumeomba, tukizipata tu hizi pesa basi tutahakikisha na Skuli yake ya Ngambwa inajengwa.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, swali la msingi lilikuwa linahusiana zaidi na mimi katika Jimbo langu la Chaani, ambapo nina skuli tano zote zinasubiri kuezekwa.

(a) Naomba Mhe. Waziri anieleze ni lini skuli yangu ya Moga ataniezekea, ili wale wanafunzi wangu wasiendelee kusoma katika Tawi la CCM ambalo ni bovu linavuja na linaweza likasababisha madhara kwa wanafunzi wetu.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Wizara ya Elimu inaonesha dhahiri kushindwa na mambo mengi moja wapo ikiwemo kuzimalizia skuli, ambazo zimejengwa na washehimiwa kwa kushirikiana na wananchi wao. Haoni sasa kuna haja ya kubadilisha sera ya kuendeleza kujenga mabanda ikafanya

kama mpango wa Wizara ya Afya sasa kwa kuzingatia idadi ya walimu, uwezo pamoja na wanafunzi wanaosoma kwanza ikaacha haya mapya yanayojengwa na ikamaliza yale ya zamani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, nasisitiza kusema kwamba tutaezeka mabanda hayo pindipo pesa zikiingia katika wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, Sera yetu ya Elimu ya mwaka 2006 licha ya kuwahimiza wazee na walimu kuwashajihisha kuwa wajenge mabanda haya, lakini pia ni kuhakikisha kila mwanafunzi wa Kizanzibari anapofikia umri anapata nafasi ya kusoma, sasa tukisema tubadilishe sera tuwambie kwamba sasa wananchi wasijenge haya madarasa kwa sababu hatuna uwezo wa kuyamaliza sidhani kama tutaweza kuwafanyia wanafunzi wa Kizanzibari haki yao. Kusema kweli Mhe. Naibu Spika, kwa hili mpaka hivi sasa hakuna mwanafunzi ambaye anafikia wakati wa kusoma ikawa hapati kuingia darasani na kusoma.

Nam. 48

Uboreshaji wa Shirika la *ZBC – TV*

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Katika kusheherekea miaka 49 ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuwa mgeni rasmi katika Uzinduzi wa Matangazo ya *Digital* na jengo la Kurikodia Mambo ya Sanaa pale Rahaleo, Mhe. Rais alitoa maelezo ya kusikitisha kwa namna chombo chetu cha habari (*ZBC – TV*) kilivyofeli kufanya kazi zake ipasavyo, pamoja na kuwa wizara husika imebahatika kuwa na wataalamu wa kila rika (waze na vijana) katika shirika hili la habari.

(a) Ni sababu gani hasa iliyosababisha hali hiyo.

(b) Hivyo ni hatua gani wizara imechukua kuondoa hali hii ya aibu.

(c) Je, kuna mambo gani ambayo yanahitaji marekebisho, ili shirika hili liweze kubadilika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa ruhusa yako kabla ya kujibu swali hili Nam. 48 la Mhe. Mjumbe kuhususiana na huduma za *ZBC*, chombo ambacho mama yetu Msanii Mkongwe Bi Kidude Binti Baraka aliyefariki jana kilimtangaza sana wakati wa uhai wake. Nichukue fursa hii niwambie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba maiti ya marehemu itasaliwa katika msikiti wa Muembeshauri saa 7 leo mchana na atazikwa Kitumba saa 8 mchana. Naomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu tushirikiane katika kumstiri mama etu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi. Ni kweli kuwa Mhe. Rais alitoa maelezo ya kusikitisha kwamba utoaji wa huduma za *ZBC* kwa umma hazijafikia matarajio yake na umma kwa jumla. Kimsingi maelezo yale ni changamoto kwa uongozi wa wizara yangu kama wasimamizi wa Shirika la *ZBC*.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali hili lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Sababu hasa iliyopelekea hali hiyo inatokana na kukatika kwa matangazo ya *ZBC* mara kwa mara na kutokuwa na ubora wa vipindi vilivyotayarishwa. Zipo sababu za kutokea kwa mambo hayo yakiambatana labda na bajeti ndogo ya kuendesha shirika.

Itakumbukwa kwa muda mrefu kumekuwa na tatizo la umeme tatizo ambalo lililoathiri matangazo ya *ZBC*, ambayo sasa inatoa huduma za masaa 24 kwa bajeti ya mwaka jana iliyokuwa ya kuhudumia masaa 12. Bajeti hiyo hiyo ilikuwa haiwezi kuhudumia gharama za mafuta ya ziada ya kuendesha majenereta muda wote umeme unapokuwa umezimwa. Aidha vifaa vinatumiwa vya kurushia matangazo na kutengeneza vipindi vimechakaa, vifaa hivyo ni pamoja na *camera*, compyuta, *editing machine*, *transmitter* na magari. Haya ni mambo yanayodhoofisha sana uwezo wa utendaji wa shirika.

(b) Hatua zinazochukuliwa na wizara katika kukabiliana na hali hiyo ni kuliongezea uwezo shirika kwa kulipatia vitendea kazi. Katika juhudi hizo ni pamoja na kuimarisha *studio* ya kutengenezea vipindi na kurushia matangazo iliyokuwepo *Karume House* na pia kuanzisha *studio* nyengine mpya huko Mkoroshoni Pemba. Pamoja na hatua hizo wizara kupitia Bodi

ya Shirika imeazimia kuangalia upya maslahi ya watendaji wa shirika, ili kuongeza ari na mori wa kufanya kazi

(c) Pamoja na niliyoyaeleza kwenye jibu (b) mambo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho katika Shirika la Utangazaji ni kurekebisha muundo wa shirika, ili kupata muundo bora na pia kuangalia safu za uongozi kwa kuwa na watendaji wachapa kazi, wenye uwezo, ujuzi na ujasiri wa kutekeleza majukumu yao kulingana na Sheria ya Shirika iliyopitishwa katika Baraza lako tukufu katika kikao kilichopita.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kupitia Shirika la Utangazaji tayari limo katika maandalizi ya kujidhatiti na kufanya marekebisho hayo, ili shirika liweze kubadilika kwa kufanya yafuatayo:-

i) Kutayarisha bajeti itakayoendana na mahitaji ya shirika kutoa huduma za saa 24. Kazi hiyo inaendelea hivi sasa.

ii) Kuwe na mitambo mipya inayoendana na wakati huu, tayari wizara inasimamia upatikanaji wa vifaa hivyo.

iii) Kupatiwa mafunzo ya kutosha kwa wafanyakazi wa *ZBC*

iv) Kuwepo kwa *"scheme of service"* inayolingana na mashirika mengine, ili kuwaongezea wafanyakazi maslahi hayo. *Scheme of Service* tayari imeshatayarishwa na imeshawasilishwa na inasubiri bodi mpya, ili iweze kufanyiwa kazi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata jibu ambalo Mhe. Waziri nampongeza tena nampongeza sana. Vile vile nampa pole kwa kupata msiba wa mzee wetu ambaye naye ni katika wizara yake na yeye yumo katika msiba, nampa pole lakini na nampongeza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika kujibu swali langu kwa matayarisho ya baadaye kuona kwamba mambo yanakwenda vizuri amesema ni pamoja na maandalizi mazuri ya bajeti yatakayomuwezesha mfanyakazi masaa 24 badala ya masaa 22 kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, kwa uzoefu nilionao ikiwa bajeti inayoombwa siyo inayoingizwa kama kiipindi hichi ambacho kinamalizika kama kumbukumbu zangu ni sahihi alipata 12% tu. Sasa kama ikitokezea hakupata bajeti kama

aliyokusudia na hii ndio ambacho kichocheo cha kuendesha hizo shughuli zake ipasavyo ana mpango gani mwengine, ili ahadi yake isije ikatenguka.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ni kweli mara nyingi bajeti tunayoipitisha sio ile ambayo tunaipata na hivi kwa kiasi kikubwa huathiri utendaji wa shughuli zetu. Lakini katika kujiweka sawa na hilo nakumbuka kwamba katika kikao kilichopita cha Januari Baraza lako tukufu lilipitisha Sheria ya Uwanzishwaji wa Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*).

Baada ya sheria hiyo kuwekwa sahihi ya Mhe. Rais na kuna sheria rasmi, wizara yangu itashauriana na Wizara ya Nchi Fedha kuangalia uwezekano wa kwamba kile kinachozalishwa na *ZBC* kiwezekane pia kutumika kwa ajili ya kuendesha vipindi kinyume na sasa kwamba kinachozalishwa kinapelekwa Hazina.

Kwa hivyo, wakati huo kutakuwa na uwezo mkubwa wa kukusanya mapato Mhe. Naibu Spika na hata vipindi hivi ambavyo tunavipeperusha moja kwa moja hivi sasa, ambavyo havilipwi basi tumeanza mashauriana na uongozi wa Baraza lako tukufu kuona namna gani katika bajeti ijayo tuweze kulipwa, ili malipo yatakayopatikana basi yaweze kusaidia katika uendeshaji wa shirika letu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kwa kuishukuru Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na waziri husika kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya mazishi ya msanii wetu, kipenzi Bi Kidude ambaye anaishi katika Shehia ya Rahaleo Jimbo la Rahaleo.

Baada ya kutoa shukrani hizo Mhe. Naibu Spika, *ZBC* na *ZBC* redio katika miaka ya nyuma tumekuwa tukishuhudia *ZBC* wakati huo inaitwa *TVZ* pamoja na redio Zanzibar kwa kutangaza na kutia nyimbo za maombolezi, siku ya maombolezi ya kipenzi chetu Mzee wetu Mzee Abeid Aman Karume. Lakini katika kipindi cha maombolezi cha mwaka huu, *ZBC* televisheni ilikuwa ikionesha vipindi mbali mbali vya kawaida pamoja na nyimbo za kawaida. Lakini *ZBC* redio ilikuwa ikipiga nyimbo za maombolezi.

Je, ni sababu zipi zilizofanya *ZBC* televisheni kutoonesha historia ya mzee wetu Mzee Abeid Aman Karume na kuonesha vipindi vya kawaida.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Ni kweli kwamba vyombo vyeti hivi vya serikali vina kawaida katika siku ile ya maombolezo ya kifo cha muasisi wa Mapinduzi mzee wetu Mzee Karume, kutangaza nyimbo za maombolezo. Hii ilikuwa ni kawaida na bado ndio mtazamo na maelekezo ya Wizara.

Lakini kipindi cha mwaka huu redio iliendelea kuendeleza. Lakini kwa bahati mbaya televisheni haikufanya hivyo. Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba chombo chetu cha televisheni hivi sasa kina matatizo sana ya ubovu wa mitambo, kwa hivyo tunapata matatizo mengi katika kuweka sawa mambo yetu. Kwa hivyo, haikuwa kwamba ni sababu yoyote ile ila tunapata matatizo.

Mhe. Naibu Spika, hata mkiangalia taarifa za habari hivi sasa zinabadilika badilika, hazina mpangilio vizuri, kwa sababu ya ubovu wa mitambo tuliyonayo. Lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, suala hili tumeliangalia kwa kina na tumefanya vikao vizuri na tunatarajia ndani ya muda wa mwezi mmoja au miwili kununua vifaa vipya vya studio kutoka nje kwa gharama kubwa ya serikali.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri hilo, lakini ilikuwa ni kwa sababu ya hali yetu ya mitambo ilivyo. Naomba niwaombe radhi sana wananchi kwa hili, na kwamba sio hilo tu la maombolezo, lakini pia na vipindi vyengine katika kipindi hichi vitakuwa havina mpangilio wa kawaida, kwa sababu ya hali hiyo.

UTARATIBU

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa jibu lake. Lakini cha kusikitisha ni kwamba televisheni ilikuwa inafanya kazi na ilikuwa inaonesha nyimbo za kawaida pamoja na mipira. Kwa nini isioneshe picha za historia za mzee wetu, ikaonesha nyimbo nyengine pamoja na mipira.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nadhani kuna haja ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, mbali ya wale wa Kamati, maana wa kamati wanajua vizuri *ZBC* wanavyofanya kazi. Wale waliokuwa sio Wajumbe wa Kamati hii inayoshughulikia redio na televisheni, basi tupate nafasi kwenda pale televisheni mkaangalie namna gani mitambo yetu inavyofanya kazi. Inawezekana baadhi ya *editing machine* katika kipindi kile ikawa haiwezi kufanya kazi, tukafanya kazi kwa utaratibu mwengine. Naomba hilo lieleweke vizuri sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suala moja la nyongeza. Mhe. Waziri moja ya wafanyakazi kupata nguvu zaidi ni kupata motisha kwa kazi wanazozifanya. Kwa kuwa hivi karibuni tuliwaona wenzetu Tanzania Bara wakitoa motisha kwa waandishi bora na wafanyakazi bora.
Je, nakuuliza Mhe. Waziri umejipanga vipi kuona wafanyakazi wetu wa *ZBC* redio na *ZBC* televisheni, kuona kwamba wanapata motisha kwa wale wafanyakazi bora na je, kwa wale wanaofanya kazi kwa muda wa ziada, umejipanga vipi kuona kuwa unawaboresha kupata mafao yao ya ziada.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, suala la kwanza linalohusiana na kupewa zawadi wafanyakazi na watangazaji. Mhe. Naibu Spika, Baraza la Habari la Tanzania ni chombo ambacho kiliratibu shughuli ile na katika kufanya hivyo waandishi wa Tanzania nzima waliwekewa vigezo ambavyo ili wakifikia wanaweza kupewa motisha ile. Kwa bahati mbaya waandishi wetu wa Zanzibar kwa mwaka huu hawakufikia viwango na kama walifikia viwango basi na wao wangeweza kupata motisha ile ambayo wenzao wa Tanzania Bara wangeweza kufanya kazi vizuri.

Kwa hivyo, niwaombe waandishi wetu waendeleze jitihada ili mwakani tukijaaliwa vigezo vitakavyowekwa, basi waweze ku-*qualify* kupata motisha mbali mbali zinazotolewa na Baraza la Habari la Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na suala la *over time* na mambo mengine. Mhe. Naibu Spika, hali ikiruhusu tutawalipa. Lakini kama nilivyosema kidogo hali sio nzuri ya kifedha na tunachukua kumbukumbu za kila kitu, tunaahidi kwamba hali ikiwa nzuri, hakuna ambaye haki yake itapotea.

Nam. 59

Kilimo cha Mwani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kilimo cha mwani aina ya cottonii unaonekana kuwa na bei kubwa katika soko la dunia, lakini mwani aina hiyo unastawi katika kina kirefu cha maji ya bahari, na bahati mbaya kilimo chake kimekwama kutokanana Idara ya Uvuvi kuchelewa kuweka mipaka ya matumizi ya bahari kati ya wakulima na wavuvi Zanzibar.

a) Je, ni sababu gani zimepelekea hadi sasa karibu miaka mitano Idara ya Uvuvi imeshindwa kuweka mipaka hiyo na kusababisha kilimo cha mwani aina hiyo kukwama Zanzibar.

b) Kwa kuwa wataalamu wa Taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar (*IMS*) tayari wamekamilisha utafiti wa kilimo cha mwani kwa kutumia chanja, lini Idara itaweka mipaka ya wakulima wa mwani na wavuvi.

c) Kitendo cha Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini kuchelewa kuweka mipaka hiyo sio kuwavunja moyo watafiti hao kwa kuwa kilimo hicho kingeinua pato la wakulima na kuongeza fedha za kigeni kwa serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 59 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi makini, naomba kueleza yafuatayo. Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba mwani aina ya *cottonii* una bei kubwa katika soko la dunia.

Hata hivyo, kukwama kwa kilimo cha mwani huu hakutokani na Idara ya Uvuvi kuchelewa kuweka mipaka ya matumizi ya bahari kati ya wakulima na wavuvi wa Zanzibar. Uhalisia wake ni kwamba mwani wa cottonii hauoti katika kipindi chote cha mwaka isipokuwa katika kipindi kifupi cha majira ya hali ya baridi. Vile vile katika maeneo machache sana ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kumjibu maswali yake yote kwa pamoja. Mhe. Naibu Spika, mipaka ya matumizi ya bahari kati ya wakulima wa mwani aina ya cottonii na wavuvi wa Zanzibar, haijawekwa kwa sababu kitaalamu haijawa na ulazima wa kufanya hivyo. Mwani wa aina hii haustawi vyema katika bahari yetu kutokana na hali ya joto kali na mabadiliko ya hali ya hewa yanayoendelea, huota kwa tabu sana kwa kipindi kifupi cha msimu wa baridi tu. Sababu hiyo wakulima wengi wameshindwa kuotesha mwani huo na kuamua kupanda mwani mwembamba aina ya *spinosum* ambao unaota bila ya shida yoyote na kwa urahisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, wananchi kwa kupitia kamati zao za uvuvi wa mwani hufanya makubaliano ya matumizi ya maeneo ya bahari katika vijiji vyao na shehia zao

mbali mbali baada ya makubaliano na wizara yangu, ikishirikiana na wanajamii kuweka utaratibu mzuri kwa matumizi ya kuweka maeneo tengefu ya bahari.

Mhe. Naibu Spika, aidha watafiti wa taasisi ya sayansi ya baharini hatuwavunji moyo. Utafuti umefaywa na taasisi matumizi yake yameelezwa na wafanyakazi wetu kupitia mradi wa *MACEMP*. Hivyo, matokeo ya utafiti huo tunayo katika wizara yangu na tunayafanyia kazi kwa karibu zaidi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri utakuwa tayari baada ya kumaliza kikao hiki kufuatana na mimi kukutana na wataalamu wa sayansi na mambo ya bahari, ambao wamekuwa wakilalamika kutowepo kwa mipaka ya wavuvi na wakulima wa mwani na kusababisha kutofika lengo la mwani huo.

(b) Kwa kuwa wanasayansi wa bahari kutoka Chuo Kikuu cha (*IMS*) yaani *Institute of Marine Sciences* wamefanya utafiti na kugundua mwani wa aina hiyo unaweza kuota katika kima kikubwa cha maji ya bahari. Je, serikali imefanya utafiti gani kuhusu suala hilo Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, wizara yangu iko tayari kufuatana na Mwakilishi makini kama wewe unayejali wananchi wako na kwenda kulifuatilia suala hili kwa umani zaidi.

Lakini naomba swali la (b) arejee Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nilisema,

(b) Kwa kuwa wanasayansi wa bahari kutoka Chuo Kikuu cha (*IMS*) yaani *Institute of Marine Sciences* wamefanya utafiti na kugundua mwani wa aina hiyo unaweza kuota katika kima cha maji makubwa Je, serikali imefanya utafiti gani kuhusu suala hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kweli watafiti wetu wamefanya, lakini kuna kazi ambayo bado wizara yangu inaendelea nayo. Lakini vile vile kumekutwa na matatizo matatu makubwa ambayo katika utafiti huo yanaendelea. Matatizo yenyewe ni kama yafuatayo.

Ukulima huu hufanywa kwa kutumia njanja za miti ya mianzi, na mianzi sasa hivi ni adimu sana katika nchi yetu hii ya Zanzibar imepungua kwa kiasi kikubwa sana, hivyo kunaleta upungufu mkubwa wa suala hilo.

Lakini suala la pili ukulima wa mwani wengi wa wakulima wetu ni wanawake na unafanywa katika kina kirefu cha maji, hivyo husababisha sana kuchukua vyombo kwenda kule itahatarisha maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, suala la tatu vile vile mwani huu upandwa katika kina kirefu na kuna upepo mkubwa, husababisha mianzi ile kuweza kupeperuka na kuharibu mazao yote.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa mwani huu wa *cottonii* ni adimu kisiwani Pemba, na kwa kuwa mwani wa mvinje ndio mwani unaoonekana sana kisiwani Pemba na mwani huu hauna bei, na kwa kuwa katika swali mama lilisema kwamba mwani wa *cottonii* haustawi hapa Zanzibar.

Je, Mhe. Naibu Spika, wakati huo na mimi nilikuwa ni mshika fedha wa kikundi cha *Hatuwafichi Society* Kisiwani Pemba katika Shehia ya Kangani. Je, Mhe. Naibu Waziri kuna uwezekano gani wa kuwapatia wakulima wetu wa mwani wa *cottonii*, ili kupata kiwango kizuri cha fedha wakaweza kujimudu kimaisha. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, katika jibu langu mama nilisema mwani wa *cottonii* unaota katika sehemu chache katika Zanzibar yetu. Lakini vile vile katika sehemu ambazo zinaota, wizara yangu inashirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuweza kupata kampuni ambazo tunawaongezea bei kubwa ili waweze kupata mafanikio mazuri wakulima wetu wa mwani.

TAARIFA ZA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamuita Mhe. Waziri, nilikuwa naomba nitoe taarifa fupi tu. Tukiangalia *Order Paper* utakuta wizara zote zimewekwa pale, ili akimaliza Waziri, wizara moja moja nayo itaweza kutoa maelezo yake japo kwa ufupi. Kwa hivyo, naomba tujipange vizuri ili wizara ikifika tuweze kutoa majibu hayo kwa yule aliyekuwa nayo na aliyekuwa hana, vile vile atasimama na kusema mimi hoja nimejibu sina. Nadhani tumefahamiana.

Kwa hivyo, namuita Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa ruhusa yako. Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha uzima na kuwepo hapa hii leo, kwa lengo la kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Aidha, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii, ili kuweza kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*), kupitia taarifa yao iliyowasilishwa ndani ya Baraza lako tukufu mnamo mwezi wa Aprili mwaka 2012.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani za kipekee kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya *PAC* chini ya uongozi wa Mwenyekiti wao Mhe. Omar Ali Shehe Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Chake Chake, kwa kuisaidia sana serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoendeshwa kwa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika kutushauri kwa njia ya kufanikisha utendaji wa majukumu ya serikali kwa mujibu wa sheria mbali mbali za nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, sitotenda haki kama sitotoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, michango waliokuwa wakiitoa katika kutekeleza majukumu yetu, imekuwa ni muongozo na kutusaidia sana katika kufikia malengo. Nachukua fursa hii kuwashukuruni nyote kwa busara, hekima na nasaha zenu, nasema ahsanteni sana Mwenyezi Mungu awabariki.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria ya fedha, afisa mas-uli wa kila taasisi, ndiye atakayekuwa na wajibu kwa Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi, wa kutoa maelezo juu ya matumizi ya fedha zilizoidhinishwa na Baraza lako tukufu kwa ajili ya taasisi hiyo. Kwa upande wa usimamizi juu ya utekelezaji wa sera na sheria za fedha na manunuzi ya mali ya umma, ni jukumu la moja kwa moja la afisi inayosimamia masuala ya fedha. Kwa hivyo, tuna wajibu wa kutoa taarifa ndani ya Baraza lako tukufu kama kanuni ya Baraza la Wawakilishi nambari 108(15), toleo la mwaka 2012 linavyoelezea.

Mhe. Naibu Spika, wakati Kamati ilipokuwa ikichunguza hesabu za serikali kwa taasisi mbali mbali, mambo yafuatayo yamejitokeza. Kwanza mapungufu katika matumizi ambayo yamepelekea Kamati kuhoji upatikanaji wa stakabadhi, uorodheshaji wa mali ya serikali iliyonunuliwa au thamani kutolingana na uhalisia

wa manunuzi yaliyofanywa, pamoja na mambo mengine yanayolingana. Eneo hili ambalo linaonesha zaidi utendaji, linahitaji kupatiwa ufumbuzi kutoka kwa afisa muhasibu au afisa mas-uli wa taasisi. Ni matarajio yangu kuwa Makatibu Wakuu wamefanya hivyo wakati wa kutoa ufafanuzi mbele ya Kamati za kudumu.

Eneo la pili Mhe. Naibu Spika, ni kutofuatwa kwa sera au sheria katika masuala mbali mbali yanayohusiana na mapato na matumizi ya fedha za umma. Mhe. Naibu Spika, eneo hili linahitaji kutolewa maelezo au ufafanuzi na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, juu ya utekelezaji wake na kwa heshima kubwa nitafanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya mwaka 2012 imetoa maagizo manane ili yatekelezwe na serikali kupitia Ofisi ya Rasi Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo au taasisi nyengine za serikali.

Kwa heshima kubwa naomba kutoa maelezo juu ya utekelezaji wake kama ifuatavyo.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, kupitia ripoti ya *CAG* na kupata maelezo kutoka kwa Wahasibu kwa nini kuna upotevu wa matumizi yasiyo na stakabadhi. Utekelezaji wake Mhe. Naibu Spika, ni kwamba mapitio ya ripoti ya *CAG* yamefanyika na kumeonekana kuwa kuna sababu tofauti kwa kila taasisi. Ni vyema kila afisa muhasibu *accounting officer* akawajibika kwa mujibu wa sheria ya fedha za umma, sheria nambari 12 ya mwaka 2005. Kifungu nambari 8 cha sheria ya fedha za umma inamtaka afisa mhasibu kuwajibika kwa matumizi ya mapato ya taasisi yake anayoyasimamia. Mhe. Naibu Spika, hapa ndio pale walipowataka Waheshimiwa Mawaziri, kuja na wao kutoa ufafanuzi juu ya maeneo ambayo niliyaeleza katika kifungu cha kwanza.

Agizo la Pili Mhe. Naibu Spika, mikopo na misaada nayo pia ikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali.

Utekelezaji wake ni kwamba utaratibu umeandaliwa na sasa miradi yote inayofadhiliwa kwa misaada na mikopo inakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali. Hatua hii ni utekelezaji wa kikatiba kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Agizo la Tatu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kuhakikisha kuwa kila taasisi ya serikali, inafunga na kuwasilisha hesabu zake kwa mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali, kwa mujibu wa sheria ya fedha.

Utekelezaji ni kwamba kwa kuwa suala la kuwasilisha hesabu za taasisi ni sehemu ya uwajibikaji wa sheria ya fedha za umma, ya mwaka 2005 kifungu nambari 24(2), kutowasilisha ripoti kwa wakati ni kosa na adhabu yake imeelezwa katika kifungu cha 38 cha sheria hii. Hatua hii ni utekelezaji wa sheria ya fedha nambari 12 ya mwaka 2005.

Mimi ninawaomba sana wale ambao hawatowasilisha hesabu zao kwa wakati, ni vyema tutakapopata taarifa zao basi itabidi tuwachukulie hatua kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, agizo la Nne ni kwamba Shirika la (*PBZ), People's Bank of Zanzibar, ZSSF*, na *Zanzibar Insurance* wanachelewa kuwasilisha hesabu zao na wengine hawatoi fursa ya kukaguliwa hesabu zao na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali.
Mhe. Naibu Spika, utekelezaji ni kwamba kikao cha pamoja baina ya taasisi hizo na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali, pamoja na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kimefanyika na taasisi zote hizo zinawasilisha hesabu zao kwa mujibu wa makubaliano, na sasa zitaanza kukaguliwa na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali.

Hatua hii Mhe. Naibu Spika, ni utekelezaji wa kikatiba kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu nambari 25 cha sheria ya fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2005. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba taasisi zote zina wajibu sasa kupeleka mahesabu yao, kama tulivyokubaliana na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu na nitafuatilia suala hili.

Mhe. Naibu Spika, agizo la tano ni kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima. Hapa nataka niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Katika bajeti ya mwaka jana wameviona vifungu ambavyo kwa kweli kutumika kwake ingekuwa hakuna lazima na wakanishauri kwamba pesa zile niziondowe na pesa zile nimeziondoa na ndio iliyotusaidia kupeleka *down payment*, kwa ajili ya ununuzi wa meli yetu mpya.

Kwa hivyo, utekelezaji ni kwamba miongozo ya matumizi imekuwa ikitolewa na hatua zaidi zitachukuliwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Agizo la Sita Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kwa kuwa serikali inatenga fedha kwa ajili ya malipo ya maji na umeme kwa kila taasisi, basi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo isimamie ulipaji wake kutoka katika bajeti za taasisi husika.

Utekelezaji wake ni kama ifuatavyo. Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imechukua hatua ya kulitaka Shirika la Umeme kufunga mita za TUKUZA, kwa taasisi zote za serikali ili kuhakikisha malipo ya umeme yanafanyika kwa wakati. Hatua hii itaimarisha uwajibikaji wa Mawizara katika usimamizi wa matumizi.

Agizo la Saba Mhe. Naibu Spika, ni kuandaliwe utaratibu kwa mashirika ya serikali kufanyiwa marekebisho moja baada ya moja ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi, au kuyafunga kama yataonekana yanajiendesha kwa hasara na hayawezi ushindani.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa agizo hili ni kama ifuatavyo. Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, imeyafanyia tathmini mashirika yake, yakiwemo Shirika la Utalii na Shirika la Magari. Aidha, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inaendelea na uchambuzi kwa mashirika yake yote yaliyobakia, yale yatakayobainika kwamba hayawezi tena ushindani, basi tutayawasilisha serikalini ili kuona kwamba tunayafunga na yale yatakayobainika kwamba yanaweza ushindani lakini yanahitajia kidogo kusaidiwa basi tutayasaidia, ili yaweze kuendelea na ushindani.

Mhe. Naibu Spika, agizo la Nane na la mwisho ni kama ifuatavyo. Kodi za nyumba za serikali zifanyiwe mapitio, serikali inatoa kodi ndogo sana kulinganisha na soko, baadhi ya watu wamepanga kutoka serikalini na wao wamepangisha kwa bei kubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa agizo hili ni kama ifuatavyo. Mapitio ya kodi za nyumba kwa ngazi za wizara husika yamefanyika kama yalivyotolewa taarifa jana na Kaimu Waziri ni kwamba tayari tumeshafanya mapitio kodi zote za nyumba za serikali. Viwango hivyo vipya vinatarajiwa kutangazwa katika bajeti ambayo tutaisoma mwaka 2013/14. Kodi hii itaongeza mapato ya serikali yasiyo ya kodi.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa na taadhima sasa naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Aidha, niishukuru sana Kamati ya

kudhibiti hesabu za serikali na mashirika yetu ya Baraza hili tukufu kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Vile vile nichukue fursa hii niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili kwa namna ambavyo wanaendelea kufanya wajibu wao kwa nia ile ile ya kuwatumikia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu hii imefanya wajibu wake kwa mujibu wa Katiba, sheria na taratibu ambazo sisi wenyewe tumejipangia katika Baraza letu hili. Nataka niseme kwamba kazi waliyoifanya ni nzuri, nawaomba waendelee kufanya kazi hiyo kwa kuhakikisha kwamba matumizi yanakwenda vizuri kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji na ushauri, mapendekezo ya *PAC* ya mwaka wa fedha 2011/2012 katika wizara yangu kulikuwa na hoja kama 6 naomba nitoe ufafanuzi kama ufuatao.

Hoja ya kwanza ilikuwa inahusu fedha shilingi milioni 2,050,000 ambazo hazina vielelezo.

Kamati inapendekeza fedha hizo ambazo hazina vielelezo zirejeshwe kwa kukatwa mishahara ya Afisa Mhasibu na watendaji wake, ili ihakikishwe fedha hizo zinarudishwa.

Utekelezaji wa Wizara. Wakati kamati ilipokuja kufanya uchunguzi wa hoja hii ambayo ni hoja nambari 13.1.3 vielelezo vilikuwepo zikiwemo tiketi za safari ya kwenda na kurudi, fomu za maombi ya safari katika vocha husika, kilichokosekana ni kielelezo kimoja tu ambacho ni risiti ya usafiri wa ndani kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma yenye thamani ya shilingi 70,000/-. Hata hivyo, vielelezo hivyo vimefuatiliwa kwa wahusika na kwa sasa hoja hiyo inavyo vielelezo vyote vinavyohitajika.

Hoja ya pili Mhe. Naibu Spika, kukosekana kwa Daftari la Kuhifadhi Mali za Kudumu na thamani yake. Kamati inazitaka Ofisi za Makamu wa Pili wa Rais, Tume ya Uchaguzi na Baraza la Wawakilishi kuwa na Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu na Thamani yake na daftari hilo liwe linatumika.

Utekelezaji, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Tume ya Uchaguzi na Afisi ya Baraza la Wawakilishi tayari zimeanzisha daftari hilo na linatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Hoja ya tatu kutokufanyakazi kwa Kamati ya Ukaguzi (*Audit Committee*). Kamati inaitaka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ihakikishe kuwa kamati hiyo inafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji ni kwamba Kamati ya Ukaguzi (*Audit Committee*) ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tayari inafanyakazi.

Hoja ya nne uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka. Kamati inazitaka Ofisi za Makamu wa Pili wa Rais, Tume ya Uchaguzi na Afisi ya Baraza la Wawakilishi kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka ziwasilishwe kwa wakati kwa mujibu wa sheria.

Utekelezaji Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Tume ya Uchaguzi na Afisi ya Baraza la Wawakilishi itahakikisha kwamba kuanzia sasa hesabu zake za mwisho wa mwaka zinafungwa na kuwasilishwa serikalini kwa wakati kama sheria inavyotaka.

Hoja ya Tano Mradi wa Ujenzi wa Baraza la Wawakilishi Pemba. Kamati inasisitiza kupatikana haraka kwa Hati Miliki ya majengo yote ya Baraza la Wawakilishi na jengo jipya kufanyiwa marekebisho ya kasoro zote zilizojitokeza. Hatua ya utekelezaji, hatua za marekebisho ya kasoro zilizojitokeza katika jengo jipya la Baraza la Wawakilishi zimeanza kufanyiwa kazi, kwa upande wa Hati Miliki za majengo ya Baraza, juhudi bado zinaendelea ili kupata hati hizo.

Hoja ya Sita ambayo ni ya mwisho Mhe. Naibu Spika, kuhusu fedha za wahisani kutooneshwa katika hesabu za mwisho wa mwaka. Serikali ielimishe wahisani kwa maendeleo, umuhimu wa taarifa za fedha, ili uweze kufahamika uwazi wa matumizi halisi ya fedha za umma.

Utekelezaji serikali imekuwa ikichukua juhudi za kuwaelimisha wahisani juu ya umuhimu wa serikali kuwa na taarifa za matumizi ya fedha zote zinazotolewa kwa matumizi ya shughuli za maendeleo na kawaida, na kwa kiasi fulani kuna mafanikio katika suala hili, wahisani kupewa taarifa za fedha za misaada zinavyotumika Zanzibar, jitihada zitachukuliwa kuhakikisha kwamba hatua hii inafanikiwa kama maelekezo yalivyotolewa na Kamati.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru wewe, kamati pamoja na Baraza na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ahsante naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuelezea juu ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilikuwa na hoja au agizo moja la kutekeleza na lilitokana na hoja Nam. 15.1.2 Kuhusiana na malipo yasiyokuwa na vielelezo ya shilingi milioni 10,432,000/= ambazo walilipwa *Community Capacity Enhancement*.

Mhe. Naibu Spika, ofisi yetu hasa katika Taasisi hii ya Tume ya UKIMWI tunapata matatizo sana ya kupata stakabadhi hasa kwa sababu tunafanya kazi na watu ambao hawafahamu sheria wala taratibu za kihasibu na wapopewa maelekezo ni watu ambao wako katika *grass root*, yaani vijijini kabisa tunapeleka fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya shughuli zetu na huko ndiko stakabadhi nyingi zinakopetea na huwa hazipatikani na kupata kwake kunakuwa ni kugumu sana.

Katika hoja hii hata hivyo, Mhe. Naibu Spika vielelezo vilipatikana, lakini kamati ilionesha wasi wasi wake juu ya uhalali wa vithibitisho hivyo hasa ilivyokuwa wakati mkaguzi anakagua hapakuwepo na stakabadhi hizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ofisi yetu imetoa maelekezo kwa Tume ya UKIMWI, kwamba ihakikishe popote pale inapozipeleka fedha inahakikisha stakabadhi zinapatikana, na ni stakabadhi zilizothibitishwa ukweli na uhakika wake, kwamba malipo yamefanyika na vyenginevyo vyovyote hatua zinazofuatwa itakuwa ni kukata mshahara wa anayehusika, ili kulipa upotevu huo wa fedha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, agizo jengine lilikuwa ni kuchelewa kuwasilisha ripoti, hili limefanyiwa kazi na ninaamini kwa mwaka huu halitakuwepo.

Nakushukuru Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kupata wasaa kwa ajili ya kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya *PAC*.

Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii ya *PAC* Mhe. Omar Ali Shehe pamoja na Wajumbe wake wote. Kwa kweli mwaka uliopita tumefanya kazi nzuri ya pamoja, na mimi niwashukuru sana kupita

kila taasisi yetu na hasa pale ambapo waliona kuna matatizo ya kihesabu kufuatia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mashirika.

Baada ya shukurani mimi ninachotaka kusema Mhe. Naibu Spika, ni kwamba maoni waliyoyatoa wakati walipotembelea katika taasisi zetu, kwa kweli walitoa maoni na wakaturekebisha tunajitahidi kuyaweka sawa yale mambo yote.

Kwa hivyo, kubwa ambalo nataka kulisema kwa upande wetu walibaini matatizo katika Vikosi kwa mfano KMKM, Valantia, JKU na Zimamoto na Uokozi. Kulikuwa na matatizo ya malimbikizo ya madeni ambayo hayajalipwa na hayo tunayafanyia mkakati wa kuyalipa. Lakini kubwa zaidi Mhe. Naibu Spika, yale waliyobaini katika ripoti yao hii iliyowasilishwa na Mwenyekiti safari hii nayo pia tunayafanyia mkakati kuyatekeleza.

Kwa upande wa Baraza la Manispaa Mhe. Naibu Spika, kwamba Kamati Teule ripoti wameiwasilisha serikalini na sisi tumeipokea na kama nilivyosema kwa sababu kuna mambo mengi sana ya kisheria, basi lazima tuwatendee haki wale ambao wametajwa.

Sasa serikali inaifanyia kazi kuona kwa taratibu za kisheria twende vipi, ili tusiwatie hatiani wale ambao hawana hatia na kuwaingiza wenye hatia. Kwa hivyo, hivi sasa Kamati hiyo inakamilishwa na imani yetu pengine katika Kikao cha Bajeti tutakuja kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema namuomba Mhe. Mwenyekiti pamoja na Baraza kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba tuvumilie hii kazi si ndogo ni nzito kama wenyewe Kamati Teule walivyoifanyia kazi.

Jambo jengine kubwa ambalo limebainika Baraza la Manispaa ni suala la kufunga hesabu kwa mwaka, yaani kwa wakati. Kwa kweli suala hili tayari tumeshalifanyia kazi na tumeshalirekebisha na pia maoni yao mazuri ya kuwaonya watu wa Manispaa kwamba wafunge hesabu kwa wakati unaotakiwa ni hili jambo zuri na tumelizingatia.

Vile vile suala jengine kubwa ni kuhusu *Fixed Asset Register* watu wa Manispaa na taasisi zetu nyengine pia zimebainika kwamba zina matatizo ya kutia mali za serikali katika *Fixed Asset Register*, hili nalo tumeliona, tutalisimamia na tutalifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, matatizo kadhaa yalibainika katika Mabaraza yetu ya Miji na Halmashauri na zaidi kule kwa sababu tulikuwa na mapungufu ya wataalamu na hasa wahasibu wenye ujuzi. Sasa kwa makusudi serikali inafanya juhudi ya kuwapeleka wahasibu na Afisa Mipango wenye ujuzi, ili mipango yao na hesabu zao ziende kwa mujibu wa kitaalamu na hilo tunalifanyia kazi na maoni yote yale tumeyasikia na niseme kwamba sitoweza kuyajibu moja baada ya moja.

Lakini ninachotaka kusema Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Mwenyekiti na timu yake kila pale walipoona kuna matatizo, basi tulifunga safari ya pamoja tukaenda wakatoa maoni na tukarekebisha *on the spot*, nafikiri wenyewe walikiri kwamba mengi yale mambo tumeyaweka sawa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache natoa shukurani, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa idhini yako naomba kwanza kumshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa mashirikiano mazuri ambayo anayafanya kwa kufanyia kazi Kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mashirika na hatimaye kuandika ripoti ya Kamati na kuiwasilisha Barazani hapo baadaye.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenye ripoti ya mwaka jana tulikuwa na hoja moja tu, hoja yenyewe ni kuhusu Chuo cha Utawala wa Umma, ambayo ilikuwa inahusu masuala ya kukodi majengo ya watu binafsi kwa ajili ya kusomeshea wanafunzi wa Chuo cha Utawala wa Umma.

Kamati ilitutaka kwanza kwa nini tulikuwa tunakodi majengo ya watu binafsi. Jibu ni kwamba tulikodi majengo ya watu binafsi katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kutokana na udogo wa jengo letu la chuo liliopo pale Mizingani. Hata hivyo, kamati ilituagiza kuhakikisha kwamba tunaharakisha ujenzi wa Chuo chetu cha Tunguu, ili tuachane na utaratibu huo.

Vile vile kabla hatujakamilisha ujenzi wa chuo hicho tulifuata maelekezo ya Kamati na tuliamua kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na tukaazima majengo yao na wanafunzi wakawa wanasoma katika majengo ya serikali kabla ya kwenda katika majengo ya Chuo Tunguu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba agizo la Kamati tulianza kulitekeleza mwaka jana kwa kuweza kuachana na kukodi

majengo ya watu binafsi na kwenda katika majengo ya serikali kama vile kuzitumia skuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Na mwaka huu tumeamua kuhamia rasmi katika jengo la Chuo kule Tunguu. Kwa maana hiyo, agizo la Kamati napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba tumelitekeleza kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, ahsante. Sasa ni zamu ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria hakuwasilisha taarifa yake naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, pia namshukuru *Allah* kwa kutupa uhai na uzima. Vile vile napenda nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* pamoja na Wajumbe wa Kamati wote kwa jumla kwa kutoa miongozo sahihi na yenye muelekeo katika mawizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kulikuwa na maagizo mawili na naomba nitoe taarifa kama ifuatavyo.

Kwanza wizarani Makao Makuu Unguja, wizara imeagizwa kukamilisha Daftari la Mali za Kudumu sambamba na kuziwekea thamani angalau gharama za awali pamoja na kuzitafutia hati miliki, ili ziweze kurikodiwa katika Daftari la Kudumu kama ambavyo kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha kinavyoelezwa na hili ndilo agizo lililotolewa.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wake ni kuwa tayari wizara imeanzisha Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu za Serikali. Daftari hilo limeainisha pamoja na mambo mengine thamani za mali zenyewe. Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kuliona na kulikagua daftari hilo wakati wa ziara yao ya mwezi wa Januari, 2013.

Mhe. Naibu Spika, agizo la pili ilikuwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Afisi Kuu Pemba, agizo lilisema Kanuni ya 264 ya Kanuni ya Fedha ya Zanzibar ya mwaka 2005 inamtaka Afisa Mdhamini kuweka Daftari la Kuhifadhi Mali za

Kudumu, ambapo kwa mujibu wa ukaguzi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Pemba haikuwa na daftari hilo.

Kwa hivyo, napenda nitoe taarifa kwamba tayari Daftari la Kuhifadhi Mali za Kudumu la Serikali limeanzishwa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya mawili ambayo ndio makubwa yalikuwa yamebakia katika utekelezaji wa mwaka 2011/2012, naomba kutoa taarifa na kuwasilisha na naomba kuishukuru sana Kamati. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wizara husika haikuwasilisha kwa ukamilifu wake taarifa hii naomba tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwako na kwa Kamati ya *PAC* na hususan kwa Mwenyekiti Mhe. Omar Ali Shehe kwa msaada wanaonipa katika kusimamia shughuli za kila siku za Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya ni kubwa na ina vipengele, vitongoji na vichochoro vingi na hivyo usimamizi wake unahitaji ukaribu wa kila kitengo. Kwa kweli Kamati hii naisifu na kuishukuru kwamba imefika kila kichochoro na kupekua yale yaliyofanyika na kutushauri nini cha kufanya.

Katika ripoti iliyopita ya Kamati tuliagizwa mambo matano, ambayo naomba kuyaeleza kwa ufupi.

Kwanza kamati imetutaka kuandaa lile Daftari la Kuhifadhi Mali za Kudumu (*Fixed Asset Register)*. Mhe. Naibu Spika, tumefanya tulipofika tumeweza na kwa upande wa Pemba tumeshakamilisha na wizarani hapa inashirikiana na Wizara ya Fedha katika kuliweka kwenye mpango uliotakiwa, ambalo ndio moja katika mapungufu yaliyoelezwa na Kamati. Kwa kweli kazi hiyo inaendelea vizuri na tumewaajiri baadhi ya wafanyakazi kwa muda, ili tuikamilishe kama ilivyoagizwa.

Hoja ya pili ilikuwa ni Mpango wa Manunuzi. Mhe. Naibu Spika, mpango wa manunuzi kuupanga kwa kila mwaka huwa tunaupanga na kuweka *cash flow* kulingana na bajeti, isipokuwa mara nyengine huwa unashindwa kutekelezwa kutokana na ufinyu wa fedha kama zinavyoingia na tunavyotakiwa. Hata hivyo, tumejitahidi tumepanga kama tulivyoshauriwa na tunategemea kila siku zikienda

basi mambo yataendelea kuwa mazuri kulingana na mapato ambayo tutakuwa tunaingiziwa.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya tatu ilikuwa ni kukosekana kwa kadi za usajili wa baadhi ya vyombo. Mhe. Naibu Spika, wizara ina vipando vya aina mbili, yaani tunavyo vipando vingi vinavyopatikana kutokana na miradi ya wahisani, ambao mara nyingi zile kadi huwa bado wanazishikilia hasa ikiwa bado ziko kwenye mradi na unapokamilika mradi tukikabidhiwa mradi ule basi huwa tunakabidhiwa na zile kadi. Lakini kwa zile zilizo chini ya wizara vyote tumeshatekeleza kuvisajili kama vilivyotakiwa.

Vile vile tuliagizwa kwamba kuna magari mabovu mengi ambayo yamekaa muda mrefu na mengine kuchakaa hata kuoza bati, vizuri ni kwamba tungefanya juhudi yakauzwa. Mhe. Naibu Spika, ugumu wa suala hili kwetu ni kuwaandikia Idara ya Uhakiki Mali na wao wanakuja kufanya uhakiki na halafu wanaruhusu. Hivi sasa tayari tumeshaandika kwenye idara hiyo na tunangojea maelekezo yao na jinsi vya kufanya, huwa tunashindwa kuuza gari na halafu kuja kuambiwa tumeliuza wakati liko zima.

Hoja nyengine ilikuwa ni kuhusu *X-Ray* hasa za Pemba kuwa hazifanyi kazi vizuri na za zamani. Mhe. Naibu Spika, suala hilo ni kweli lakini tumeshazitengeneza na zinaendelea kutoa huduma kama vile pale tutakaponunua nyengine basi tutanunua zile kwa hali ya sasa ya teknolojia. Kwa hiyo, zile pamoja na uzee wake lakini ndizo tulizonazo kwa sasa na zinatusaidia.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine pia tulitakiwa kwenye ile sehemu ya *X-Ray* tufundishe wataalamu wa kufanya kazi kwenye *X-Ray*. Taarifa niliyonayo ni kwamba hivi sasa tunao wanafunzi wanne ambao wako masomoni Uganda wawili kutoka Unguja na wawili kutoka Pemba. Kwa hivyo, agizo hili tumelitekeleza kama tulivyotakiwa.

Mwisho tuliagizwa kuhusu utunzaji wa magari na hasa hayo mabovu kuweza kuuzwa au kuondolewa, ili yasiendelee kuwepo. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye hoja ya 16.3 yaani juu ya uchakavu tunawasiliana na Wizara ya Fedha, taarifa ya kuondoa magari mabovu hufikishwa kwa Mhakiki Mali.

Vile vile tuliagizwa kwamba tuwadhibiti madereva wanaopewa magari kwamba mara nyengine wanatumia ovyo. Mhe. Naibu Spika, hilo tumelifanya na tunategemea kubadilisha baadhi ya uongozi katika sehemu ile maana kuna mtu

ambaye anayesimamia, ili haya ya kudhibiti matumizi yapate utaratibu na yawe yanafahamika kama muongozo unavyotaka.

Kwa mfano, hakuna kitu ambacho madereva hawakipendi pamoja na kwamba ni sheria kama kutumia *log book* ni kitu ambacho hawakipendi hasa. Sasa juhudi tunafanya kuhakikisha kwamba magari yale wanapotumia wawe wanatumia *log book* kama utaratibu unavyotaka. Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii, pia nichukue nafasi hii kwa kuishukuru Kamati ya *PAC* chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Omar Ali Shehe kwa mashirikiano waliyotupa wakati walipokuja katika wizara yetu na sisi tulishirikiana nao vizuri. Kwa kweli sisi hoja zetu zote tulizijibu vizuri na Kamati iliridhika.

Lakini kwa faida ya Baraza hili tukufu naomba niseme kwamba tulikuwa na hoja nne na naomba nizisome kama hivi ifuatavyo.

Hoja ya kwanza ilikuwa ni kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi, ukaguzi ulibaini kwamba wizara haifanyi mpango wa manunuzi na kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu Nam. 19 cha Sheria Nam. 9 ya Manunuzi ya mwaka 2005.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilitayarisha Mpango wa Manunuzi, ili kwenda sambamba na kifungu cha Nam. 9 cha Sheria Nam. 5 ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali ya mwaka 2005.

Hoja ya pili ilikuwa ni kukosekana na thamani za Mali za Kudumu. Mhe. Naibu Spika, kuhusu utekelezaji, hali hii inatokana na baadhi ya mali tulizokuwa nazo tumezipata kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo kama vile *UN*, vile vile baadhi ya mali hizo tumezirithi kutoka hapo nyuma, pia mara kwa mara tunapokea mali kama vile magari na *computers* kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar.

Kwa kweli hali hii ilitupa ugumu sana wa kuweza kuzitathmini mali hizo na hatimaye tulikosa thamani halisi ya mali hizo. Pamoja na hayo, jitihada za makusudi tumezichukua, ili kuhakikisha mali tulizonazo tumeziingiza kwenye *Fixed Asset Register*.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeandaa mpango maalum wa kuzitia thamani mali zote za serikali na kwa kuanzia wameanza na wizara tano kati ya hizo wizara yetu haikuwemo. Lakini imani yetu ni kwamba tutaingizwa kwenye mchakato wa pili.

Hoja ya tatu ni Udhibiti wa utunzaji wa Nyumba za Wazee Sebleni. Mhe. Naibu Spika, kuhusu utelekezaji wizara imefanya jitihada kubwa kuwaenzi wazee kwa kuweza kuimarisha maeneo yao ya makaazi. Wizara tayari imeshakarabati nyumba moja, ukumbi mkubwa, kujenga ukuta kuzunguka eneo lote la Nyumba za Wazee, tumekarabati vyoo, tumejenga msikiti, tumerekebisha mtandao wa maji kwa kuchimba kisima kipya na kujenga mnara wa kuweka matangi ya maji. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wizara itaendelea kuzifanyia matengenezo nyumba hizo kadri ya upatikanaji wa fedha utavyoruhusu. Mhe. Naibu Spika, kwa kuongezea hapa Kamati ilipokuja kwenye Nyumba za Wazee Sableni ilifurahishwa sana na kazi tuliyoifanya. *(Makofi)*

Hoja ya mwisho ya nne ni kuhusu Umiliki wa kiwanja katika kijiji cha Muungoni Wilaya ya Kusini Unguja, ukaguzi umebaini kwamba wizara inamiliki kiwanja katika kijiji cha Muungoni Wilaya ya Kusini Unguja, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Vijana. Kwa kweli kiwanja hicho bado hakijatumika kama ilivyokusudiwa na baadhi ya wananchi hawajalipwa malipo yao ya fidia kwa kuchukuliwa maeneo yao. Mhe. Naibu Spika, kuhusu utekelezaji ujenzi huu awali ulikuwa ufadhiliwe na *ILO*, hata hivyo *ILO* walibadili muelekeo wa ujenzi wa vituo hivyo.

Maelekezo ya serikali juu ya suala la ujenzi wa umiliki wa vituo vya Ujasiriamali vibakie chini ya udhibiti na usimamizi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa mujibu wa makubaliano na uongozi wa wilaya wanaopaswa kulipwa ni wale wenye vipando vya kudumu na sio vipando vya muda, hivyo watalipwa kabla ya ujenzi.
Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali za Kamati yetu ya *PAC* ya Baraza lako tukufu.

Kwa hivyo, na mimi napenda niipongeze sana Kamati kwa namna ambavyo inavyotusaidia sisi Mawaziri katika usimamizi wa shughuli mbali mbali zilizomo katika wizara zetu. Mhe. Naibu Spika, kama si juhudi zao kubwa wanazozifanya kupitia na kukagua mambo mbali mbali, kwa kweli Mhe. Naibu Spika utawala

bora katika nchi yetu ungekuwa na matatizo sana. Kutokana na hali hiyo, naipongeza sana na hasa Mwenyekiti wake kwa sababu ana uzoefu mwingi Mhe. Omar Ali Shehe katika suala hili nampongeza anafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa katika Wizara yangu kulikuwa na hoja kumi na moja katika Wizara na Taasisi mbali mbali.

Hoja ya kwanza kuhusu fedha za wahisani wa maendeleo, kamati ilitushauri kwamba kuwe na utaratibu mzuri kwa Wizara za Serikali kwa ujumla kufanya mawasiliano na wakawaelewesha wafadhili haja ya kutoa taarifa za matumizi ili kutimiza matakwa ya sheria zetu. Ni kweli Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo hili na hasa miradi inayohusu na baadhi ya wafadhili kwa kweli wengine hawako wazi. Lakini tunashukuru baada ya maelekezo haya ya kamati, na baada ya mashauriano na wafadhili sasa utaratibu tumekubaliana kwamba lazima utaratibu wa kifungu cha 24 cha sheria ya fedha kifuatwe na hili tumekubaliana sana.

Kuhusu hoja ya pili kukosekana kwa daftari la kuhifadhia mali yaani *fixed asset register* hoja hiyo tumeifanyia kazi na maoni ya kamati katika suala hilo sasa liko vizuri na wao walipokuja katika ukaguzi wao mara hii wameona kwamba angalau pale makao makuu ya Wizara kuna *fixed asset register* ambalo pamoja na miongozo waliotoa midogo midogo lakini liko vizuri sana tunashukuru sana kwa maoni yake haya.

Hoja ya tatu ilikuwa vifaa ambavyo havikuingizwa katika hesabu za mwaka, maoni ya kamati ilikuwa kwamba kutoorodhesha vifaa katika hesabu ni kinyume cha sheria na kwa hivyo tunasisitizwa umuhimu wa kufuata sheria ili kuepuka upotevu wa mali za serikali kiholela. Kipengele hiki nimekifanyia kazi na kwa kiwango kikubwa mali nyingi ya pale Wizarani tayari zimeingizwa na muongozo waliotoa juzi nao ushafanyiwa kazi.

Kuhusu hoja ya nne kucheleweshwa kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka ni kweli tatizo hili lilikuwepo siku nyingi lakini hasa sasa hali imetangamaa vizuri.

Kuhusu ufafanuzi wa miradi ya maendeleo kwamba kulikuwa na miradi ya viwanja vya michezo vya Amani na Gombani ambao kwa kweli kulikuwa hakuna ufafanuzi mzuri, ambavyo vilitumia pesa nyingi mabilioni na mchango wa wahisani kwa mabilioni. Kwa hivyo maoni ya kamati ilisisitiza kwamba, kwa kuzingatia sheria katika matumizi ya fedha hususan katika miradi ya maendeleo eneo ambalo nyingi taratibu za matumizi hazifuatwi lakini pia umuhimu wa

kuvitunza viwanja hivyo vimeigharimu taifa fedha nyingi na pia hazina kubwa kwa taifa.

Mhe. Naibu Spika, suala hili kama nilivyosema awali baada ya kukaa na wenzetu wanaotusaidia tumekubaliana vizuri katika suala hili na tumefika pahali pazuri. Kuhusu utunzaji wa viwanja tunajitahidi, kiwanja cha Amani baada ya matengenezo yale kiko vizuri, na kiwanja cha Gombani nacho baada ya kuwekewa nyasi bandia tunajaribu kuitunza hasa baada ya maoni haya ya kamati.

Kuhusu hoja ya sita Kamisheni ya Utalii kukosekana kwa orodha ya mali za kudumu za Kamisheni, Hoja hii ilikuwepo huko nyuma na imefanyiwa kazi na sasa hali ni nzuri na katika ziara ya kamati ya mwaka huu wao wenyewe wamejionesha kwamba kumekuwa na improvement kubwa.

Kuhusu tatizo la kupatikana kwa takwimu sahihi za watalio Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo ambalo tumekuwa nalo na bado Mhe. Mwenyekiti suala hili tunalo hadi leo na kwamba tumelifanyia kazi baada ya maoni yenu ya kamati na maelekezo yenu na tumeunda kikosi kazi cha wizara nne. Sisi Kamisheni ya Utalii, Wizara ya Fedha hasa *ZNB* pamoja na watu wa Wizara ya Fedha wenyewe pamoja na watu wa uhamiaji tumeshafanya vikao mara nyingi na tunaangalia utaratibu wa kileo katika kuhakikisha kwamba watalii wanaokuja pale airport basi wanahesabiwa kwa mitambo ya electronic.

Tumetoa timu imekwenda *TANAPA* wenzetu wamefanya kazi hiyo siku nyingi, wamefaulu kujua watalii wanaoingia pale sasa timu ya wataalam ya Kamati hizi za Tasisi nne imerudi imeandika ripoti yake nzuri kwa hivyo tunawasiliana na baadhi ya taasisi za kifedha, vifaa hivyo wako tayari kutupa na katika mwaka ujao wa fedha vifaa hivi vitakuwepo pale *airport* na bandarini, kwa hivyo mtalii yoyote anayeingia hapa tutakuwa tuna utaratibu wa ki-*electronic* ya kisasa ki-*digital* kuona kwamba kila mtalii anaingia nchini anajulikana.

Tunakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na Kamati yako kwa kutupa maoni haya na kwa kweli yametusaidia sana kutusukuma kulifanyia kazi kwa umuhimu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, agizo namba nane kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Utalii hasa kuhusu madeni ya wanafunzi ambayo hayakuingizwa katika taarifa ya fedha. Mhe. Naibu Spika, kamati ilitupa agizo kwa uongozi wa Chuo kufuatiliwa wale wote wanaodaiwa. Kazi hiyo tumeifanya vizuri na kwa kiasi Fulani tumepata mafanikio makubwa.

Hoja ya tisa ilikuwa ni Hoteli ya Bwawani kuhusu udhaifu wa udhibiti wa ndani, Mhe. Naibu Spika, maoni ya kamati ilitoa wito kwa Wizara kuandaa utaratibu mzuri wa utoaji wa msamaha ili kuepusha wajanja kuitumia fursa hiyo vibaya. Mhe. Mwenyekiti muongozo umetolewa na Wizara na sasa kuna utaratibu unaoeleweka wa nani ambaye ana uwezo na mamlaka kutoa misamaha hii.

Hoja nambari kumi namoja ilikuwa ni kuhusu malipo yasiyokuwa na vielelezo ya shilingi milioni tano, laki nane arubaini moja elfu kwa kweli hili lilikuwepo lakini ilipopita kamati ilielezwa hivyo vilionekana, lakini pamoja na hayo kamati ilitoa maoni kwamba kitendo hiki kinapingana na kanuni za fedha na ni kweli na kwa hiyo ilitaka Wizara ilishughulikie suala hili tayari mimi nimekaa na Katibu Mkuu na Watendaji wengine na hasa internal *auditors* kwa kweli suala hili limefanyiwa kazi vizuri sana.

Kuhusu hoja nambari kumi na moja inayohusu msamaha unaotolewa na Hoteli ya Bwawani, maoni ya kamati inapendekeza kuweka utaratibu mzuri wa utoaji wa misamaha hiyo Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika kipengele kilichopita kwamba utaratibu mzuri umewekwa na Alhamdulillahi sasa kuna utaratibu mzuri ambao unaeleweka.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala la mwisho ambalo linahusu eneo la kufulia *laundry* hali sasa iko vizuri, maoni ya kamati tumeyazingatia vizuri na tayari laundry hilo sasa linamilikiwa na wenyewe hoteli ya Bwawani sio taasisi ya mtu binafsi.

Mhe. Naibu Spika, hayo ndio yaliyokuwa maoni au maelekezo ya kamati kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na kama nilivyosema awali kwamba ninashukuru sana kamati kwa kazi ambazo wanazozifanya na Mhe. Mwenyekiti kwa sababu muda wa kamati unafikia mwisho mimi ningeshauri kama inawezekana kwa sababu ya uzoefu mkubwa walioupata kamati hii katika kufanyia kazi kama itawezekana wote kurudishwa kuendelea na Kamati katika kipindi kijacho ni jambo ambalo itaisaidia sana serikali kwa sababu wanao uwezo mzuri, wamepata uzoefu mkubwa Mhe. Naibu Spika, ukilinganisha na watu wengine wanaopoteza muda sana kupata tena uzoefu.

Kwa hivyo kipindi kinachokwisha miaka miwili na nusu ningetoa ushauri kama unaweza kukubalika basi iendelee kutufanyia kazi kupitia katika taasisi zetu mbali mbali za mawizara.

Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: (Kny. Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati): Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wizara husika haijawasilisha kwa ukamilifu wake taarifa kuhusu hoja hii naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: (Kny. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa katika maelekezo na utekelezaji wa maagizo Wizara ya Kilimo haikuwa na agizo la kujibu kwa hivyo haikuwasilisha taarifa kutokana kwamba haikuwa na agizo la kujibu. Kwa hivyo naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Afya: (Kny. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko) Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena naomba kuwasilisha taarifa ya hoja za Kamati ya *PAC* ya Wizara ya Biashara kwa niaba ya Waziri wa Biashara.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia sote kufika hapa tukiwa wazima na afya njema na kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa. Aidha naomba kuchukua fursa hii adhimu kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo ya Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijatoa ufafanuzi wa hoja hizo naomba kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* Mhe. Omar Ali Shehe mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake pamoja na wajumbe wote wa Kamati. Mhe. Naibu Spika, usimamizi mzuri wa raslimali na udhibiti wa hesabu za serikali katika Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kwa sehemu kubwa unatokana na ushauri pamoja na miongozo inayotolewa na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti wa Hesabu za Serikali. Ushirikiano uliopo baina ya Kamati na Wizara unatufanya kuweza kutimiza majukumu yetu yakiwemo ya kutunza na kudhibiti mali na raslimali za serikali kwa mujibu wa taratibu zilivyo.

Mhe. Naibu Spika, aidha kwa heshima kubwa napenda kuwashukuru na kuwapongeza wajumbe wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi, kwa jinsi wanavyotupatia ushirikiano wa dhati kwangu mimi binafsi pamoja na watendaji wa Wizara yangu yaani Biashara kwani maelekezo ya Baraza hili tukufu yanaisaidia kupata mafanikio katika utekelezaji wa majukumu na malengo yake. Nawaomba waheshimiwa wajumbe muendelee kushirikiana na Wizara yangu na kutuunga mkono ili tuweze kutekeleza majukumu tuliyopangiwa kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya shukurani naomba kueleza kwamba katika ripoti za kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali ya Baraza Wawakilishi kwa mwaka 2011/12 wizara iliagiza kufanya jitihada kuhakikisha kwamba kiwanda kinaendeshwa vizuri na kwa ufanisi ili kilete tija kwa taifa. Ninachoamini kiwanda hiki na cha Makonyo. Naomba uniruhusu kutoa maelezo ya utekelezaji wa agizo hilo kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Kamati imeagiza uongozi wa Kiwanda kufanya jitihada kuhakikisha kwamba Kiwanda kinaendeshwa vizuri na kwa ufanisi ili kuleta tija kwa taifa. Katika jitihada za kuhakikisha kwamba kiwanda kinaendeshwa kwa ufanisi mambo yafuatayo yamefanyika. Kutekeleza mpango wa mageuzi wa *ZSTC* yaani reform program ikijumuisha mageuzi ya Kiwanda cha Makonyo. Hivyo kiwanda kinafanyiwa upembuzi yakinifu na Shirika la Viwanda Tanzania kwa ajili ya kufanya tafiti kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:

Mifumo ya uzalishaji kwa kiwanda, teknolojia inayohusika, kupendekeza hatua za kuchukuliwa.

Kwa upande wa biashara kiwanda kimeanza kutumia vifunganisho maalum vya mafuta ya makonyo kwa uzito wa gram 100, gram 50, gram 20 na gram 10. Biashara hiyo itaweza kuleta faida kubwa kwa kiwanda badala ya kuuza mafuta yote kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, nichukuwe fursa hii na mimi kukushukuru lakini vile vile nichukuwe fursa hii kuishukuru Kamati ya *PAC* kwa juhudi zao za kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda sawa.

Kwa upande wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, hakukuwa na makubwa kwa kweli kama Wizara yenyewe ilivyo, hoja kubwa ilikuwa ni suala la matumizi juu ya mradi wa *artificial insemination* yaani mradi wa kupandisha ng'ombe sindano. Wizara imetoa ufafanuzi uliohitajika pamoja na kuwasilisha baadhi ya vielelezo vilivyohusika. Lakini maelezo ya kamati kuhusiana na mradi huo wa upandishaji wa ng'ombe kwa njia ya sindano, unaelezwa kwamba kutumia kwa fedha wa ununuzi wa madume, kamati imehitaji kupatiwa uthibitisho zaidi wa vielelezo na gharama za ununuzi wa madume haya.

Aidha kamati imeelezwa kwamba wananchi walifaidika kwa kweli na mradi huo ni mkubwa kwa Unguja na Pemba na hivyo inahitaji kupata muda wa kuwatembelea baadhi yao ili kuona kwa kiasi gani wamenufaika.

Pamoja na yote maoni ya kamati ni kwamba kamati inahitaji muda wa ziada kukagua mradi ili iweze kufikia maamuzi yanayofaa. Aidha inahitaji muda wa ziada vile vile kufatilia maamuzi ya mahali halisi ya Wizara hii kwa mwaka huo.

Wizara haikuwa na pingamizi na maelezo yote kuhusiana na makadirio na hali halisi ya fedha ya matumizi ingawaje haikuweza kutoa uchanganuzi wa kina juu ya namna fedha hizo ilivyozitumia kutokana na kutokufahamu utaratibu gani kamati ilihitaji katika kuwasilisha taarifa hizi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio iliyokuwa hoja kubwa na kwamba Kamati itahitaji muda zaidi na kufatilia jinsi gani matumizi ya mradi huo yalivyoenda, sina zaidi.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata wasaa huu kuja kuwasilisha na kutoa majawabu ya hoja ambazo kamati iliwasilisha.

Kwanza nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa wote wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya na jinsi walivyotushauri. Lakini pia naomba nieleze kwa ufupi kwamba hoja hizi zilizokuja zilikuwa mwaka 2010/2011wakati Wizara hii haipo na baadae ikawepo. Kwa hivyo ilikuja katikati kwa hivyo ni taarifa ambazo zinahusu 2010/2011.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na hoja za kimsingi kama 6 ambazo tuliwasilishiwa. Tatizo kubwa ambalo Kamati imeonesha na ni kweli tumeliona hilo ni utaratibu wa kukosekana vielelezo hasa katika shughuli za safari za ndani na zile za nje. Na tatizo jengine suala la uhaulishaji na ununuzi wa vifaa kama vya Honda na badala kutengenezwa magari.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kufatilia kwa makini nina furaha kusema vielelezo vyote hivyo viliwasilishwa hapa Barazani na kurekebisha zile kasoro za hapa na pale. Hata hivyo kulikuwa na agizo jengine ambalo tulipewa suala zima la mikopo nalo Mhe. Naibu Spika, tumechukua juhudi ya kufatilia mikopo hiyo. Tatizo la mikopo hiyo Mhe. Naibu Spika, ni ile mikopo hasa ya AK na JK ambayo ilikuwa

inasimamiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar lakini hivi karibuni tumekuwa na mazungumzo ya karibu ili kuhakikisha kwamba kasoro hizo tunazirekebisha na fedha hizi tunatarajia Wizara itasimamia wenyewe.

Lakini hata hivyo kuna maendeleo makubwa ya urejeshaji wa mikopo hii, agizo ilikuwa ikifika 2013 mwisho basi tujitahidi kwamba fedha hizi tuzirejeshe. Tutajitahidi kadri itakavyowezekana kwa kushirikiana na waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Masheha wetu huko ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinarudi.

Mhe. Naibu Spika, tunakiri kulikuwa na tatizo la kukosekana vielelezo kama alivyosema awali lakini hatimae vielelezo hivyo vilipatikana na vimewasilishwa kunakohusika. Tatizo la kutokufata taratibu za uhaulishaji wa fedha tumeligundua la laki tatu na sitini na tano na suala hilo totalirekebisha kutokana na taratibu za sheria zilivyo.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, nataka kutoa maelezo mafupi kuhusu hoja moja ambayo imejitokeza suala zima la fedha hizi hasa za ununuzi kwa nini tumefanya hivyo.

Katika mwaka 2010/2011 Wizara chini ya Kamisheni ya Kazi na Idara ya Ushirika ilikuwa na bajeti ya shilingi nne mia saba na sabiini elfu na sabiini na sita kwa ajili ununuzi wa vipando. Jumla ya shilingi mia mbili na sitini zilitumika kununua baskeli mbili, vielelezo viliwasilishwa. Kwa kuwa Wizara ilikuwa mpya kati ya jumla ya shilingi milioni nne laki tano na kumi arubaini na sita zilizobaki, basi shilingi hizo zilitumika kufanya matengenezo ya magari manne ambayo yamesaidia sana kupunguza tatizo la usafiri lililokuwepo na vielelezo vyote viliwasilishwa.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru.

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali): Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kuendelea kuturuzuku uhai na afya iliyotuwezesha kuendelea kuhuduhuria vikao vya Baraza na tukaweza kushiriki mambo mbali mbali kwa nia ya kuwatumikia wananchi wenzetu na kushirikiana na Serikali yetu kwa ajili ya kujenga na kuiendeleza nchi yetu. Aidha, naomba pia nikushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii muhimu ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa nia ya

kuwasilisha ripoti ya kazi za Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi (*P.A.C*) kwa mwaka 2013.

Mhe. Naibu Spika, uwasilishaji huu unafanyika wakati ambapo uhai wa Baraza letu la Nane uko katikati ya uhai wake wa miaka mitano (2010-2015). Wahenga walisema "Nyota njema huonekana alfajiri kwa kuadhimisha kipindi hiki, kwa niaba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*P.A.C*), naitumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Spika wa Baraza hili kwa namna anavyosimamia na kuliongoza vyema Baraza letu hili ambalo ndio ngome ya wananchi wa Zanzibar.

Nadhani Waheshimiwa Wajumbe mtakubaliana name kwamba, kutokana na Uongozi uliojaa hekima, ujasiri, uadilifu na uaminifu wa Mhe. Spika (Mhe. Pandu Ameir Kificho), Baraza letu sasa sio tu limejijengea heshima mbele ya macho ya Wazanzibari, bali pia limeonekana kuwa kweli ni tegemeo na kimbilio la Wazanzibari, kwa namna linavyotekeleza vyema majukumu yake, ikiwa ni pamoja na kuisimamia serikali. Aidha, kwa niaba ya Kamati, naomba nimpongeze Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, pamoja na Maofisa wake kwa namna wanavyotekeleza vyama majukumu yao licha ya mazingira magumu pamoja na changamoto mbali mbali zinazowakabili kiutendaji.

Mhe. Naibu Spika, kazi ya Kamati haikuwa rahisi, ilihitaji muda wa ziada, ushauri na maelekezo ya kitaalamu yatokayo nje ya Kamati katika kufanikisha majukumu yake. Katika hili naomba kwa mara nyengine tena kumshukuru Mhe. Spika, kwa kukubali kuipa muda wa ziada na kukubali kukutana mara kwa mara na Mwenyekiti wa Kamati na kumpa maagizo na maelekezo yaliyopelekea Kamati kufanikisha majukumu yake. Kadhalika tunamshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa ukaribu wake kwa Kamati yangu. Ukaribu ambao ulituwezesha kupata ushauri na miongozo ya mara kwa mara iliyotusaidia sana kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu kwa urahisi na ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, yote yaliyowezekana yalitokana na ari, Umakini na Mshirikiano ya Wajumbe wa Kamati, kati yao na Mwenyekiti wao, kati ya Kamati na katibu wa Kamati. Sio siri kwamba, baadhi ya siku Wajumbe wa Kamati ya *PAC* walifika Barazani saa 1:30 Asubuhi na kurudi kazini majumbani kwao nyakati za usiku. Naomba kabla ya kuwatambua Wajumbe wa Kamati yangu, niwashukuru sana kwa mashirikiano makubwa yaliyofanikisha kazi yetu pamoja na Kamati nyengine zote za Baraza hili ambapo ilijengea kulijengea heshima kubwa Baraza letu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati yangu kama ifuatavyo:

1. Mhe. Omar Ali Shehe - Mwenyekiti
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Juma Abdalla - Mjumbe
4. Mhe. Farida Amour Mohammed - Mjumbe
5. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Mjumbe
6. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad - Mjumbe
7. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman - Mjumbe
8. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Mjumbe

Aidha, Mhe. Naibu Spika, kazi yetu haingeliwezekana bila ya uratibu wake na usimamizi wake kutoka kwa Makatibu wetu. Kwa heshima, pia naomba niwatambue Makatibu wa Kamati ambao ni:

1. Ndg. Amour Mohamed Amour na
2. Ndg. Othman Ali Haji

Mhe. Naibu Spika, nalazimika kuwapongeza sana Makatibu hao, kwani pamoja na majukumu mengine mengi ambayo afisi yako imekuwa ikiwapa mara kwa mara, lakini wamejitahidi kadri ya uwezo wao kuhakikisha kwamba, shughuli zetu za kamati zinakwenda kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka huu 2012/2013, Kamati yangu ilizifanyia kazi jumla ya Ripoti tano za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama zifuatazo:

1) Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali, kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

2) Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali, kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

3) Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

4) Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Udhibiti na Uhifadhi wa Mali za Kudumu za Serikali, kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

5) Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Miradi ya Maendeleo ya Wananchi na Miradi ya *TASAF*, kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mhe. Naibu Spika, ripoti zote tano zilikuwa na jumla ya Hoja 117. Napenda niliarifu Baraza lako tukufu kwamba, Kamati yangu ilikwenda kwenye Taasisi zote zilizohusika na Hoja na ilizifanyia kazi hoja zote 117, kwa kuwahoji Maofisa Wahasibu (*Accounting Officers*) na wale wote waliolazimika kujibu. Katika mahojiano, jumla ya hoja 162 zilipata majibu. Jumla ya hoja 65 majibu yake yalikubaliwa na Kamati, jumla ya hoja 97 majibu yake hayakuiridhisha Kamati ama yalikataliwa kabisa, ambapo Jumla ya hoja 15 majibu yake hayakukamilika kwa kutopatikana Wahusika au Kamati haikupata taarifa ya kina ya hoja hizo, na inahitaji muda wa ziada kuzifuatilia.

YATOKANAYO NA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU:

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyotangulia kueleza awali kuwa, kwa mwaka huu Kamati yangu ilizifanyia kazi jumla ya ripoti tano tofauti. Mbili kati ya hizo zilihusu Ukaguzi wa Hesabu (*Financial Auditing Reports*) na ripoti tatu zilihusu ukaguzi Yakinifu (*Value for Money Auditing Reports*), kwa miradi ya taasisi za Serikali, Uhifadhi wa Mali za Kudumu za Serikali, pamoja na Miradi ya Wananchi na ile miradi ya *TASAF*. Mhe. Naibu Spika, Ripoti ya Kamati ihusianayo na majibu ya hoja mbali mbali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, zimo katika Kitabu mlichopewa Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, kitabu husika cha Ripoti ya Kamati ya *P.A.C* ni hii iitwayo ‘Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika, *P.A.C*, kwa mwaka 2012/2013. Ripoti ambayo ukubwa wake ni sawa na Ripoti zote Sita za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, imekusanya Ufafanuzi wa Ripoti Tano za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kutoka ukurasa wa 6 hadi ukurasa wa 187.

Mhe. Naibu Spika, katika Ripoti zetu hizi, kwanza tumeeleza Hoja husika ambayo ni kama ilivyoelezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Pia baadae tumeeleza maelezo ya wizara ama taasisi husika kuhusiana na wao wanatoa ufafanuzi gani juu ya hoja ya Mdhibiti iliyotolewa dhidi yao. Aidha, baadae tumetoa Ufafanuzi wa Kamati, kwa kuita ‘Maelezo ya Kamati’ na hatimae Maoni ya Kamati yanayoelezea maelekezo ya Kamati kwa kutoa Mapendekezo ama Maagizo ya kwa Serikali ama Taasisi husika.

Mhe. Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba, Wajumbe wa Baraza wamepata muda wa kutosha wa kuzipitia hoja mbali mbali, majibu ya hoja pamoja na maoni ya Kamati kuhusiana na hoja husika. kwa hivyo, nitakachokifanya hapa Mhe. Naibu Spika, ni kueleza muhtasari wa Hoja zilizomo katika kila Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu pamoja na Mapendekezo ya Kamati kwa Serikali.

Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za miaka 2009/2010 na 2010/2011.

Mhe. Naibu Spika, katika hali ya kuangalia hali ya ukaguzi wa mahesabu katika Taasisi za Umma, Kamati inaitumia ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu ya mwisho kutoka kwa Mdhibiti-ya mwaka 2010/2011 kama ni kigezo na kipimo cha kubaini maendeleo ya ukaguzi na uwajibikaji katika nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Katika ripoti hiyo, kuna sura zifuatazo:

HALI YA UKUSANYAJI WA MAPATO NCHINI KWA MWAKA 2009/2010:

Moja kati ya kazi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ni kupokea mahesabu yaliyofungwa kutoka kila Taasisi ya Umma kwa kila mwaka. Ufungaji wa mahesabu hujumuisha pamoja na mambo mengine, hali ya ukusanyaji wa mapato sambamba na hali ya uchumi kwa mwaka uhaohusika. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya mwaka 2010, inaonesha hali ya ukuaji wa mapato yameongezeka kwa asilimia 17.7 kutoka mwaka 2009/2010 hadi mwaka 2010/2011, ukilinganisha na ukuaji wa mapato kwa mwaka uliotangulia.

Mhe. Naibu Spika, mapato ndio yanayotumika katika utekelezaji wa uendeshaji wa shughuli za serikali kadhalika ndio yanayotumika katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali za maendeleo nchini.

Mapitio ya Kamati yangu, kwa mnasaba na hoja mbali mbali zilizomo kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, yanaonyesha kuwa ukuaji huo wa mapato hauridhishi, kwa vile mapungufu kadhaa yaliyobainisha yanachangia sana ukusanyaji usioridhisha wa mapato. Kwa mnasaba wa hoja mbali mbali za Mdhibiti, Kamati imebaini yafuatayo:-

1. Kuna udhaifu katika Ukisiaji wa mapato katika taasisi zenye jukumu la kukusanya kodi na mapato mengineyo ya huduma

Mhe. Naibu Spika, taasisi nyingi zenye dhamana ya ukusanyaji wa mapato zinakabiliwa na uwezo ama vigezo vya ukadiriaji wa makusanyo katika taasisi zao,

ambapo msingi mkubwa unaotumika ni kuangalia hali ya mapato ya mwaka uliopita. Mhe. Naibu Spika, hicho ndicho kigezo kinachotumiwa na taasisi zetu.

2. Wingi wa wafanyakazi katika sekta ya umma wasiokuwa na kazi

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Umma inakabiliwa na changamoto kubwa ya wafanyakazi ambao licha ya kutokuwa na uwezo wa kazi zao wanazozifanya, lakini pia kutokuwa na kazi za kufanya katika sehemu zao za kazi. Kwa mfano, naomba kutoa mifano miwili tu kati ya mingi inayoikabili sekta ya umma.

1. Kamati yangu ilitembelea Shamba la Kilombero na kugundua gari moja la kulimia linaendeshwa na Madereva tisa. Walioajiriwa kama madereva wa kuendesha gari hilo walikuwa ni watatu na wengine sita walipewa mafunzo baada ya kuonekana kuwa hawana kazi ili wende wakaliendeshe trekta hilo.

2. Kamati yangu ilitembelea kiwanda cha upasuaji wa mbao kilichopo Wete na kugundua kuwa mashine moja chakavu ya upasuaji wa mbao inaendeshwa na wafanyakazi saba, ambao kwa mwezi kipato wanachoingiza serikalini ni elfu Sabiini na nne 74,000. Wakati wao kwa mwezi (chukulia kiwango cha chini cha mshahara 120,000/-) wanapokea kutoka serikalini jumla ya shilingi 840,000/-. Mhe. Naibu Spika, hiyo nataka nijenge picha namna gani tuna wingi wa wafanyakazi waliokuwa hawana tija serikalini. Leo nawapeni mifano miwili.

Mhe. Naibu Spika, suala la Uvujaji wa mapato ya serikali si suala geni katika mijadala na hoja nyingi zinazowasilishwa katika Baraza hili tukufu. Kwa mnasaba na matokeo ya ripoti ya Ukaguzi maeneo yafuatayo yamebainika.

1. Baadhi ya taasisi za umma zinazofanya biashara ya manunuzi na baadhi ya wafanyabiashara wasiolipa kodi serikalini. Hii ni hatari sana kwa sababu tunategemea mapato yale yale ya serikali yanayolipwa kwa wafanyabiashara yarudi tena serikalini kama kodi, lakini ni serikali wenyewe kwa upande mmoja nayo inachangia kupoteza mapato yake kwa makusudi.

2. Kuna tatizo la udhibiti wa risiti pamoja na matumizi holela ya risiti za malipo, wakiti mwengine hata malipo yanayofanywa serikalini. Serikali yenyewe hutumia risiti za vichochoroni.

3. Kuna uvujaji wa mapato ya huduma hasa upimaji wa viwanja. Mhe. Naibu Spika, nataka kueleza kwamba sasa hivi upimaji wa viwanja imekuwa ni dili

la watu binafsi katika Wizara ya Ardhi, ukitaka mifano ipo mingi rudieni katika ripoti mtagundua hilo.

4. Kuna udanganyifu katika ulipaji wa mapato ya *Income tax (with holding Tax)* ambayo hutozwa kwa asilimia 10% sambamba na kodi ya *VAT* ambayo hutozwa kwa asilimia 18%. Mapato yanayolipwa mara nyingi huwa hayaoneshi uhalisia katika malipo.

5. Hakujawa na utaratibu ama kuna uregevu wa ukusanyaji wa kodi kwa wajenzi wa majengo pamoja na biashara inayofanywa ya ukodishaji wa majengo kibiashara. Bahati mbaya na serikali sasa hivi nayo hukodi majengo kwa gharama kubwa bila ya hao waliokodishwa Mhe. Naibu Spika, sehemu ile ya kipato kurudi serikalini kama kodi. Katika eneo hilo serikali inapoteza fedha nyingi sana.

6. Taasisi za Umma (Hasa Vikosi vya SMZ) kufanyakazi za kuingiza mapato bila ya kuyatumia kwa ajili ya kuendeshea taasisi zao ama kurudi tena serikalini kama ni mchango wa serikali katika taasisi.

7. Mashirika kuendelea kutolipa Kodi Serikalini wakati mashirika hayo yana uwezo mkubwa mkubwa wa kulipa kodi serikalini.

8. Taasisi zinazojitegemea kuendelea kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

Mhe. Naibu Spika, haya ni baadhi ya mambao yaliyobaibnika kuchangia kwa kiasi kikubwa kasi inayoridhisha ya ukusanyaji wa mapato. Kamati yangu inaamini kuwa hali ya ukusanyaji wa mapato inaweza kuimarika na kufikia zaidi ya bilioni 30 kwa mwezi.

Mhe. Naibu Spika, utafiti uliofanywa ambao si rasmi kwa kamati yangu umebaini kuwa sasa hivi kwa mwezi serikali tukikaza buti tunaweza tukafika shilingi 30 bilioni na kupindukia katika mapato ya kila mwezi. Na hivyo badala ya kukusanya mapato ya shilingi 22 bilioni kwa sasa na hivyo kuiwezesha serikali kuweza:-

- Kutoa mishahara mizuri kwa watumishi wa Umma
- Kuweza kutekeleza utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo na huduma kwa jamii.
- Kuweza kupunguza kasi ya utegemezi. Kwa sababu tunapotegemea kunaathiri sana uhuru wetu Mhe. Naibu Spika, tulioupata kutokana na Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964.

Mhe. Naibu Spika, katika kufikia azma hiyo, Kamati yengu ina pendekeza mambo yafuatayo:-

1. Serikali haina budi kuanzisha mradi wenye lengo la kuimarisha mfumo wa ulipaji kodi serikalini.

2. Serikali haina budi kuimarisha miundombinu hasa ya kiuchumi kwa lengo la kuanzisha vyanzo vipya vya kodi ama kuvutia wawekezaji zaidi.

3. Serikali haina budi kuandaa mpango wa Udhibiti wa Utolewaji na matumizi ya risiti kupiga vita wafanyabiashara wasiolipa kodi sambamba na kuacha tabia ya kufanyabiashara serikali na wafanyabiashara wasiolipa kodi.

4. Serikali haina budi kuanzisha Sheria zitakazopelekea wajenzi wasio na Makampuni yaliosajiliwa na hivyo kulipia kodi serikalini. Zoezi hili halina budi kwenda sambamba na kuanzisha Kodi ya Biashara ya ukodishaji wa majengo.

5. Kuna haja kubwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kufanyia kazi Ukaguzi kwa malipo ya *VAT*.

6. Serikali haina budi kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za mapato kwa taasisi zinazofanya kazi za kutoa huduma ama ujenzi pamoja na kuhakikisha taasisi hizo zinalipa kodi serikalini.

7. Serikali hainabudi kuhakikisha utekelezaji wa agizo la ulipaji wa kodi kwa Mashirika.

8. Serikali hainabudi kuandaa mkakati wa kupunguza mgao wa ruzuku kwa kila mwaka kwa taasisi zinazojitegemea.

2. SURA YA MALIMBIKIZO YA MADENI

Mhe. Naibu Spika, Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2010/2011 inauonesha kuwa, kuna malimbikizo makubwa ya madeni yaliyofikia jumla ya shilingi 2,696,653,243 yatokanayo ama na malipo ya ununuzi wa huduma, manunuzi ya serikali ama malipo yatokanayo na kodi ya mali ya serikali. Madeni yanatokana ama serikali kudai au serikali kudaiwa.

Mhe. Naibu Spika, kuwepo kwa madeni (kwa Serikali kudai au kudaiwa) sio tu kunaathiri sana mapato ama bajeti ya taasisi husika, bali pia kunaathiri ufungaji wa mahesabu kwa taasisi pamoja na uthabiti (*stability*) hasa kwa taasisi za umma zinazojitegemea.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi kirefu, Kamati yangu imekuwa ikilifanyia kazi suala hili na hapa naomba niipongeze serikali kwa hatua ilizozichukua za kuyalipa takriban madeni yote yaliyokuwemo chini ya mwaka 2004 na kwa msimamo uliotolewa na serikali wa kuzitaka taasisi zote baada ya mwaka 2005, kwambaTaasisi zote zenye madeni zijilipie wenyewe kupitia bajeti zao, lakini bado suala la taasisi kulipa madeni kupitia bajeti zao limeonekana kuwa ni mzigo mkubwa unaoathiri sana bajeti ya taasisi husika. Kwa upande wa Taasisi za Umma kudai madeni yake, Kamati imebaini kuwa, kuna udhaifu mkubwa unaotokana na kutokuwa na umakini kwa Maofisa Wahasibu, udhaifu wa mikataba na wakati mwengine kutokutekelezwa kwa maamuzi ya Mahakama.

Mhe. Naibu Spika, bado hadi sasa tabia ya taasisi za umma kukopa na kukopesha katika huduma na manunuzi mengineyo inaendelea, hali inayoashiria kwamba serikali haiwezi kupiga mstari mwekundu kwa kumaliza kulipa na kudai madeni yaliyotangulia kabla. Kwa kuwa suala hili linaathiri sana mfumo wa bajeti na mahesabu, Kamati yangu inatoa mapendekezo yafuatayo:

1. Mchakato wa kufuta madeni ya muda mrefu na yasiyolipika, ulioanzishwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*P.A.C*) ambao umekwama katika Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, hadi sasa bado madeni hayo hayajawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi kupitia Mhe. Waziri, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo , ambapo kwa mujibu wa Kanuni ya 13 na 14 ya Kanuni za Fedha za mwaka 2005, madeni hayo(ambayo ni sawa na '*Loss'* kutokana na kutoweza kulipika tena) yanapaswa yawasilishwe katika Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kupata Azimio la kuyafuta.

2. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ifanye tathmini juu ya madeni yote yanayodaiwa kwa Taasisi za Umma, ili kubaini taasisi yenye uwezo wa kulipa kupitia bajeti za taasisi hizo na kwa zile zisizo na uwezo, ili madeni yasioweza kulipika kupitia Taasisi husika, yalipwe na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

3. Taasisi za Umma zenye kudai (hasa watu na taasisi binafsi), zipangiwe muda na utaratibu maalum kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, juu ya kudai malipo yatokanayo na madeni.

4. Serikali haina budi kufanya mapitio ya mikataba mbali mbali (hasa ya ukodishwaji wa nyumba za Serikali), ili kubaini mapungufu yanayoweza kuleta utata katika kudai au mali kurejeshwa katika milki ya serikali.

3. SURA YA UKIUKWAJI WA TARATIBU ZA MALIPO NA MANUNUZI:

Mhe. Naibu Spika, licha ya juhudi kubwa inayofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu pamoja na Kamati ya *P.A.C* ya kuhakikisha kwamba, taratibu za malipo na manunuzi ya Fedha za Umma zinafanywa kwa kuzingatia Sheria zilizopo, bado baadhi ya Taasisi za Umma zinaendelea kukabiliwa na tatizo la ukiukwaji wa taratibu za malipo na manunuzi.

Mhe. Naibu Spika, Ripoti ya Uchunguzi wa Hesabu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka 2010/2011 inaonesha kwamba, malipo mbali mbali yaliyofanywa kwa kukiuka utaratibu, yalifikia jumla ya shilingi 2,377,383,335. Uchunguzi wa Kamati utokanao na hoja ya hesabu hii, umeainishwa katika ripoti ambapo uchunguzi umebaini kwamba, tatizo hili pamoja na mambo mengine, limechangiwa sana na mambo yafuatayo:

1. Udhaifu wa Udhibiti wa Ukaguzi wa Ndani (*Internal Control System*) pamoja na uchache wa wakaguzi wa ndani.
2. Baadhi ya Maofisa Wahasibu *(Accounting Officers*) kutokuwa makini katika usimamizi wa fedha hasa katika malipo.
3. Upatikanaji wa fedha kwa wakati kutoka Hazina.
4. Kutokuwepo kwa Mpango wa Manunuzi (*Procurement Plan*) kwa taasisi nyingi za umma.
5. Elimu duni ya uhasibu kwa wahasibu wengi hasa katika naomba nisisitize kwa Serikali za Mitaa.
6. Kutokuwepo kwa Maofisa Manunuzi na kutokuwepo Maofisa Manunuzi wenye sifa.

Mhe. Naibu Spika, hayo ni baadhi ya mambo ambayo kwa kiasi kikubwa, mbali na baadhi ya Watendaji kukiuka taratibu kwa makusudi, yameonekana kuwa ndio yanayopelekea kukiukwa kwa taratibu za malipo na hivyo kupotea ama kuibiwa

kwa fedha za wavuja jasho wa nchi hii. Katika kukabiliana na hali hii, Kamati yangu inapendekeza mambo yafuatayo:

1. Kuimarishwa kwa Udhibiti na Ukaguzi wa Ndani kwa kuongeza ajira za wakaguzi wa ndani hadi kufikia kiwango cha kuwa na Mkaguzi wa Ndani kwa kila sehemu inayofanyiwa malipo. Aidha, katika kulipa nguvu suala hili, Kamati inapendekeza kuundwa kwa Idara kamili ya Ukaguzi wa Ndani.
2. Maofisa Wahasibu wanaoonekana kushindwa kusimamia majukumu ya Udhibiti wa Fedha za Umma, kamati inapenda wawajibishwe.
3. Taasisi zote za Umma zitekeleze matakwa ya Sheria kwa kuandaa Mpango wa Manunuzi kwa kila mwaka wa fedha kwa vile MPANGO WA MANUNUZI ndio msingi wa kuandaa Bajeti katika Taasisi husika.
4. Serikali kupitia Wizara husika na kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, iandae utaratibu wa kuwasomesha Wahasibu na Washika Fedha hasa katika Serikali za Mitaa.
5. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, na Wizara inayohusika, ichukue juhudi maalum ya kuwafunza na kuwaajiri Maofisa Manunuzi wenye sifa zinazohitajika.

TATIZO LA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU KUSHINDWA KUKAGUA HESABU YA *ACCOUNT* MAALUM YA VIKOSI (*CANTEEN ACCOUNTS)*:

Mhe. Naibu Spika, ripoti yetu inaonesha kuwa Mdhibiti kashindwa kukagua fedha katika '*Account'* ya '*Canteen'* na hivyo jumla ya Tsh. 610,507,490 zimeshindwa kukaguliwa katika Kikosi cha JKU. Hiyo ni kwa mujibu wa ripoti. ukiacha mbali na vikosi vyengine. Hivyo, Mdhibiti kashindwa kutoa maelezo juu ya usahihi wa matumizi yaliyofanywa kupitia fedha hizo.

Mhe. Naibu Spika, hicho ndicho kiwango kilichoainishwa na Mdhibiti, lakini tatizo la Vikosi vyetu kuitumia '*Account'* hii bila ya kuweka wazi mahesabu yake na bila ya kukaguliwa, sio tu kwamba, suala hili linatatiza maendeleo ya Udhibiti wa mapato ya Serikali, lakini pia linachochea kwa kiasi kikubwa matumizi mabaya ya fedha za Umma nchini. Tunapaswa tufahamu kuwa, hesabu hii ya *Canteen* inaingiza fedha kutokana na michango ya askari wenyewe, lakini pia huingiza fedha nyingi kutokana na mapato mbali mbali ya Vikosi, hasa fedha zotokanazo na huduma na kazi za ujenzi zinazofanywa na Vikosi vyetu kwa Taasisi nyingi za Serikali na watu binafsi.

Mhe. Naibu Spika, tunapaswa kufahamu kutokuonekana kwa fedha hizi katika bajeti ya Vikosi kama sehemu ya mapato na tukiangalia upande wa pili, namna vikosi vyetu vinavyokabiliwa na mzigo wa madeni ya fedha zilizoshindikana kulipwa hadi sasa. Kwa vile fedha hazikuainishwa katika Bajeti kama sehemu ya Mapato kwa Vikosi, naomba niwarejeshe katika bajeti za Taasisi mbali mbali (hasa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi) juu ya malipo yaliyofanywa katika miradi ya ujenzi kwa miaka tofauti.

5. TATIZO LA UFUNGAJI WA MAHESABU YA MWISHO WA MWAKA *(FINAL ACCOUNTS)*:

Mhe. Naibu Spika, ufungaji wa Mahesabu na Uwasilishaji wake kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ni sharti la kisheria kwa kila Taasisi ya Umma kwa mujibu wa kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2005. Aidha, hesabu hizo ziwasilishwe kwa Mdhibiti si zaidi ya tarehe 30 Septemba ya kila mwaka. Umuhimu wa taasisi kufunga hesabu mbali ya kuwawezesha wananchi kutupitia ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kufahamu hali ya rasilimali fedha na rasilimali nyenginezo katika taasisi husika, bali pia huiwezesha serikali kuweza kufahamu uwezo wake wa kifedha na kirasilimali katika serikali.

Mhe. Naibu Spika, Ripoti ya Ukaguzi wa Fedha ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka 2010/2011, imebaini kwamba, baadhi ya Taasisi za Umma hazifungi kabisa mahesabu. Aidha, baadhi ya taasisi hufunga mahesabu lakini huwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu nje ya muda uliowekwa kisheria.

Mhe. Naibu Spika, hali ya kusikitisha zaidi ni kwa baadhi ya Taasisi za Serikali na zaidi Mashirika ya Umma, kwamba hufunga hesabu lakini hawawasilishi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa hoja ya kuwaruhusu kwa mujibu wa Sheria zao (zinazoanzisha Mashirika hayo) kutafuta Mkaguzi wa Nje, asiwekuwa Mdhibiti huyu wa Serikali. Hali hii pamoja na kuruhusiwa na Sheria hiyo, inapingana na matakwa ya Katiba ya Zanzibar, kifungu cha 112(3)(c). Lakini kibaya zaidi, hesabu hizo huishia katika ngazi ya Bodi za Wakurugenzi tu, zinazosimamia Mashirika hayo, hata Barazani hazifiki na kama zinakuja, basi zinakuja kwa mlango wa nyuma, lakini hazitufikii sisi Wajumbe wa Baraza hili, ili tukazijadili na kuzifanyia kazi kwa mujibu wa utaratibu tulioweka.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano, Mfuko wa Barabara ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 2 ya mwaka 2011. Kwa mujibu wa kifungu cha 14(2) cha Sheria

hiyo, Bodi ya Mfuko ndio yenye majukumu ya kumteua Mkaguzi wa kuikagua taasisi hii, lakini pia kwa mujibu wa kifungu cha 14(7) kinamtaka Waziri anaesimamia masuala ya Fedha, kuiwasilisha Ripoti hiyo ya Ukaguzi katika Baraza hili tukufu. Cha kushangaza, haijawahi kutokea kwa Waziri wa Fedha kuwasilisha Barazani na haijawahi kutokea kwa Kamati ya *P.A.C* kuchunguza na kufuatilia juu ya Ripoti ya Mfuko wa Barabara tokea kuanzishwa kwake.

Uchunguzi wa Kamati kwa hoja hii imebainika mambo yafuatayo:

1. Baadhi ya Wahasibu kutokuwa na uwezo wa kufunga hesabu, unaweza ukawa mhasibu lakini huna uwezo wa kufunga hesabu.
2. Kutokuwepo kwa Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu kitu ambacho ni sehemu katika ufungaji wa hesabu.
3. Tofauti ya mwaka wa fedha katika ya wa fedha wa Serikali (July-June) na Baadhi ya Mshirika ambayo hesabu zao zinaanza kufungwa (January-December).
4. Kutokuwepo kwa Sheria zinazotoa fursa kwa baadhi ya taasisi hasa Mashirika kuwa na uwezo wa kuajiri Wakaguzi wa Nje wa kujitegemea na kuwasilisha taarifa zao za ukaguzi wa mahesabu kwa Bodi ama taasisi zinazosimamia taasisi hizo.

Katika kukabiliana na tatizo hilo la taasisi kutofunga hesabu ya mwaka, Kamati yangu inakuja na mapendekezo yafuatayo:

1. Kwa vile Zanzibar tunacho Chuo cha Uongozi wa Fedha ambacho mbali ya kuwa na wataalamu wenye uwezo katika ufungaji wa mahesabu na kwa kutumia gharama nafuu, lakini pia wanatoa mafunzo ya ufungaji wa hesabu kwa Taasisi za Umma. Kwa hivyo, tunapendekeza kwa taasisi husika wakitumie Chuo hicho kwa lengo la kufungiwa hesabu pamoja na watendaji kupata ulimu inayohitajika.

2. Kwa taasisi zinazoongozwa na Bodi na Mabaraza ya Madiwani, Kamati inapendekeza kuwa, mbali ya watendaji, Wajumbe wa Bodi na Waheshimiwa Madiwani wapewe mafunzo juu ya umuhimu wa ufungaji wa hesabu katika taasisi zao.

3. Kwa taasisi zote zilizokuwa hazikuwasilisha taarifa zao za ukaguzi pamoja na hesabu za mwaka kama zilivyoainishwa katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za mwaka 2009/2010 na 2010/2011 (pamoja na Mfuko wa Barabara ambao hauonekani katika ripoti za mdhibiti), taasisi hizo zinapaswa kuelewa kuwa, Katiba ya Zanzibar kifungu cha 112(3)(c)

kimempa uwezo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar, Mamlaka ya kukagua Taasisi zote, Mashirika na Taasisi zote za Umma Zanzibar na kuwasilisha ripoti zao katika Baraza la Wawakilishi kupitia kwa Rais, ili kuwawezesha Wawakilishi kwa niaba ya wananchi wafahamu hali na mwenendo wa taasisi hizo kifedha.

Hivyo basi, Kamati inaliomba Baraza la Wawakilishi liridhie kupitisha Azimio la kuziagiza Taasisi zote zilizokuwa hazikuwasilisha taarifa zao za ukaguzi na ufungaji wa mahesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ziwasilishe taarifa hizo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ili naye Mdhibiti afuate utaratibu wa kuziwasilisha katika Baraza la Wawakilishi, kabla ya tarehe 30 May 2013. Tunapendekeza kwamba taarifa hizo ziwe ni za miaka mitatu, yaani 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, Kwa ruhusa yako naomba nizitaje taasisi zilizoainishwa kwamba ama hazifungi na kuwasilisha hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi ama zinafunga lakini haziwasilishi tripoti zao za ukaguzi na hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkauguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, ili taarifa hizo hatimae zikawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:

1. Shirika la Meli na Uwakala.
2. Shirika la Utalii.
3. Shirika la Umeme.
4. Shirika la Maktaba.
5. Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*).
6. Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*).
7. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.
8. Shirika la Bima la Zanzibar.
9. Baraza la Manispaa.
10. Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*).
11. Mfuko wa Barabara.

RIPOTI YA UKAGUZI YAKINIFU KWA MIRADI YA MAENDELEO YA WANANCHI NA MIRADI YA TASAF:

Mhe. Naibu Spika, Ripoti za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu zilizohusu pia ukaguzi wa Miradi mbali mbali ya wananchi na ile iliyopata fedha kutoka Mfuko wa *TASAF*. Ukaguzi huu umefanywa kutokana na ukweli kwamba, fedha zilizotumika katika miradi ya wananchi zilitoka katika Bajeti ya Serikali,

fungu la Miradi midogo midogo, wakati fedha zitokanazo na Mfuko wa TASAF ni fedha zitokanazo na Mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa Tanzania.

Kwa uzito huo Mhe. Naibu Spika, baada ya uchunguzi wa Kamati yangu, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

1. Kiwango cha Fedha kilichotolewa na Wizara ya Fedha na Uchumi kwa miradi ya wananchi kilikuwa ni kidogo na kisicholingana na ukubwa wa miradi, hali iliyopelekea baadhi ya miradi kukwama.

2. Wizara ya Fedha iliyohusika na utoaji wa fedha haikuwa na utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo kwa lengo la kupata uhakika juu ya uwezo wa miradi hiyo inayotekelezwa kwa vile kama vile ilivyoombewa. Hali hii wakati mwengine ilipelekea kutolewa kwa fedha kwa miradi hewa na kwa kupitia kamati hewa za maendeleo.

3. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa ilitekelezwa kwa kiwango cha chini, hapa naomba niseme hasa miradi ya ujenzi.

4. Mashirikiano duni kati ya wananchi na kamati za maendeleo husika. Aidha miradi mingi hasa iliyohusu kilimo na ufugaji haikuendelea kwa kukosa utaalamu kutoka sekta husika.

5. Kutokuwepo kwa mpango mzuri wa uratibu kwa miradi ya wananchi na hata ile ya serikali kuu, hali iliyopelekea ujio wa mradi mmoja kupelekea kuharibu mradi mwengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa miradi ya *TASAF* ambayo ilikuwa na kiwango kikubwa cha fedha kati ya milioni 30 kwa mradi mmoja hadi kufikia milioni 120 kwa miradi minne ama mitatu iliyotekelezwa kwa pamoja, matokeo ya uchunguzi wa kamati ni kama inavyoonekana.

1. Matumizi ya fedha ya miradi hii hazingatia matakwa ya sheria ya fedha Nam. 12 Sheria ya Manunuzi na Sheria Nam. 9 zote za mwaka 2005 na hivyo kupelekea asilimia kubwa ya miradi hii, nasisitiza hasa ya ujenzi kutekelezwa chini ya kiwango kilichohitajika.

2. Hakukuwa na mashirikiano kati ya management ya *TASAF* na uongozi wa mikoa, wilaya pamoja na sekta husika katika mawizara, hali iliyopelekea

miradi mingi hasa ya kilimo, ufugaji na uvuvi kufa kwa kukosa utaalamu na uendelezaji mara tu baada ya miradi kukamilika kuingiziwa fedha, kwa ufupi haikuwa na uendelevu.

Baada ya uchunguzi huu hasa kwa vile pesa za miradi ya wananchi imehamashiwa sasa kwa mfuko wa jimbo (*CDF*) na kwa vile sasa tunaingia katika awamu mpya ya *TASAF* (*TASAF* 3), kamati inapendekeza:

Kwanza kutolewa kwa mafunzo maalum kwa kamati maalum za jimbo ama kwa makatibu wa kamati za maendeleo ya jimbo juu ya elimu ya utunzaji wa kumbukumbu, sheria ya fedha pamoja na sheria ya mununuzi.

Kwa upande wa miradi ya *TASAF* kamati inashauri mambo yafuatayo:-

1. Utekelezaji wa miradi utekelezwe kwa kuzingatia sheria ya fedha na sheria ya mununuzi.

2. Kwa vile fedha hizi ni mkopo kwa Tanzania ingekuwa ni vyema fungu la Zanzibar walau kufikia kile asilimia 4.5 kama kiwango kinachopatikana kwenye *GBS*. Mhe. Spika, inasikitisha utakuta wakati mwengine mkoa mmoja wa Tanzania Bara unapata zaidi kuliko Zanzibar kwa jumla yake.

3. Utekelezaji wa miradi hii pamoja na maendeleo ya wananchi ihusishe kikamilifu kwa lengo la kupata utalaamu na hivyo kuifanya miradi kuwe endelevu.

4. Kwa vile inaonekana kuwa hakuna uratibu (*co-ordination*) ya miradi ingekuwa ni vyema kuanzishwa dawati au kitengo cha uratibu wa miradi kwenye ofisi ya wilaya.

5. Kiwango cha asilimia 10 kinachotozwa kwa kila mradi kama ni gharama ya uendeshaji hakina budi kupitiwa upya ili kufanya miradi hii kuwa na ufanisi.

6. Pamoja na kwamba taratibu za *TASAF* kwamba wananchi ndio wenye mamlaka ya kuamua aina ya mradi unaohitajika, serikali ingeliona umuhimu wa kuelekeza fedha hizi kupitia kwa eneo moja ambalo utekelezaji wake ungesaidia kuleta faidia zaidi kwa wananchi pamoja na serikali.

Ripoti Sanifu kwa Miradi ya Maendeleo ya Serikali:

Mhe. Naibu Spika, kati ya ripoti tano zilizofanyiwa kazi na kamati yangu hii ni hii iliyohusu ukaguzi yakinifu kwa miradi ya maendeleo ya serikali ambapo ilihusu miradi.

1. Ujenzi wa jengo la Wizara ya Fedha Pemba ambayo ilisimamiwa na Wizara ya Fedha.

2. Mradi wa *ZUSP* ambao ulisimamiwa na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais.

3. Mradi wa kuelimisha elimu ya lazima ambao ulisimamiwa na Wizara ya Elimu.

4. Mradi wa kuendeleza kilimo na ufugaji na SSPL ambao ulisimamiwa na Wizara ya Kilimo.

5. Mradi wa maji safi na salama ambao ulisimamiwa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

6. Mradi wa uimarishaji wa barabara ambao ulisimamiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

7. Mradi wa kupunguza vifo vya akinamama na mtoto ambao ulisimamiwa na Wizara ya Afya.

8. Jengo la Kamisheni ya Utalii ambalo lilisimamiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, ukaguzi yakinifu kwa miradi ya maendeleo ni aina mpya kwani kwa kipindi chote kilichopita tulizoea kuona aina moja ya ukaguzi wa mahesabu kwa namna ya kuangalia uhalali wa malipo tu. Aina hii ya ukaguzi mbali ya changamoto zake zinazoikabili ina faida kubwa ya kuhakikisha matumizi bora na sahihi ya fedha ya matumizi yanayozingatia fedha inayotumika, ufanisi na tija kwa lengo lile lililokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, uchunguzi wa kamati kupitia miradi hiyo imebaini mambo yafuatayo:-

1. Baadhi ya miradi haikutekelezwa kwa viwango vinavyolingana na fedha iliyotumika.

2. Kuna ukwamaji wa baadhi ya miradi unaotokana na ukawiaji wa ulipaji wa fidia kama ni sehemu ya utekelezaji kwa upande wa serikali, hali inayopelekea hasara kwa serikali na wakati mwengine serikali kupigwa faini.

3. Kuna ukiukwaji wa mikataba lakini vile vile kuna udhaifu wa mikataba hali inayotoa fursa kwa serikali kushindwa mara kwa mara mbele ya vyombo vya sheria.

4. Kuna tatizo la kutekelezwa kwa amri ya Mahakama. Amri nyingi za Mahakama hazitekelezwi.

Mhe. Naibu Spika, msingi wa mkubwa wa kadhia hii unatokana na sababu ya ukiukwaji wa makusudi wa sheria ya fedha, sheria ya manunuzi na kanuni zao. Aidha uwezo wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kufanya ukaguzi yakinifu pamoja na uwezo wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali ya *PAC* ya kufuatilia hoja ya Mdhibiti ni moja kati ya changamoto zinazoendelea kukabili aina hii mpya ya ukaguzi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kubaini mapungufu haya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali inapendekeza mambo yafuatayo:-

1. Msisitizo usimamizi wa utekelezaji wa sheria ya fedha na manunuzi pamoja na kanuni zao katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha ni muhimu kufanya mapitio ya sheria hizo ili ziendane na wakati tulionao sasa.

2. Msisitizo wa utekelezaji wa maazimio ya Baraza la Wawakilishi juu ya uchunguzi wa kamati ya Baraza hili kwa jengo la Wizara ya Fedha Pemba.

3. Msisitiza kuhusishwa kikamilifu kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika uandaaji wa mikataba.

4. Msisitizo wa kuimarisha kwa Ofisi ya *CAG* katika kuajiri wataalamu wenye fani mbali mbali pamoja na maslahi bora kwa wakaguzi pamoja na mafunzo ya mara kwa mara kwa kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali na kuwapatia uwezo wa kukodi wataalamu pale ambapo inapohitajika.

5. Msisitizo wa serikali kujidhatiti katika kukamilisha utekelezaji wa sehemu yake katika mikataba kwa muda uliokubalika, kitendo cha serikali kutangulia kukiuka mikataba, naomba nirejee Mhe. Naibu Spika, kitendo cha serikali kutangulia kukiuka mikataba kinatoa fursa kwa upande wa pili kufanya watakavyo bila ya kuwa na hofu ya kuchukuliwa hatua na serikali.

Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa mali za Serikili 2009/2010:

Mhe. Naibu Spika, kati ya ripoti ya Mdhibiti ambazo zilifanyiwa kazi ni pamoja na ripoti yakinifu kwa mali za serikali ya mwaka 2009/2010. Ukaguzi juu ya eneo hili ulifanywa kutokana na ukweli kwamba asilimia kubwa ya bajeti ya serikali tunayoipitisha katika Baraza hili isiyopungua asilimia 60 inatumika katika manunuzi ya vifaa, huduma, vyombo vya usafiri pamoja na ujenzi ama ukarabati wa majengo ya serikali.

Kwa vile serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili hiyo, suala la kuwa na matumizi sahihi pamoja na utunzaji ni kitu cha msingi sana kwani itatuhakikishia kutokurudia kutumia fedha chache tulizonazo kwa ajili ama kurejea kununua ama kufanya matengenezo ndani ya kipindi cha muda mchache na hivyo itapelekea kuzielekeza fedha hizo katika matumizi ya shughuli nyengine za kimaendeleo ama shughuli za utoaji huduma.

Mhe. Naibu Spika, mbali ya suala la matumizi ya sahihi pamoja na utunzaji, jambo jengine la maana ni haja ya kuekwa kwa utaratibu mzuri unaokubalika wa uuzwaji wa vitu chakavu. Hili ni muhimu kwa vile fedha ya serikali aghlabu huwa ni ya mzunguko, yaani inakuwa *recycle* kwa maana ya serikali kutumia fedha kwa kununulia vifaa mbali mbali na baadae baada ya vifaa hivyo kuwa chakavu vifaa hivyo huuzwa na serikali kwa ajili ya kurejesha tena fedha hiyo kama ni sehemu ya mapato ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, hapa ndipo tunapoona umuhimu wa uwepo wa daftari la mali za serikali (*Assets register*) katika taasisi zote za serikali nchini kwa maana ya kuweka kumbukumbu ya mali pamoja na kujua thamani kwa madhumuni ya kufahamu kiwango cha uchakavu au thamani ya soko hasa kama vile majengo pamoja na viwanja. Kamati katika kulifanyia kazi suala hili ilibaini mambo yafuatayo:-

1. Mbali ya wizara tano zilizoanza kufanyiwa kazi na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuandaliwa buku la mali za serikali bado zoezi hili linakwenda kwa kasi ndogo sana katika hatua ya awali ya kuzitambua (*identification*).

Mhe. Naibu Spika, kazi ya kwanza ya kutayarisha buku ni kwa taasisi yenyewe kuanza kuzitambua mali zake katika wizara baadae ndio watu wengine watafanya kazi nyengine. Kwa hivyo kwanza tatizo hasa hatua ya awali ya kuzitambua na kuziweka thamani ya awali (*initial cost*), vile vile thamani ya kwanza ya kununulia ni kazi ya taasisi husika ya manunuzi ya wizara nyengine 11 zinakwenda katika hali ya kusuasua.

2. Mhe. Naibu Spika, hakuna sera inayoainisha mfumo wa ushukaji wa thamani ama upandaji wa thamani.

3. Taasisi nyingi za umma hazina mpango wa kiutawala na kibajeti uhusiano na utunzaji na matengenezo ya vyombo vya moto, zana pamoja na majengo, hali inayopelekea mali hizo kuchakaa ama kuharibika mara kwa mara na wakati mwengine kwa vyombo vya moto kupata ajali mara kwa mara.

4. Kutokuwepo kwa utaratibu mzuri katika uhifadhi mzuri wa mali katika stoo.

5. Kutokuwepo kwa utaratibu wa kukatiwa bima kwa vyombo vyote vya serikali hasa vyombo vya moto.

6. Licha ya kuwepo kwa utaratibu wa sheria ya kuuza mali chakavu baadhi ya maafisa wahasibu hawazingatii matakwa ya sheria na hivyo kupelekea kuitia serikali hasa. Hapa naomba nisisitize kwamba zoezi la uuzaji wa vyombo vya moto linatokana kwa taasisi kwanza husika, sio Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha ni kitu cha kupelekewa tu mwisho.

7. Ni tatizo la taasisi zinazohusika zinazopelekewa vyombo moto kutokupewa hati za umiliki kutoka ama kwa wahisani au kwa taasisi iliyohusika na kununua ambayo mara nyingi huwa ni Wizara ya Fedha.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa majengo mbali ya tatizo la kutokuwepo kwa mpango thabiti wa utunzaji, tatizo jengine lililobainika ni kwamba kwanza majengo mengi ya umma ya kutokuwa na hati miliki pamoja na hatimiliki ya ardhi.

8. Kutokufahamika kwa thamani kwa majengo mengi ya umma.

9. Majengo mengi yamekuwa mabovu na yamechoka sana, hali inayopelekea matengenezo kugharimu fedha zaidi kuliko hata kujenga jengo jipya.

10. Kutokufahamika kwa uhalali wa umiliki kati ya taasisi za umma, hali inayopelekea kutokujulikana taasisi yenye dhamana ya matengenezo.

11. Tatizo la kutolipwa kwa madeni yanatokanayo na kodi ama kulipwa kwa kodi isiyolingana na thamani ya soko.
12. Tatizo la uuzwaji holela wa majengo na viwanja vya serikali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya uchunguzi huu Kamati ya *PAC* sasa inaleta mapendekezo yafuatayo:-

1. Wizara ya Fedha kupitia Kampuni ya Ushauri ya *Property Market Consultant Limited* haina budi kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa daftari la mali katika Wizara nyengine zilizobaki. Aidha ni muhimu pia kwa wizara zilizokuwa hazijakamilisha wakaharakisha uimarishaji wa usajili wa mali zote ziliomo katika wizara zao pamoja na mambo muhimu yanayohitajika.

2. Kuna umuhimu kwa Wizara ya Fedha kuandaa sera ihusianayo na upandaji na ushukaji wa thamani.

3. Taasisi zote za umma hazina budi kuwa mpango maalum wa kiutawala na kibajeti kuhusiana na utunzaji na utengenezaji majengo. Aidha kamati inapendekeza kurejesha mpango wa kuyafanyia matengenezo ya vyombo vyote vya serikali katika Karakana za Serikali.

4. Kamati inapendekeza kuekewa bima vyombo vyote vya moto pamoja na udhibiti wa matumizi ya vyombo hivyo. Katika hili kamati inapendekeza kurejeshwa kwa utaratibu wa kutokuvitumia vyombo vya serikali baada ya muda wa saa sa kazi ila kwa viongozi maaluma waliokubalika na kwa dharura maaluma zilizokubalika. Vile vile kamati inapendekeza kutekelezwa kwa matakwa ya sheria kwa madereva wote kutumia buku la madereva (*log book*).

5. Tatizo la majengo, viwanja na maeneo ya miundombinu ya serikali kutokuwa na hati, serikali haina budi kuandaa utaratibu wa kufanya uthamini kupima maeneo husika pamoja na kutoa hati kwa majengo hayo au kwa ardhi hizo.

6. Tatizo la serikali kutumia fedha nyingi katika kuyafanyia matengenezo ya majengo, serikali haina budi kuzingatia umuhimu wa kujenga majengo mapya na ya kisasa.

7. Tatizo la baadhi ya majengo kutofahamika uhalali wa umiliki kati ya taasisi za serikali na watu binafsi pamoja na tatizo la kodi isiyolingana na bei ya soko, kamati inapendekeza kutolewa hadharani kwa ripoti ya Mhe. Waziri wa Maji na Nishati ya mwaka 2007. Aidha inapendekeza kuharakishwa kwa mchakato wa uundwaji kwa Shirika la Nyumba pamoja na fedha za kodi kutumika katika matengenezo ya majengo hayo.

8. Kuuzwa kwa mali zote zinazofikia kiwango cha uchakavu kwa utaratibu kwa kufuata taratibu zilizoekwa kwa mujibu wa sheria.

Hitimisho:

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuainisha na kupendekeza tena mambo mawili ya msingi ambayo yatasaidia sana kupunguza sana matatizo ya kuweka nidhamu nzuri ya matumizi ya fedha za umma na hivyo kuharakisha maendeleo ya uchumi nchini mwetu.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, inapendekeza kurekebisha kalenda ya vikao vya bajeti ya serikali katika Baraza. Mhe. Naibu Spika, kawaida bajeti ya serikali huanza mwezi wa Julai na kumaliza mwezi wa Juni, wakati kalenda ya vikao vya Baraza huanzia Juni na kumalizika mwishoni mwa mwezi Julai au mapema mwezi wa Agosti.

Kwa kipindi hiki cha mwezi Julai ambacho ni kipindi cha kuanza kwa bajeti mpya, wakati huo Baraza halijapitisha sheria ya matumizi na marekebisho ama ruhusa ya kukusanya (*Finance Bill* na *Appropriate Bill*) hali inayopelekea serikali wakati huo kufanya matumizi kwa njia ya Rais kuomba kibali maalum cha matumizi.
Mhe. Naibu Spika, tunahitaji kuliangalia suala hili kwa vile kamati imegundua kuwepo kwa matumizi holela kwa kipindi cha kumalizia na kuanzia kwa mwaka mpya wa fedha. Kamati inapendekeza serikali kulizingatia suala hili ili kalenda ya shughuli za bajeti kiwe kabla ya Juni na kumalizika kabla ya mwezi wa Julai.

Uwasilishaji wa sera za Serikali katika Baraza la Wawakilishi:

Mhe. Naibu Spika, msingi wa utekelezaji wa mipango mbali mbali ya serikali ni kuwepo kwa sera mbali mbali za serikali ambazo huwa ni muongozo wa

utekelezaji wa mipango hiyo. Mipango mingi inayofeli ya serikali huwa haitokani kwa kutokuwepo kwa wataalamu au ukosefu wa fedha pekee, bali aghalabu ni matokeo ya kuwa na sera mbovu, sera zisizofaa na sera zisizotekelezeka.

Hata hivyo suala la kutokuwepo kwa uwazi wa sera za serikali ni kitu cha maana sana ili kuepusha kulitia taifa hasara.

Mhe. Naibu Spika, katika hilo kamati yangu inapendekeza kurudiwa kwa mfumo utakaowezesha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa na fursa za kuweza kuzijadili, kuzichambua na hatimaye kuzipa baraka sera zote za serikali.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali kama zilivyo kamati nyengine za Baraza la Wawakilishi linapaswa kukaa na wadau wake kwa lengo la kufanikisha majukumu ya kamati. Vikao vya aina hii vina utaratibu na gharama zake, vitu ambavyo vipo nje ya mamlaka ya kamati.

Katika kufanikisha vyema majukumu ya kamati ninaiomba Ofisi ya Mhe. Spika kuwezesha ofisi kuwezesha ufanikishaji wa vikao vya wadau wa kamati hii angalau mara moja kwa mwaka ambao naomba niwatambue wadau wa kamati hii:

1. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
2. Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali
3. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
4. Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka
5. Vyombo vya Habari
6. Jeshi la Polisi
7. Kitengo cha Kuzuia na Kupambana na Rushwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, lawama zinachosha lakini shukurani hazichoshi. Naomba nimalizie kwa kurudia shukurani kwa niaba ya kamati kwa Mhe. Spika wa Baraza hili Mhe. Pandu Ameir Kificho na Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa namna mulivyotuwezesha hadi leo kamati yetu imeweza kuwasilisha ripoti yake mbele ya Baraza hili. Kwa niaba ya kamati tunawaambia ahsanteni sana na shukurani sana. (*Makof*).

Mhe. Naibu Spika, shukurani zangu za pili nazielekeza kwa Wajumbe wa kamati yangu, makatibu wa kamati, wenyeviti wenzangu wa Kamati za Kudumu pamoja na wajumbe wote ambao kwa umakini wao wamekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha kazi ya kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, shukurani maalum zinapeleka kwa Waheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yussuf Mzee (Alhajj mtarajiwa) kwa uwezo na juhudi yake ya kuisimamia Wizara ya Fedha na hivyo tukaanza kuona mwanga wa mipango mizuri ya ukuzaji uchumi katika nchi yetu.

Aidha ningependa vile vile niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri waliofika mbele ya kamati yangu na kushuhudia namna ya Makatibu wao Wakuu na watendaji wao wa kada ya fedha walivyokuwa wakijibu hoja mbali mbali za kamati.

Naomba niwatambue Waheshimiwa hao:-

1. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ingawa leo ripoti yake hakuweza kuja hapa kueleza ripoti ya utekelezaji.
2. Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ingawa na yeye hakuwepo kueleza utekelezaji wake.
3. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.
4. Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.
5. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.
6. Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi.
7. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili.
8. Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.
9. Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Mhe. Naibu Spika, shukurani zangu naomba pia nizielekeze kwa Makatibu Wakuu, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Mameneja na Wakurugenzi Watendaji wa Mashirika, Maafisa Wadhamin, Makamanda wa Vikosi vya SMZ, Waheshimiwa Madiwani, Wahasibu na watendaji wote wa kada ya fedha pamoja na Masheha.
Mhe. Naibu Spika, pamoja na shukurani zangu kwa Makatibu Wakuu tofauti wa wizara, kamati yangu ina masikitiko makubwa kwa baadhi ya Makatibu Wakuu walioona kwamba shughuli zao ni muhimu zaidi kuliko shughuli za kamati.

Mhe. Naibu Spika, mwisho naomba nizielekeze shukurani zangu za kamati kwa vyombo vya habari kwa kazi nzuri wanaendelea kuifanya ya kuwapasha wananchi habari muhimu ya matumizi ya fedha zitokanazo na kodi zao. Sisi katika kamati tunatambua na tunathamini sana mchango wa vyombo vya habari katika kujenga jamii iliyozindukana na yenye uelewa wa kudai haki inayoporwa na wachache. Vyombo vya habari tunaomba mutusaidie sana katika hili.

Mhe. Naibu Spika, ni matumaini ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali na Mashirika kwamba mapendekezo yaliomo katika ripoti kuu ya kamati na yaliomo kwenye mawasilisho haya ya mwenyekiti ambayo ni ufupisho wa ripoti kuu, na ambayo itakuwa ni sehemu ya ripoti kwamba yatatekelezwa kwa ukamilifu na baadae serikali itakuja na majibu sahihi juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya kamati ambayo muda mchache ujao huenda yakawa ni mapendekezo na maagizo ya Baraza la Wawakilishi.

Ninamalizia kwa kukushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na kunivumilia. Ninashukuru sana Wajumbe wenzangu kwa utulivu na umakini wenu wakati ninawasilisha ripoti. Hata hivyo naomba Mhe. Naibu Spika, uniruhusu nifunge ripoti yangu hii kwa maneno ya Jaji maarufu nchini Uingereza, ni Jaji Maarufu sana huyu aliposema, *I may be wrong but I am always clear*.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza naomba tufahamiane. Kwanza tunamshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati ya *PAC* kwa hotuba yake nzuri ambayo imeeleza dhamira nzima wanayofanya kamati yake. Lakini pia niwashukuru na Mawaziri wote waliowasilisha taarifa zao kabla ya yeye kwamba zote tumezielewa, wale wenye *quiries* zilijibiwa zimejulikana na zilizokuwa bado pia zimejulikana.

Sasa nina tangazo moja Mwenyekiti wa UWAWAZA amesema kwamba leo mafunzo ya Wawakilishi Wanawake yatakuwepo kama kawaida, na baada ya hayo tumeshauriana hapa kwamba tuna maziko ya mzee wetu ambaye amelitangaza taifa letu duniani nzima, kwa hivyo tunaombwa tushirikiane na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utali na Michezo kwenda kumzika saa saba.
Kwa maana hiyo ninaahirisha kikao cheti hiki hadi saa kumi na moja jioni ili tukashiriki maziko hayo.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tuna majina ya Waheshimiwa 6 wachangie wasirejee, waende kwenye *point*. Nia yetu ni kwamba majadiliano leo

kwa Kamati hizi zote tumalize, ili kesho tumalize kamati iliyobakia. Kwa hivyo, mchangiaji wa mwanzo namuita Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadae ajiandae Mhe. Hija Hassan Hija. Dakika 20.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana, zinanitosha. Mhe. Naibu Spika, kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii ya *PAC* pamoja na Wajumbe wenzake katika hotuba yao iliyokuwa nzuri yenye muelekeo, lakini utendaji tu unakosekana katika taarifa yao. Kwa sababu wanapotoa maelekezo basi utendaji wake unakuwa ni mzito sana. Sasa kwa hilo niwape pole kwanza kuwa lengo lao utekelezaji uwe madhubuti.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitachangia kwa jumla. Lakini kwanza katika kitabu hiki cha PAC, kwa mtazamo wangu kwa kweli hamna hata Waziri mmoja aliyeonesha kujibu zile hoja walizotoa Kamati hizi. Kwa kweli hili ni suala ambalo Mhe. Naibu Spika, linasikitisha sana, hata na sisi wachangiaji tunapata shida. Kuna kabrasha hili lililopita, majibu ni yale yale ya nyuma na mwaka huu ni yale yale yanajieleza.

Mhe. Naibu Spika, sasa tunafika pahala Baraza letu linaanza kushuka hadhi yake na wakati huo ilikuwa Baraza tumepanda chati, hata wananchi nje walikuwa wanapenda kutusikiliza jinsi gani ambavyo *backbenchers* inavyotoa malalamiko yake kwa serikali na kuweza kupata hoja ambazo wanazozipeleka Kamati na kuweza kujibiwa. Kwa kweli ni jambo linalosikitisha sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia leo utajua kama kweli Baraza linashuka hadhi. Siku hizi za kamati, tuna mawaziri 6 tu na wakati tuna mawaziri 16. Hili ni jambo la kusikitisha kweli, hiki sio kitu cha mchezo Mhe. Naibu Spika. Ni fedha za wavuja jasho, wanyonge ambazo sasa tunakwenda kuzitumia pahala ambapo ni pabaya sana. Mhe. Naibu Spika, inatilisha huruma.

Mhe. Naibu Spika, siku moja mimi nilisema, *PAC* ni lazima wapewe askari watie watu pingu. Kila unapokwenda katika mawizara, kuna baadhi ya wizara utakuta mapungufu yamo na fedha watu wamezila. Mwenyekiti, unangoja nini usitie watu pingu, Mwenyekiti unanitia wasi wasi, kwa sababu ni lazima unatakiwa uwe shujaa, ni lazima utembee na pingu, watu wezi. Wenzetu Uganda wanakua na pingu na *peace* ndani yake. Polisi wanakuwa nao chini ya ubavu, kama Uganda na Kenya. Hata hapa siku moja nilimsikia yule Mwenyekiti wa *TLP*, alitaka polisi mara moja waje. Mhe. Naibu Spika, tungefanya hivyo heshima ingekuwepo.

Mhe. Naibu Spika, watu wanafanya kazi hii ni kwa muda mchache tu wanakuwa na majumba ya ghorofa, sisi huku watu mishahara wanalia hakuna fedha. Hebu

Mhe. Naibu Spika, sasa tutageuka badala ya wale wezi wa ardhi, sasa tutakwenda kwa ujumla wao. Tunawajua wala hatuwaogopi, fedha zinaliwa vibaya sana na ndio maana tunasema mishahara kidogo. Fedha hizo *PAC* wameshatukusanyia mabilioni ya fedha zimo humu, kwa nini hatuwakamati, tunaogopa nini. Leo wananchi wanapiga kelele huko mishahara kidogo na kweli. Maana yake ukiangalia leo askari wetu wanapata mishahara midogo kabisa. Mtu koplo hata shilingi 200, 000/- hafiki, anapata pesa kidogo sana.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba sana tusifanye mchezo, kwa sababu hii Kamati ni kubwa sana, japo tumepewa siku chache tu. Maana yake leo msahafu huu tutaujadili saa ngapi na siku zetu ni chache tu, hii ni kamati kubwa sana na ndio roho ya nchi Kamati hii na tunaifanyia mzaha kama hivi. Mwenyekiti na Kamati yake watajisikiaje, watu wenye akili, wenye maarifa, watu waliosoma na wamekwenda ndani zaidi kwa masuala haya na hatimaye katika utendaji wame-*fail*, Mheshimiwa inasikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, kodi za *laundries* kasema Mwenyekiti wangu hazilipwi. Kama zinalipwa ushahidi hauoneshi, wapo watu hawalipi makodi na wanajulikana, lakini pingu hazichezi sijui tunaogopa nini. Siku moja Mhe. Hija Hassan alipokuwa akisema habari ya walioiba umeme, watu wengine wakamletea ujumbe wa kuwa watamuua, hapana tusiogope katika kutetea haki kuuliwa, kufa utakufa tu, hakuna binadamu hata mmoja mwenye ahadi na Mwenyezi Mungu hapa, anayemwambia kuwa wewe utaendelea katika maisha yako, hakuna hata mmoja hapa, utakufa tu wewe binadamu, ukiuliwa ndio minalfaidhina kabisa, keshakupunguzia mengi anakusafishia njia, ndio na yeye atakufa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hili suala linasikitisha sana. Mikataba inafungwa mibovu, haistahiki kabisa kufungwa, inakiuka sheria, makandarasi wanapewa kazi ambazo sio *field* zao na ni moja katika ubadhirifu, ilimradi fedha za miradi ziliwe. Wameonesha humu kuna fedha za miradi za wananchi kwenye shehia, hatimaye wale wahusika Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na wenye vitengo vyao hawaendi kuwaelimisha na hawawafuatilii zile fedha.

Leo tunarudi pale pale kwenye umaskini, *PAC* imeonesha, tena wamekwenda vizuri sana katika buku lao. Nisisahau kusema kwamba Mwenyekiti hii ripoti yako, sifikirii kama katengenezewa na Katibu, wameshauriana na Katibu, lakini Mwenyekiti katoa mwenyewe kwenye akili. Nimpongeze sana sifa hiyo aliyokuwa nayo, hapotezi hata siku moja dira. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hizi kamati lazima tuzipe kipaumbele, na ndio leo tunakuja kueleza hapa jinsi tulivyofanya ule mzunguko.

Mhe. Naibu Spika, tukienda kwenye kilimo ndio hayo tunakuja manyago yenyewe muna mapungufu humu wametuonesha vile vile. Kuna wengine wanashindwa hata na madaftari, basi daftari Mhe. Naibu Spika, kama sio udanganyifu ni kitu gani. Linashindwa kununuliwa daftari kwa ajili ya kuweka mipangilio mizuri ya bidhaa ambazo zilizokuwemo na zilizokuwa hamna. Kwa hivyo, haya mambo yanatuumiza na yanaendelea kutuumiza.

Mhe. Naibu Spika, wahusika tunao hapa wanasheria wetu, kwa nini tusiibadilishe kanuni. Ni jinsi gani ya kuweza kuibadilisha kanuni, *PAC* waende na askari wawe na pingu zao mkononi. Wanapogundua tu manyago pale pale hakuna kumwachia mtu pumzi, mpeleke ndani tu tuone kama nchi yetu haikupata tija hapa.

Lakini wakisha wanakuja kutuletea ripoti humu serikali inalala. Tunasema tumechoka sisi wananchi wetu kulalamika. Wananchi wanatulalamikia sisi Wawakilishi na sisi tunailalamikia serikali. Jamani watu wa serikali tunawaombeni sana tubadilike, kubadilika kwetu jamani tuzienzi hizi fedha ili angalau tuweze kuwasaidia watu kwenye mishahara yao, ili tuweze kununua dawa serikalini kupeleka hospitali, tunakuwa hatuna fedha. Madawa mahospitali hatuna, baadhi ya zana nzito hatuna, hata mabomba hatuna hospitalini tuseme ukweli.

Mhe. Naibu Spika, leo hii nimeshanunua mabomba matano nimekwenda kupeleka. Tunashindwa angalau kuwapa watu motisha katika kazi zao, kama ilivyosemwa juzi kutokana na fedha hatuna.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo mengine ambayo yameelezwa, hasa katika Kamisheni ya Utalii, hebu haya mambo ambayo yanaelezwa humu tunaomba sana katika bajeti inayokuja, tusiyaone tena haya mapungufu, hebu tuwaheshimu hawa wenzetu, kila siku tutakuwa tunapigishana kelele tu humu. Mhe. Naibu Spika, mimi naomba kwamba kila aliyeguswa. Mfano Hoteli ya Bwawani udanganyifu mtupu katika upimaji, haijulikani.

Hiyo ramani yenyewe haitambulikani, basi hata ile tunashindwa kufanya tuna lengo gani, pengine zimetoka fedha kwa kufanya mambo yale, lakini watu wamezila, halafu tunyamaze, haiwezekani. Mheshimiwa hawa waliohusika na kula fedha hizi tia pingu, hakuna kumwacha mtu, tuwe *serious* bwana, tumechoka. Wananchi wetu wanatulalamikia na kusikitika sana kuwa hawaoni maendeleo. Maendeleo yenyewe kumbe watu binafsi wanakula wanaondoka, watu wanafanya kazi kwa muda wa wiki moja au wiki mbili siku mbili tatu ana jumba la ghorofa, watu wa chini wanakufa maskini.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende kwenye suala la vikosi, nitauliza kidogo. Kuna watu siku hizi tumesema watapata fedha kwa ajili ya viti vyao, vikosi vya SMZ wanapata mafunzo na mwengine wanapata daraja ya vyeti, lakini ulipaji wake mimi unanishangaza, wengine wanalipwa shilingi 12,500/- sijui ndio niite vipi hiyo, kapata cheti nashindwa niite vipi.

Wengine wanapata shilingi 28,500/- ana cheti huyo, sijui akipata *diploma* atapata ngapi na wengine wana shilingi 15,500/-. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, hebu tuelezwe ndio upandishwaji wa askari mishahara katika viwango vya kusoma, au basi tu, pengine kuna pesa zao zaidi huko wanaliwa. Inawezekana Mhe. Naibu Spika, kuna fedha hapa ziko zaidi kuliko hizo, inasikitisha sana kusema kweli.

Mhe. Naibu Spika, naona kama unatizama saa. Hilo ni suala la kusikitisha sana, naomba sana Mhe. Waziri kama hulijui ulijue na ulifanyie kazi kwenye bajeti ikija naomba sana mtupe jibu ambalo limekamilika.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hatutaki tena mzaha, tumechoka Waheshimiwa kila siku kutafuta mambo tukaleta hapa, halafu tukachezewa tu. Hali hii sasa imekwisha. Tutatafuta kanuni za aina yoyote Waziri yeyote tutamwambia pale jiuzulu, tutamwambia hivi hivi, imekwisha kweli. Mawaziri jiuzuluni ondokeni *backbenchers* ifanye kazi, ndio, tuna uchungu sana Mhe. Naibu Spika, tumechoka. Kwa nini tumechoka, kwa sababu wananchi wetu wanatupigia kelele ndio wanaoumia kuliko sisi.

Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio hali ambayo tunaiona kuwa leo tuna mawaziri 16, lakini tunawaona mawaziri wachache ni siku ambayo ni kubwa sana ya kupitisha ripoti ya kuonesha ni jinsi gani utekelezaji. Mwenyekiti kawataja hao mawaziri wengine hawajatoa ripoti zao, wameingia mitini wame-*disappear* kwa nini tusiwaseme. Mhe. Naibu Spika, kwa nini tusiseme. Hili Baraza lako ni kubwa tena ni tukufu, linajulikana katika dunia nzima, isifike tukaharibiwa sifa zetu, mimi naomba sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia twende kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Kusema kweli Mheshimiwa bado kuna madudu mengi katika wizara hii. Maneno ya Mzee Juma bado kuna madudu mengi sana. Tunaomba sana Mhe. Waziri kama tulivyosema sasa hivi *PAC* itakuja na pingu, hakuna mchezo sasa hivi *PAC* lazima itakwenda na askari na pingu ndani yake ndipo tutakapokwenda sawa.

Ndio, hii ni nchi ya Mapinduzi ni lazima twende hivyo hivyo, hakuna kumtizama mtu sasa hivi, kweli nakuambia hii ni nchi ya Mapinduzi bwana hakuna mzaha na tutafika huko, tukienda hivi tutafika huko. Wananchi wetu wataondokana na umaskini fedha zao sasa tunaziokoa na kuzirudisha serikalini, hiyo kazi itafanywa chini ya dhamana ya *PAC*, chini ya jemadari mwenyewe Mwenyekiti wa *PAC* akiongozwa na Wajumbe wake, sio yeye peke yake, pamoja na Wajumbe wake wote wanafanya kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, namalizia niwaunge mkono *PAC* kwa mambo waliyotuletea, lakini ndani yake tuna majonzi kuwa hadidu rejea ni zile zile tu hazina utekelezaji. Naamini Mhe. Naibu Spika, hapa itakuwa kikomo. Ahsante sana naunga mkono Kamati hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima mpaka sote leo tumeweza kumzika msanii maarufu wa Zanzibar, Marehemu Mama Fatma Bi Kidude na namuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pema.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba ametumia dakika 17 na bila shaka hizo tatu amenigaia mimi, kwa hivyo nitatumia 23 kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nataka niipongeze Kamati ya *PAC* chini ya Dr. Omar Ali Shehe na timu yake yote, Makamo Mwenyekiti, Wajumbe na Makatibu wake wawili. Pia niipongeze Ofisi ya *CAG* kwa kuwapatia ripoti ile na wakaweza kufanya kazi. Lakini sambamba na hilo Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa jinsi alivyosimamia na kuleta majibu, maana yake kwa tathmini yangu majibu ya serikali ameleta peke yake. Tupo hapa hapa ndani ya Baraza Mawaziri wanauliza nijibu nini kama kwamba walikuwa wako katika ardhi ya saba.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Kiwani nimpongeze sana Waziri wa Fedha kwa kuliokoa jahazi na huo ndio uwaziri hasa.

Mhe. Naibu Spika, mtakumbuka tarehe 12 Novemba, 2010 baada ya kuchaguliwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohamed Shein alikuja humu akazindua Baraza la mwanzo katika hii Serikali ya Awamu ya Saba. Naomba uniruhusu Mhe. Naibu Spika, ninukuu maeneo manne muhimu aliyosema Mhe. Rais. Mhe. Naibu Spika, eneo la mwanzo ukurasa wa 4 Mhe. Rais alisema,

> “Mhe. Spika, tunaianza Awamu hii ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tukiwa tumebeba dhima na matumaini makubwa ya Wazanzibari”. Hiyo ni sehemu ya kwanza Rais aliyotukumbusha kwamba Baraza hili linaanza tukiwa tumebeba dhima na matumaini ya Wazanzibari wote.
>
> Lakini ukurasa wa 6 Mhe. Rais akasema tena maneno matamu, alisema kwamba;
>
> > “Tumeingia katika Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na hii ina maana itakuwa ni serikali yenye kujali maslahi ya wananchi wote na matakwa yao”.

Ukurasa wa 8 alitwambia ni dhima, ukurasa wa 6 alisema,

> “Serikali hii itajali matakwa ya wananchi na matarajio yao”.

Ukurasa wa 20 Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais akatukumbusha tena, akasema kwamba,

> “Vile vile nitaimarisha maana yake yeye mwenyewe, nitaimarisha uwazi na uwajibikaji nataka nirudie tena, na kulifanya suala la uwajibikaji kuwa ni ajenda ya kitaifa”.

Maneno ya Mhe. Rais ukurasa wa 20, alisisitiza kwamba ajenda ya uwajibikaji ndio ajenda ya kitaifa.

Mhe. Rais hakuchoka hapo, ukurasa wa 22 akasema tena kwamba, “watendaji wote wa serikali wa ngazi mbali mbali wataendelea kutimiza wajibu wao kwa ufanisi, tija na matakwa na kwa nidhamu ya hali ya juu, kwa wale watakaoteuliwa kushika dhamana mbali mbali wakiwemo mawaziri, makatibu wakuu na wengine. Napenda niwatanabahishe kuwa wanachopewa wao ni dhamana, na ni dhamana ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar|.

Mhe. Naibu Spika, Rais aliowateua amewapa dhamana hakuwapa nyumba, fedha wala maji, aliwapa dhamana ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa maslahi yetu. Mhe. Naibu Spika, hayo ni maneno ya Rais aliyasema humu sote mashahidi, leo nakumbusha kwa niaba yetu sote Wawakilishi pamoja na wananchi wa Zanzibar.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nataka nitoe nukuu mbili za watu wa kawaida, nukuu ya mwanzo falsafa ya mwanzo Mhe. Marehemu Thobias Makungila wa Fuoni, alikuwa Mwakilishi miaka mitano iliyopita, alikaa miaka yote mitano

hakuzungumza hata siku moja. Mimi na Mhe. Omar Ali Shehe tukamuuliza kwa nini huzungumzi Mhe. Thobias? Akasema kwamba, hajawahipo kusikia kwamba kuna mtu amefungwa kwa sababu hazungumzi. Akasema kusema ni hasara, na kwa hivyo bora anyamaze aje atie saini apate maposho. Hiyo ni falsafa ya Mhe Thobias marehemu kutoka Fuoni.

Sasa hivi karibuni nilipata falsafa nyengine ya mtu wa Kiwani anaitwa Fundi Ndevu, aliniuliza mbele ya Mhe. Omar Ali Shehe kwamba nyinyi Wawakilishi kule wangapi mmekwenda Makka? Nikamwambia nadhani hawatimii watu 20 Baraza la Wawakilishi, kwa nini? Nikwamwambia sina hakika, akasema hamna uwezo maana uwezo wa Makka si pesa uwezo wa Makka ni taqwa na imani. Kwa hivyo, akanambia inaelekea taqwa hamna wala imani ndio maana msiende Makka sio pesa, pesa tunazo. Kwa hivyo, nakunasihini madhali Makka hamuwezi kwenda semeni jambo moja tu, semeni ukweli kwa maslahi ya watu, hii ni sadaka yenu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, falsafa hizi mbili ya Thobias na Fundi Ndevu, mimi nachukua hii ya Fundi Ndevu niseme ukweli kwa maslahi ya watu. Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi wangu huo sasa niseme yafuatayo. Wafanyakazi ambao ni wengi, ripoti hii imetuonesha mtambo mmoja wa mashine chakavu ina watu zaidi ya saba. Trekta moja lina madereva 9 hii ndio serikali yetu ilivyo. Kama *PAC* ingepewa uwezo wa kuchambua, basi nina hakika ingekuta cherehani moja ina mafundi 40. Ndivyo tulivyo na ukisema watu wanakasirika, lakini ndivyo tulivyo. Kwa falsafa ile ya Fundi Ndevu mimi nasema kwamba tuseme ukweli kwa maslahi ya watu.

Sasa Mhe. Waziri wa Fedha hii serikali yako ndivyo ilivyo. Una *bill* kubwa sana ya mishahara lakini huna wafanyakazi, na ndio maana kila ofisi ukichungulia, utakuta mavumbi na mabuibui tele kwa sababu huna wafanyakazi. Una watu wanasubiri mshahara mwisho wa mwezi na kiinua mgongo watu wakifika miaka 60. Kwa hivyo, tuangalie ikiwa wewe kazi yako ni kutafuta fedha utulipe sisi tunaofanya kazi hiyo tuendelee.

Mhe. Naibu Spika, jengine mapato yanakuja, ripoti imeeleza. Suala hili tulilisema zamani na ninaamini Waziri wa fedha suala hili ana nia safi ya kulisaidia, lakini waziri wa fedha peke yake atafanya nini, mwisho wa siku ataambiwa yeye ni adui, huo ni ukweli.

Lakini ninachomuomba Mhe. Waziri wa Fedha afahamu kwamba kazi moja ya Waziri wa fedha ni kutafuta vyanzo vya fedha. Mimi namshauri sana kaka yangu waziri wa fedha na ninamuamini sana. Kama anataka kuimarisha mapato ya

serikali basi aanzishe *Central Database for Revenue Collection*, ili mapato yote ya nchi yakusanywe katika mtandao mmoja, hii kuwaachia madaraka *ZRB*, Manispaa na Ardhi ni wizi tu.

Kwa hivyo, andaa mtandao mmoja ili mapato yote yakusanywe hapo, uangalie kwa mwaka mmoja kama hutoona mapato yake yamepanda maradufu. Najua hilo ni gumu huliwezi kwa sababu, unaweza kulianzisha hilo wenzako wakakupiga vita. Kwa sababu nilisema juzi hapa kila kitu ni dili. Hapa ukicheka dili, ukilia dili, ukiumwa dili kila kitu dili. Kwa hivyo, najua una nia safi ya kufanya hivyo, lakini nina wasi wasi kama utaweza kwa sababu mtandao umedhibitiwa na mipango ya dili.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni madeni ya serikali. Mimi naomba Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hebu atuambie hasa Zanzibar tuna deni kiasi gani. Mimi nina wasi wasi itafika siku Wazanzibari wote watauzwa, itakuwa madeni yamezidi inabidi kila mtu na familia yake wauzwe ili tulipie madeni ya watu, maana yake kinachofanyika hapa ni watu kukopa tu, lakini hakuna *value for money* ya miradi yetu.

Wasi wasi kama Mhe. Hija Hassan, kuna siku ukiwa umeshakufa Mhe. Waziri wa Fedha basi utatuachia deni kubwa itabidi familia zetu zilipe na hatuna uwezo maana ardhi yote imechukuliwa na wakubwa. Ndio, imebakia bahari tu, bahari ndio hatuwezi kuichukua. Lakini nina wasi wasi kwamba itafika siku Waziri wa fedha utashindwa kulipa madeni ya taifa, kwa sababu hatuna nyenzo wala mtaji. Kwa hivyo, utuambie basi deni la taifa ni shilingi ngapi na vipi tutalilipa hilo deni, kwa sababu tumejenga juzi uwanja wa ndege na tumekopa zaidi ya dola milioni 8, uwanja wa ndege tayari *terminal* imefeli. Keshokutwa mnakwenda tena kukopa, hayo ni madeni ya taifa kwa ajili ya wanyonge.

Mhe. Naibu Spika, pia nimshauri Waziri wa Fedha kuna deni la milioni 98.7 ni kwa Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa ajili ya fidia ya wafanyakazi wa serikali wanaopata madhara kazini, hili deni hawaliwezi wizara ya ustawi nakuomba ulichukue na uweze kulilipa haraka. Wafanyakazi wetu katika taasisi mbali mbali wanapata madhara na deni hili halilipiki kwa upande wa wizara ya ustawi, bajeti yao ni ndogo. Kwa hivyo nakuomba Mhe. Waziri wa Fedha ulichukue deni hili na ulifanyie kazi haraka iwezekanavyo kwa busara zako.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda haraka zimebaki dakika zangu mbili nimalize. Masuala ya kufunga hesabu. Ripoti imesema kwamba wizara nyeti zimeshindwa

kufunga hesabu. Lakini jamani niwakumbushe fungeni hesabu vizuri mpunguze ushamba. Watu wanazungumzia *PBZ* hata habari hawana, maana yake *PBZ* kutofunga hesabu ni jambo la kawaida, watu wanaona ni jambo dogo.

Kwa hivyo, hili halifanywi kwa sababu hatuna uwezo wa kielimu au kwa sababu hatuna nyenzo, kwa sababu ni sehemu ya mafao ya watu, maana yake ukifunga hesabu *CAG* atakagua, akikagua atampa Omar Ali Shehe ayafanyie kazi. Watu wanajitia kusahau kwa sababu ni sehemu ya mafao ya watu. Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, nakuomba sana ulisimamie suala hili, hii ndio *CV* yako katika maslahi ya nchi yetu.

Leo mfuko wa barabara hakuna hesabu iliyofungwa. Katika sehemu ambayo fedha inatumika nyingi katika nchi hii ni kwenye mfuko wa barabara. Siamini kwamba kule hakuna wataalamu, kama *PAC* walivyosema ni kwa sababu watu wanafumba macho kwa ajili ya maslahi yao.

Mhe. Naibu Spika, ukaguzi yakinifu. Mimi hapa napingana sana na ripoti ya kamati, kwamba eti kuna maeneo wameshindwa kufanya ukaguzi yakinifu, kwa hivyo kamati inapendekeza kwamba tukafanye ukaguzi yakinifu. Jamani umevaa shati mbovu bado utafute mtu akuambie kuwa hii shati ni mbovu.
Jengo la Wizara ya Fedha Pemba ni bovu limewekewa miunda, bado utafute mtu akuambie hili ni bovu, uwanja wa ndege Karume umefeli, utafute mtu kutoka nje umlipe fedha akwambie huu umefeli. Mhe. Naibu Spika, tunaumwa na lazima tugangwe kama umevaa shati mbovu basi wewe mwenyewe ujue kama hii ni shati mbovu niivue.

Sasa leo Kamati ya *PAC* wanatuambia eti jengo la Wizara ya Fedha Pemba limeekewa miunda kutoka chini mpaka juu na baada ya kuekezea migomba miunda yanawekewa maghorofa. Kwa hivyo, serikali itafute mwelekezi aje atuambie hili ni bovu, basi tufuteni tuwalipe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niseme jengine kuhusu fedha za Vikosi katika *Account* ya *Canteen*. Kamati ya *PAC* wametuambia kwamba JKU milioni 610 hazijakaguliwa na *CAG* hajafika kukagua. Kutokana na hali hiyo, ninahakika na vikosi vyengine vya KMKM, Mafunzo na vyengine basi ninahakika hali ni kama hii.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atueleze kwa nini Ofisi ya *CAG* haipati fursa ya kwenda kukagua sehemu hizi na hizi ni fedha za umma za walipa kodi. *(Makofi)*

Mwisho kabisa niseme kwamba ukurasa wa 129 mpaka 130 Kamati ya *PAC* imeeleza wazi kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko alikimbia kwenye kamati na hakutaka kutoa mashirikiano. Kwa kweli nadhani niseme kwamba sisi ndio wakosa, yaani Baraza hili ndio wakosa, kwa sababu siku ambayo Baraza litaamua kumshughulikia Waziri au Katibu Mkuu basi siku hiyo hiyo mambo yatakaa sawa, lakini muhali ni mwingi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, serikali hii ikawa hatujaamua sisi kuwashughulikia watu hakuna atayewashughulikia na wala musidhani kama mawaziri watashughulikiana na hawawezi kushughulikiana. Kwa hivyo, tusidhani kwamba kuna siku Rais atawashughulikia mawaziri, hawawezi kushughulikiana, isipokuwa ni sisi wenyewe dhima ya kuwasaidia wananchi kuwashughulikia watu. *(Makofi)*

Sasa leo Kamati imelipwa wiki mbili fedha nyingi Katibu Mkuu anakimbia, kiasi ameteuliwa na Rais, tunajua ukiteuliwa na Rais ukitangaziwa pale unakuwa mkubwa sana na mimi nimetangaziwa na Tume ya Uchaguzi Wilaya na mwenzangu Rais amemtangazia ni jambo kubwa sana hilo, lakini ni jambo ambalo ni aibu. Kwa hivyo, Katibu Mkuu anakimbia kamati, ambapo kamati ambayo fedha za wananchi ndizo anazolipwa yeye, kesho nina hakika Katibu Mkuu atafanya hima mpaka aje.

Kutokana na hali hii mimi naona sisi wenyewe ndio tatizo, hebu tuamue mara hii na mimi ningemuomba Mhe. Salmin Awadh Salmin Mnadhimu wa CCM, mara hii mchague Waziri ambaye hafanyi kazi utukabidhi tumtoe na Mhe. Abdalla Juma Abdalla Mnadhimu *CUF* mchague Waziri upande wako ambaye hafanyi kazi tumtoe, kwani hatuwezi mnawalinda nini? Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Salmin Awadh Salmin mchague waziri ambaye kazi haiwezi tumtoe na Mhe. Abdalla Juma Abdalla na yeye pia afanye hivyo na tunataka tuanzie hapo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, ahsante nimeshapewa kazi ambayo ni nzito kweli na sijui nitamtoa nani. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu nikaweza kuchangia hoja hii iliopo mbele yetu, hoja muhimu ambayo inahusu Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika.

Kwanza kabla sijatoa mchango wangu nitumie nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* Mwenyekiti wa Kudumu wa Kamati ya *PAC*, kwa ripoti yake

nzuri iliyotimia na haikuficha hata neno moja. Kwa hivyo, tunakupongeza sana na pia tunawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, leo tumefanya kazi mbili ambazo zipo kwa mujibu wa kanuni. Kazi ya kwanza tuliyoifanya ni kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotangulia, ambapo kwa mujibu wa Kanuni yetu ibara ya 108 inaitaka serikali kueleza namna ya utekelezaji wa ripoti iliyotangulia.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, tumepokea Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili kama nilivyotangulia kusema jana ni jambo jipya, lakini ni jambo muhimu sana na kwa sababu tunapata vipimo namna serikali inavyoweza kutekeleza maagizo na majukumu yake kwa umma na hapa ndipo kwenye kipimo. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Naibu Spika, wakati Waheshimiwa Mawaziri walipokuwa wakitekeleza moja ya kifungu cha Kanuni ya kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa maagizo ya *PAC* pamoja na hoja za *PAC* katika ripoti iliyopita, kwa kweli kazi ile haikuonesha picha nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wapo Waheshimiwa Mawaziri ambao hawakuwepo kabisa na taarifa zao hazikujulikana kabisa. Sasa hebu tuangalie jinsi ya umakini wetu ulivyo katika kusimamia shughuli hizi za umma, yaani *seriousness* yetu ikoje katika jambo hili, kwa vyovyote jibu lake utaona kwamba bado tuna mzaha katika masuala haya. *(Makofi)*

Pia wapo Waheshimiwa Mawaziri ambao walitoa majibu ya ripoti mpya, yaani hoja mpya ambazo zinatakiwa zije zijibiwe kikao kijacho nao wamejibu, wanajibu ripoti ya leo. Mhe. Naibu Spika, wapo Waheshimiwa Mawaziri walikuwa hawajui hata kile cha kufanya. Kwa hivyo, hayo yote Mhe. Naibu Spika tumeyashuhudia leo na hiyo ndio picha halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Baraza lako tukufu lingetegemea serikali kupitia wizara mbali mbali kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbali mbali zilizotolewa na *PAC* katika ripoti yake ya Kamati iliyopita na hilo ndilo tulikuwa tukitegemea. Kuangalia hoja zile ambazo zimeshughulikiwa vipi, zile ambazo hazijashughulikiwa ziko vipi na utaratibu uko vipi na mipango iko vipi na hilo ndilo tulikuwa tukitegemea Mhe. Naibu Spika, lakini hakuna tulililoliona. *(Makofi)*

Kwa kweli jambo hili ni la kusikitisha sana na wala si la kufurahisha hata kidogo. Mhe. Naibu Spika, kinachoonekana ni kwamba bado tunafanya kazi kwa mazoea. Zamani Mhe. Naibu Spika, Ripoti hizi za *PAC* zilikuwa zikishakusomwa na kuelezwa zikishatoa taarifa zao, basi tunaondoka na makabrasha yetu ndio yamekwisha, yaani ndio yamekwisha.

Lakini leo utaratibu huu mpya tulioanzisha unatusaidia kuona namna serikali inavyo-*act* katika masuala haya hususan katika masuala yanayohusu maslahi ya umma, yaani fedha za wananchi au umma. Kwa hivyo, bado inaonekana serikali, mawaziri na watendaji tunafanya kazi kwa mazoea. *(Makofi)*

Jambo hili Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kila wakati analisisitiza jambo hili kwamba jamani tuache kufanya kazi kwa mazoea na mwenyewe anayo lugha anaisema "*business as usual*" na Mhe. Rais ameliona hili. Kwa kweli wakati huu tulionao ni tofauti na wakati uliopita. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, unakumbuka Baraza la Wawakilishi lililopita kulikuwa na upande wa Chama Kinachotawala na upande mwengine kunakaa Chama cha Upinzani. Sasa upande wa chama kinachotawala kuanzia mawaziri mpaka *backbenchers* wao wanatetea serikali tu, likiwa zuri au baya linatetewa na serikali, na kwa upande wa chama cha upinzani wao kazi yao kupinga tu, liwe jambo zuri au baya wao kazi yao kupinga tu na huko ndiko tunakotoka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa hatuko huko na tuko kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa na mawaziri 9 wa chama kinachotawala na mawaziri 7 wa upande wa upinzani na *backbenchers* tumechanganyika sote tunaisimamia serikali. *(Makofi)*

Mhe. Rais anapowateua mawaziri pamoja na watendaji maana yake lengo lake wamsaidie, Rais peke yake hawezi kufanya kazi hizi ndio maana anatafuta Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Makamishna, ili wamsaidie katika utekelezaji wa shughuli za umma na hilo ndio lengo. Sasa kama hatutamsaidia Mhe. Rais katika majukumu haya basi tutafika pahala tutashindwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tokea Baraza hili lianze tumekuwa tukisema sana, lakini naona dalili kwamba tutafika pahala tutachoka kusema. Kwa kweli hii kusema si maana kazi yetu kulaumu tu, isipokuwa tunataka tufanye kazi ya umma kwa pamoja tushirikiane, pale panapotokezea matatizo tushirikiane, ili tutatue nchi yetu iende

mbele na hili ndio lengo, lakini dalili naziona kwamba tutafika pahala tutachoka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia mambo katika ripoti hizi tutazungumzia kwa ujumla, kwamba kuna mambo ambayo *PAC* katika ripoti yake ya mwaka 2011/2012 kuna mambo hapa kwenye ukurasa wa 59, mambo ya msingi yaliyobainika katika ukaguzi wa kamati wameorodhesha hapa.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo karibu 7 ya msingi kwa ujumla, ambayo haya yamekutikana katika wizara tofauti na wakayatolea ufafanuzi, wakashauri pamoja na kutoa maoni juu ya namna ya kuyashughulikia masuala haya. Jambo la kusikitisha Mhe. Naibu Spika, mambo hayo ambayo yalizungumzwa kushughulikiwa katika ripoti ile yamejitokeza katika ripoti hii ya leo. *(Makofi)*

Kutokana na hali hii hivi tuseme mambo haya yameshindikana au ndio kazi yetu kusema tumesema tumemaliza, lakini ni mambo ya msingi ambayo serikali ilikuwa inahitaji kuyashughulikia, ili yasitokezee kwa sababu ni kasoro katika masuala mazima ya ushughulikiaji wa masuala ya fedha za umma.

Mhe. Naibu Spika, kuna kitu hapa kwenye hoja ya mwanzo PAC inasema kutowepo kwa Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu za Serikali (*Fixed Asset Register*) kwa taasisi nyingi za serikali, bado tatizo la kutowepo kwa Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu za Serikali linaendelea miongoni mwa taasisi nyingi za serikali licha ya ukweli kwamba mafunzo na muongozo wa uwekaji wa daftari hilo umeshatolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa watendaji wa taasisi za serikali. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Naibu Spika, lugha hii bado inaendelea kujirudia na kama utaichambua hoja nyingi zilizowasilishwa humu bado zinaelekeza katika eneo hili, tunashindwa nini kutekeleza jambo hili? Ugumu wake uko wapi? Kwa kweli hoja zilizowasilishwa na *PAC* bado zinaelekeza tatizo hili lipo katika wizara za serikali na taasisi mbali mbali za umma. *(Makofi)*

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambapo ni hoja ya pili inasema kutofuatwa kwa Sheria ya manunuzi ya Sheria ya Fedha (*Public Finance Act and Public Procurement and Disposal and so and so*). Hivyo, kamati imebaini kwamba taasisi nyingi za serikali hazifuati Sheria za Manunuzi na Sheria za Fedha hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ambapo mara nyingi matumizi hayo yamekuwa yakifanywa kwa njia ya mazoea badala ya kufuata taratibu za kisheria.

Aidha Kamati imebaini kutowepo kwa vyombo muhimu vya kusimamia masuala ya fedha na manunuzi kama ambavyo imeelezwa katika sheria hizo. Kwa mfano, Bodi ya Zabuni (*Tender Board*), Kitengo cha Manunuzi (*PMU*) na Kamati za Ukaguzi (*Audit Committee*).

Mhe. Naibu Spika, hoja hii ni nyingi ndani ya kitabu hichi na bado mambo hayo hayajashughulikiwa na bado hakuna Sheria ya Manunuzi na Sheria za Fedha, utawezaje kushughulikia masuala ya fedha, pia utawezaje kutumia bila ya kufuata taratibu hizi za *Procurement,* hivi wenzetu mnatumiaje fedha hizi za umma bila ya kuwa na *unity* kama hizi.

Mhe. Naibu Spika, ndio maana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk akasema kwamba *PAC* sasa watembee na polisi na pingu, kwa sababu tunatumiaje fedha za umma bila ya kuwa na utaratibu huu wa sheria ambao tumeweka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, bado dakika zangu tano.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tatu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, tulipokwenda Uganda tuliwauliza wenzetu wanafanyaje Kamati ya *PAC*, walisema sisi *PAC* inatembea na polisi kila wapokwenda basi wanakwenda na polisi, wakiona pahala kuna wizi wanasema mkamateni kamfungulieni mashtaka, ndio hizi nchi za Afrika lazima iwe hivyo, lakini kwa kupiga kelele namna hii inakuwa hatwendi.

Lakini haya yapo mengi saba na mengine na mkiyasoma Waheshimiwa Wajumbe mtayakuta kwamba yapo na yanaendelea kuwepo na wala hakuna hatua zozote zinazochukuliwa, katika hali kama hii tutafika wapi.

Kwa hivyo, niiombe sana serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba jamani tuwe makini katika kusimamia mambo haya, kwa sababu sisi tunaamini kwamba mambo haya hayafanywi na Mawaziri isipokuwa yanafanywa na watendaji, lakini jukumu letu kama mawaziri ni kusimamia mambo haya au kuwasimamia watendaji, ili mambo haya yaweze kurekebishika na hiyo ndio dhamana yetu.

Kwa kweli masuala ya matumizi na manunuzi ni mambo yanayofanywa na watendaji, Makatibu Wakuu na wenzao, lakini sisi kama mawaziri jukumu letu ni kuhakikisha mambo yale yanayofanywa yanafuata taratibu za kisheria na wala si vizuri kila siku yanajitokeza na wakati sisi wasimamizi tupo. Mhe. Naibu Spika,

kusimamia jambo sio unyapara Mwalimu Nyerere alisema, kusimamia jambo ni kutimiza wajibu wako, ili kuona jambo lile linakwenda kadri ya vile lilivyopangwa. *(Makofi)*

Mwisho Mhe. Naibu Spika, kwa kuheshimu muda wako, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kutumia risiti za serikali. Kinachoonekana ni kwamba kuna stakabadhi ambazo zimekosa taarifa za *tin number* na mambo mengine na risiti hizo huwa zinatumika na serikali yenyewe ambazo si za kiserikali, lakini na hata taasisi za watu binafsi.

Wakati *PAC* inapotaka ushahidi au stakabadhi za manunuzi, basi risiti zinazotolewa hazina *tin number* ni risiti hizi za kienyeji, hapa Mhe. Waziri wa Fedha serikali inakosa mapato. Kwa maana hiyo, kama serikali imenunua kitu kwa mtu na akatumia stakabadhi ambayo haikubaliki haina *tin number* maana yake serikali yenyewe inajikosesha mapato ndio tafsiri yake, kwa sababu huyu anayeuza na yeye alikuwa na *right* ya kulipa, sasa kama anatumia stakabadhi zisizokubalika au si za serikali maana yake serikali inakosa mapato.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, suala hili tumeiomba mara nyingi *ZRB* kutayarisha risiti za serikali ambazo zitakuwa zinatumika kama ushahidi au stakabadhi kwa ajili ya malipo mbali mbali, ili wafanyabiashara na wao waweze kwenda kuzinunua stakabadhi zile katika Bodi ya Mapato, ili stakabadhi hizo ziweze kutumika, lakini stakabadhi zinazotumika ni za ajabu madukani. Kwa mfano, unakuta huyu ana stakabadhi hii na yule ana stakabidhi ile, yaani hazieleweki na wala hakuna utaratibu wa kutoa stakabadhi. Kwa hivyo, ZRB isimamie suala la stakabadhi, ili wafanyabiashara binafsi waende kule wakanunue stakabadhi ambazo zinatumika na zitakuwa zinaeleweka.

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Naibu Spika mimi nikubaliane na Ripoti hii ya Kamati ya *PAC*, lakini niiombe sana serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, mwakani bado safari ni ndefu, basi ripoti hizi zifanyiwe kazi ipasavyo na waheshimiwa wasimamizi wa mambo haya turidhike na utekelezaji huo, badala ya ripoti hizi kuwa tu kama hivi zilivyo. Pia Waheshimiwa Mawaziri wawepo wakati wa kupitisha shughuli hizi, na kwa sababu haya tunayoyasema yote hawayasikii, hawayajui, hawajui kumejadiliwa nini. *(Makofi)*

Jambo la mwisho Mhe. Naibu Spika, tuachane na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea, kwa sababu tukiendelea kufanya kazi kwa mazoea, basi tutafika pahala tutawekana pahala pabaya na hatimaye tutakuja kulaumiana.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii, ili niseme machache kuhusu ripoti hii ya Kamati yangu ya *PAC*.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa kamati hii na kwa hivyo nina uzoefu au ushahidi wa haya ambayo wenzangu wameyazungumza na mimi nitazidi kuyasema.

PAC kazi yake kubwa pamoja na mdau wake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG)* ni kujaribu kuangalia au kudhibiti matumizi ya serikali. Lengo kuu Kamati ya *PAC*, lakini pamoja na Ofisi ya *CAG* ni kuhakikisha kwamba matumizi ya serikali yanafanywa kwa uadilifu na kwa kufuata Sheria ya Fedha. Sasa kadri tulivyofanya kazi na kwa bahati nzuri ni mara nyingi nimewahi kuifanyia kazi Kamati hii ya *PAC* kuna mambo yanakuwa yanajirudia, yaani kuna makosa yanakuwa hayarekebishiki kirahisi.

Kwa mfano, mimi mara nyingi huwa nawaambia watendaji ni aibu kuwa mpaka leo tunashindwa kukusanya zile *documents* katika matumizi yetu, zile *supporting documents* kwenye *voucher* unakuwa huzikuti. Mhe. Naibu Spika, wenzetu hivi sasa wameondoka katika ukaguzi wa namna hii na wamepiga hatua wako kwenye *value for money* sasa na sisi mpaka leo tunahimizana risiti haipo, sijui kitu gani hakimo humu.

Kwa kweli ni aibu na ni aibu kwa sababu serikali inajitahidi sana kusomesha Wahasibu kwa gharama kubwa na imeajiri wahasibu wa kutosha na kila taasisi inaye mhasibu ambaye ni *qualified*. Lakini bado unakuta matatizo ya *supporting documents* hazimo katika matumizi.

Mhe. Naibu Spika, mimi mara nyengine huwa ninajiuliza hivi ikiwa mhasibu anashindwa kukusanya *supporting documents* katika matumizi yake, basi ana haja gani kuwepo si bora awekwe Abdalla Juma ambaye hana taaluma ya uhasibu ndio afanye mambo haya, maana yake anajua umuhimu wa *supporting documents* na sheria ndivyo inavyomuongoza, lakini bado mpaka leo karne hii tuliyonayo haoni

umuhimu wa kukusanya risiti na kuziweka mule, sasa ana haja gani mhasibu yule kukaa pale.

Jambo jengine pia ni ukiukwaji wa sheria ni suala ambalo wenzangu wamelizungumza sana na hata katika ripoti yetu limezungumzwa kwa kina sana ni kuhusu ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka. Mhe. Naibu Spika, suala hili halifanyiki kwa baadhi ya taasisi, yaani kuna wengine hawafungi kabisa na kuna baadhi wanafunga lakini wanazichelewesha kuzipeleka kwa *CAG*. Sasa matokeo yake huwezi kupata, maana yake athari yake hii kutofunga hesabu na taasisi moja tu ikiwa haikufunga hesabu basi serikali nzima haiwezi kuleta hesabu zilizo sahihi.

Kutokana na hali hiyo, hesabu za serikali zitakuwa pungufu kwa sababu kuna taasisi hawakuweka mahesabu yao mule. Kwa mfano, mpaka leo kuna taasisi hapa zimetajwa ambazo ni nyingi tu taasisi 11 hazikufunga au kama zikifunga basi zinachelewesha na nyengine ni taasisi ambazo zinakusanya mapato.

Mhe. Naibu Spika, ukiniambia Baraza la Manispaa halifungi hesabu au *ZRB* ama Mfuko wa barabara hizi ni taasisi nyeti ambazo zinakusanya mapato yetu, sasa leo kama hazifungi hesabu hivyo serikali itajuaje kilichokusanywa, na kama serikali haiwezi kupata *transparency* ya hii maana yake nini? Maana yake kuna watu wanaiba fedha za serikali.

Sasa nadhani wakati wa kuvumiliana Mhe. Naibu Spika chombo hiki ni cha wananchi tunayo dhima kubwa sisi ya kuhakikisha kama fedha za wananchi hazipotei kiholela kama kuna taasisi mpaka leo hazifungi hesabu kwa makusudi, basi mimi nafikiri si wakati wa kuvumiliana tena, maana yake tukiendelea kuvumiliana katika hali hii na wala tusiwe na ndoto kama siku moja nchi yetu itaendelea, kwa sababu wenzetu walioendelea wameondoka katika masuala kama haya.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri hivi sasa ni wakati wa kuchukua hatua kwamba Mhasibu haleti mahesabu basi Mhasibu Mkuu fukuza lete mwengine na huyu ni mwizi anatuibia ndio maana yake.

Tatizo jengine ambalo tumekumbana nalo mara nyingi ni kuhusu Mashirika ya Umma, ambapo kuna matatizo mawili. Kwanza wao wanaongozwa na sheria nyengine isiyokuwa hii Sheria yetu ya Fedha, kwa hiyo ndani ya sheria hiyo wanalazimika kumuajiri *Auditor* ambaye si wa serikali.

Vile vile tatizo jengine hawa ule mwaka wao wa fedha unaanzia Januari na kumalizia Disemba, kwa hivyo hata wakifunga mahesabu yao hawapati kuyapeleka kwa *CAG* kwa sababu ya muda ule ambao wafunga mahesabu. Sasa hii inaleta ile kasoro niliyoizungumza kwamba mahesabu ya mashirika kama haya mara nyingi yatakuwa hayamo katika hesabu za serikali kwa jumla. Sasa nadhani hapa pana umuhimu wa kurekebisha sheria tukawa na sheria moja tu ambayo na mashirika ya serikali nayo yatafuata sheria ile ile.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, ni taarifa hii ambayo tumeigundua katika ripoti ya *CAG* kwamba katika mwaka 2010/2011 kuna matumizi karibu ya shilingi bilioni mbili mia tatu na sabiini na saba milioni laki tatu na thamanini na tatu ambazo hazikufuata utaratibu wa sheria ya fedha. Bado naendelea kusema Mhe. Naibu Spika, kutofuata sheria ya Fedha ni dalili moja mbaya na ni dalili ambayo mimi nasema kwa lugha ya chap chap ni kwamba kama unatumia bila ya kufuata sheria ya fedha maana yake una mambo yako unafanya. Tabaan kuna wizi mkubwa katika fedha hizi, na hizi si kiwango kidogo cha fedha bilioni mbili zinatumiwa kiholela holela tu. Sasa hii ni hatari kubwa Mhe. Naibu Spika, na hii inaonesha ile kawaida yetu ya Kizanzibari, maana yake Wazanzibari tuna tabia moja ya kutokuwa *serious* katika mambo tunafanya vile tulivyozoea.

Mhasibu anatumia anakwambia nitakuja kukusanya baadae *document* au chukua utaniletea baadae au iweke hapo halafu inapotea wakija maafisa wa *CAG* wanakuta mule mna mapungufu ya *document* kadha wa kadha, matokeo yake ndio yanakushanywa kushanywa wanapata kitu kama hiki, bilioni mbili zimetumika kiuzembe uzembe.

Kwa kweli bado naendelea kusema hii si hali ya kuiachia kwa sababu tukiendelea kuachia mambo kama haya, basi tutaendelea kufuga wizi wa pesa za umma jambo ambalo kwa kweli halitotupeleka pahali pazuri. Na kuna hatari wananchi wanaofuatilia nyenendo hizi wakafika pahali wakaondoa imani kwa serikali yao. Sasa mimi nadhani serikali ina wajibu Wahasibu kama hawa kwa kweli mimi ninawachukulia kama wameshindwa kazi, ni afadhali wakae pembeni watafute watu wengine watakaokuwa *serious* na kazi.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo tumeligundua ni ukusanyaji wa mapato wenye udhaifu mkubwa. Kwanza makisio ya taasisi pale wanapokisia kuwa mwaka huu tunakusudia kukusanya kiasi fulani kwa kweli hayafanywi kitaalam, kwa sababu kwenye bajeti hapa taasisi fulani inatwambia kwamba mwaka huu tunapanga kukusanya hiki na hiki na tunaomba ruhusa hiyo. Lakini matokeo yake mwisho wa mwaka tukipokea ripoti, tunakuta taasisi ile imekusanya mara mbili

zaidi ya ile iliyoombea ruhusa. Sasa hii kama hawafanyi makusudi basi itakuwa wana kasoro kubwa ya kuweza kukisia kile ambacho wanaweza wakakusanya.

Lakini udhaifu wa pili katika ukusanyaji mapato Mhe. Naibu Spika, ni usimamizi usioridhisha wa mapato ya serikali. Tuna vyanzo vingi vya mapato na siku zote mimi nasema kama vitasimamiwa vizuri basi vinaweza vikaleta maendeleo makubwa katika nchi yetu lakini vyanzo vyetu vya mapato inaonekana havisimamiwi vizuri na mapato mengi hayakusanywi. Mhe. Naibu Spika, mpaka leo pamoja na juhudi wanazofanya *ZRB* na *TRA* sijui na nani lakini mpaka leo wafanyabiashara wanakuuzia hawakupi risiti kama hujang'ang'ania hawakupi risiti mpaka leo, na mule mapato mengi sana ya serikali yanapotea.

Sasa matokeo yake yanakuwa nini? Matokeo yake ni kuongeza viwango vya kodi katika zile taasisi ambazo zinalipa kodi. Kwa mfano mwaka huu na hili kwa kweli naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha aje anijibu vizuri. Mwaka huu leseni za magari, *road licence* zimepandishwa kimya kimya kwa karibu asilimia 150. Gari uliyokuwa ukikata *road licence* kwa shilingi 36,000 au 40,000 sasa hivi iko karibu 90,000 mpaka 100,000 ni kiwango cha kutisha. Wakati ilikuwa hakuna ulazima wa kuongeza kiwango chote hicho, mimi nadhani watu wakusanyaji mapato wangefanya kazi vizuri katika hawa wafanya biashara tungeweza tuka-*cover* hilo pengo tulilonalo.

Hivi karibuni tumesikia kama Shirika la Bima nalo linakusudia kuongeza kiwango cha Bima kwa karibu ya asilimia 150 tushasikia. Sasa tunakamua humo humo tu wakati kuna sehemu hamfanyi kazi mkapata pesa. Hii ni kasoro kubwa.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, ni uvujaji wa mapato ya serikali. Na katika hili tumeligundua kwanza mashirika mengi ya umma hayalipi lile gawio la fedha kwa serikali. Haya yameelezwa kwa kina sina haja ya kusema sana.

Lakini jambo jengine Mhe. Naibu Spika, kuna taasisi za serikali zinafanya biashara humu, kwa mfano Vikosi vya SMZ, Vikosi vya SMZ sasa hivi vinafanya kazi kubwa sana biashara ya kujenga majumba na wanaingia *contract* kubwa kubwa lakini fedha wanazopata hatuzioni wanatumia nguvu kazi ya serikali, wanatumia wakati wa serikali lakini ukija ukiwauliza haya *contract* hii mmeiingizia serikali kiasi gani hakuna tumeiona hiyo kwenye JKU, tumeiona hiyo kwenye KMKM.

Sasa hii ni aina moja ya upotevu wa pesa za serikali. Mimi nadhani kuna haja sasa na niliwahi kutoa ushauri huu kama Vikosi vyetu vina Kampuni za Kujenga basi ni afadhali Kampuni zao wakazisajili rasmi na wakawa wanalipia ile kodi

inayotakiwa ilipiwe serikalini kwa makampuni. Lakini wasitumie muda wa serikali na nyenzo za serikali na kila kitu cha serikali wewe huku unapokea mshahara lakini unakwenda kujenga huko unapata pesa haziingii serikalini, kwa kweli sio uzuri.

Jambo jengine kuna misamaha ya kodi ya kinyemela. Mhe. Naibu Spika, kuna mtindo sasa hivi kuna hii *exemption* inayotolewa labda kwa mahoteli ya kitalii kuna mambo nyeti. Kumbe ujanja unaofanyika kama mtu anahitaji mifuko 200 ya saruji anakwenda kuomba *exemption* anapewa lakini analeta mifuko 1000 mengine anaiuza kwa njia zake mwenyewe anazojua. Kwa hivyo hapa lazima serikali iwe makini sana katika kutoa *exemption*.

Jambo jengine haraka haraka Mhe. Naibu Spika, ni upoteaji wa mali za serikali kiholela. Serikali inakuwa haizijui mali zake na hiyo inatokea kwa sababu mpaka leo kuna taasisi za serikali hazina *fixed asset register* mpaka leo pamoja na juhudi zote ambazo *PAC* imefanya, pamoja na juhudi zote za Wizara ya Fedha kutoa miongozo hii na hii lakini mpaka leo unakwenda kwenye taasisi ya serikali hawana *fixed asset register* mpaka leo. Maana yake nini? Maana yake taasisi ile mali za serikali hazijulikani, na kwa sababu hazijulikani mtu anaweza akaiba nyumba, akaiba gari akaiba chochote anachotaka kuiba wala serikali haina habari, ndio maana ya kukosa daftari. Wanasema *mali bila daftari hughibu bila ya habari*.

Kwa hivyo, mpaka leo Mhe. Naibu Spika, kuna taasisi za serikali hazina hati miliki za mali zake mpaka leo. Ukishakuwa huna hati miliki maana yake nini? Maana yake hiyo mali si ya kwako na mtu yoyote akiwa mjanja anaweza aka-*complain* akatengeneza hati miliki ya kwake akaja akalalamika na serikali hapo ikashindwa siku zote ndio inavyotokea. Kwa hivyo haya si mambo kabisa ya kupuuza. Serikali lazima iweke utaratibu maalum wa kuhakikisha kama mali zake zote zina hati miliki.

Mhe. Naibu Spika, mpaka leo kuna magari ya serikali, pikipiki, vespa mpaka leo hazina magamba yale ya umiliki mpaka leo. Mtu akishagundua kama gari hii kama haina ile kadi si anaweza akachukua tu akafanya anavyotaka. Kwa hivyo mali za serikali kwa kweli zinaendelea kupotea kwa wingi sana na kama hatukuwa macho tutakuwa tunahesabu nyumba fulani ni yetu au gari fulani ni yetu kumbe si ya kwetu kabisa na ukienda mahkamani serikali itashindwa.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo kwa kweli kamati yetu imelibaini kila pahali ni kwamba kuna ile sheria ya manunuzi; *procurement act* ina mapungufu makubwa katika taasisi za serikali. Kwa sababu mpaka leo mule kama *PMU*

hazimo, *tender board* hazimo katika taasisi za serikali sio mote wengine tayari wanazo lakini kuna wengine mpaka leo hawana.

Lakini mpaka leo kuna watu hawapangi *procurement plan* mpaka leo. Na hili suala la *procurement plan* hili ni tatizo la nchi nzima. Mimi nilidhani kwa sababu ni serikali moja basi *procurement plan* kila taasisi itakuwa ya aina moja. Lakini leo unaweza ukaenda kilimo kuna yake, ukienda Wizara ya Fedha wana yao, ukienda sijui kwa Mhe. Haji Omar kuna yao wana nyengine, yaani zinatofautiana. Sasa mimi nadhani huo si utaratibu mzuri sijui tatizo liko wapi, lakini mambo kama haya ilikuwa ni muhimu yawekewe *formula* ya aina moja, ikiwa *procurement* wizara zote iwe hivyo hivyo maana yake.

Jambo jengine la mwisho ambalo nakusudia kulisema Mhe. Naibu Spika, ni kwamba sisi *PAC* mdau wetu mkubwa tena kwa mujibu wa Katiba ni Ofisi ya *CAG*. Ofisi ya *CAG* ndio iliyo na jukumu la udhibiti wa matumizi ya Serikali na Ofisi ya *CAG* inajielekeza zaidi kwenye ukaguzi yakinifu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, ukaguzi yakinifu unahitaji matayarisho makubwa. Kwanza bajeti yao *CAG* ni ndogo sana mpaka leo, na kwa hivyo hawana uwezo wa kuzikagua taasisi nyingi za serikali mpaka leo hawawezi. Kuna taasisi kibao tunakwenda *CAG* bado hajapita na halaumiki kwa sababu hana bajeti. Lakini pili wafanyakazi wake alionao bado ni kidogo hawamtoshi. Na tatu tukienda katika ukaguzi yakinifu anahitaji wataalam wa kuweza kuchambua mambo ya kitaalam zaidi mainjinia kama kujenga hana. Sasa nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa kweli aitupie ofisi hii macho, kuimarika kwa ofisi hii ndio udhibiti wa mali za serikali, udhibiti wa fedha za umma tunaweza tukadhibiti itakiwavyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache mimi naunga mkono ripoti hii ya *PAC* kwa asilimia 100.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi jioni ya leo nikaweza kuchangia hotuba hii au ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika yake, iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kazi nzuri ya uwasilishaji aliyoifanya asubuhi hii ya leo pamoja na Wajumbe wote wa Kamati na mimi mwenyewe nikiwemo.

Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kushukuru Ofisi ya *CAG* kwa jitihada zake za kuiwezesha Kamati hii kimafunzo ikaweza kutoa ripoti kama hii leo. Hizi Mhe. Naibu Spika, ni jitihada ambazo zilikuwa zinafanywa sana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu akishirikiana na Wizara ya Fedha. Kwa hivyo niwape pongezi kwa usaidizi wao walioisaidia Kamati hii mpaka ikaweza kuwasilisha ripoti hii leo.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu katika ripoti hii utaanzia kama mnadhim wangu wa Chama cha Mapinjduzi aliposema pale amelalamika namna ya serikali ilivyokuwa inaichukulia ripoti hii kwa wepesi. Kwa nini nasema hivyo.

Mhe. Naibu Spika, Mnadhim amezungumza sana juu ya jambo hili kwamba *PAC* inawasilisha ripoti lakini ule mchanganuo wa ripoti iliyopita ule uliowasilishwa na mawaziri hapa ukiutizama kama utaukusanya wote hapa *paper* moja ninafikiri haujai kwa kweli si kitendo kizuri. Lakini Mhe. Naibu Spika, ukiangalia *PAC* inatofautiana kidogo na Kamati nyengine za kudumu. Maana Kamati hizi za kudumu hizi nyengine utakuta labda Kamati ina Wizara mbili, Wizara tatu sijui kama kuna Kamati ina Wizara nne sina uhakika.

Lakini *PAC* wizara zote za SMZ pamoja na mashirika yake zinakaguliwa au zinapitiwa na Kamati hii. Sasa kwa kuwasilishwa ripoti hii leo, ninafikiria mimi ningefikiria hivyo viti vya Waheshimiwa Mawaziri vyote vingekuwa vimejaa kwa kusikiliza yale ambayo yatakuwa yamewasilishwa na michango ya Wajumbe juu ya ripoti hii.

Vile vile leo ningeona huko juu kumejaa watendaji, ma-*accounting officers*, wahasibu na watu wanaoshughulikia zile mamlaka za fedha kuja kusikiliza kile ambacho labda kimegundulika katika taasisi zao. Lakini nikitupia kwa haraka haraka pale naiona labda timu ya Wizara ya Fedha imekuwa hii ripoti kama ya Wizara ya Fedha peke yake, wakati ripoti hii ni ya serikali nzima. Kwa hivyo mimi niungane mkono na mawazo aliyoyatoa Mnadhim wangu wa Chama cha Mapinduzi kwamba serikali inaonekana haiko *serious* katika kuzifanyia kazi ripoti zinazowasilishwa. Mfano hai ndio huu tunaouona Mhe. Naibu Spika.

Baada ya utangulizi huo Mhe. Naibu Spika, sasa kidogo niingie kwenye hii ripoti mimi nitaanzia na miradi ambayo ilikuwa ikifadhiliwa na Wizara ya Fedha, miradi ile ninafikiria kwa sasa itakuwa haipo maana yake ndizo zile fedha zimehamishwa zimepelekwa Ofisi ya Makamu wa Pili kwa ajili ya kupeleka Mfuko wa Jimbo *CDF*.

Katika pitapita yetu kule Mhe. Naibu Spika, tukuwa tunakagua sasa unaweza ukakuta mimi nimepata shaka kidogo unakuta labda jimbo au kamati ya maendeleo ya chochote kile ambacho wamejipangia wameomba fedha pale Wizara ya Fedha labda milioni tano kwa ajili ya kuendeleza ile shughuli yao waliyonayo. Lakini fedha ambayo ilikuwa inatolewa pale wanapewa milioni tano ya kimaandishi unaambiwa milioni tano lakini kule unakatwa laki tano wanasema hizi za utendaji.

Sasa tulikuwa tunahoji mimi nilikuwa nataka Mhe. Waziri aje atusaidie laki tano zile ambazo zinachukuliwa na maofisa wale za kazi gani. Walioomba walipaswa wapewe pesa zile wenyewe, milioni tano kwa ukamilifu. Lakini unapozichukua laki tano ukanambia za utendaji, wakati watendaji wale wa Wizara ya Fedha wanalipwa mshahara, ukiuliza sana wanasema aa pesa za mafuta kwendea kule shamba kushughulikia, sijui kufuatilia lakini huyu anaesema haya yeye ni Afisa wa Wizara ya Fedha. Analipwa mshahara, kama ni posho kama ni nini kwa ajili ya shughuli ile sasa na huku fedha ile ambayo ilikuwa wapelekewe wananchi anaikata laki tano, sasa hapa mimi napata shaka kidogo.

Sasa hebu kidogo Mhe. Waziri atakapokuja kujibu hizi hoja atusaidie hizi, hizi laki tano wanazozichukua hizi kwa mantiki ipi maana mimi siioni sasa aje atusaidie kidogo. Na hili haliko kwake tu kwenye Wizara ya Fedha lipo hata kwenye miradi ya *TASAF*. Kwenye miradi ya *TASAF* wanachukua 10% ya fedha ambazo zimeombwa na wananchi, sasa unapata mashaka kidogo. Mmekaa wananchi wamepiga hesabu zao labda mradi wao huu uta-*cost* kiasi hichi, sasa ukiichukua 10% ile fedha ndio inakuwa haitimii na kama haitimii maana yake lile lengo lililokusudiwa halifikiwi.

Lakini wakati huo huo *TASAF* mimi kuna kitu wananishangaza vile vile kwa mfano natoa ndani ya jimbo langu la Mkwajuni. Kulikuwa na mradi wa ujenzi wa skuli ya Potoa pale. Skuli ya Potoa ile ukiitizama imezungukwa karibu na shehia tatu hivi. Maana kuna shehia ya Potoa, Shehia ya Muwange na kuna shehia ya Pitanazako, ambayo hii shehia ya Pitanazako iko kwa Mhe. Haji Omar Kheri Jimbo la Tumbatu lakini wanatumia Skuli ya Potoa.
Sasa mradi ni ujenzi wa Skuli ya Potoa lakini utakuta ule mradi wakaugawa katika shehia tatu na kwa kila shehia wanachukua 10% kwa mradi ule ule mmoja kwa nini walikuwa wasichukue 10% moja tu kama ndio utaratibu wao, lakini kwa kila ile shehia wanaichukulia 10%. Sasa kwa mradi mmoja ule hawakuchukua 10% wamechukua 30% ya ule mradi.

Kwa hiyo, hapa mimi nikawa nimepata shaka sana, kwa hivyo hebu Mhe. Waziri uje utusaidie hao maofisa wenu wa *TASAF* ni watu wa kujitegemea kwamba kipato

chao au mishahara yao itokane na fedha zile wanazoomba wananchi? Na kama nyinyi mnawalipa mishahara na maposho yao fedha hizi ni za kazi gani sasa? Wakati *TASAF* ukienda kuitizama huku ina shughuli za uendeshaji ambazo zinalipwa na Makao Makuu kule. Sasa hizi pesa wanazozichukua 10% za kazi gani? Mhe. Waziri utakapokuja hapa kidogo nataka uje utusaidie.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele kuna tatizo ambalo wenzangu waliotangulia wamelizungumza hasa Mhe. Abdalla pale kuhusu daftari *fixed asset register*, hili daftari la kuhifadhia kumbukumbu za mali zile ambazo za serikali ziko pale. Hili ni tatizo Mhe. Naibu Spika, na tatizo hili tumejaribu kulieleza mara nyingi sana lakini linaonekana bado limekuwa sugu na kwa makusudi kwa sababu mwanzo kila ukiwagusa walikuwa wanarudi wanasema Wizara ya Fedha, lakini Wizara ya Fedha ilishatoa muongozo na imeshatoa mafunzo kwa Wahasibu na wasaidizi wao wale namna ya kuweka hizi kumbukumbu lakini mpaka leo tatizo hili limekuwa sugu hata Mhe. Mnadhim hapa amelikemea sana, na mimi naendelea kusema kwamba huu ni udhaifu wa kutochukuliwa hatua kwa wale ambao wanazembea katika suala hili. Kwa hivyo huu ni udhaifu ambao unaonekana serikali haiko tayari katika hili. Haiko tayari kwa sababu kama ingekuwa inawachukulia hatua wale ambao wanazembea katika tatizo hili, hili suala lingekuwa limemalizika. Lakini bado linaonekana limekuwa sugu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele kidogo hapo mimi naingia kwenye tatizo jengine ambalo tumeliona pale kutofunga mahesabu kwa watendaji wa taasisi mbali mbali wa serikali. Kuna tatizo sugu Mhe. Naibu Spika, unakuta taasisi haifungi mahesabu yake, lakini pale unakuta pana mtu anaitwa Mhasibu pengine Mhasibu Mkuu, vyovyote cheo watakavyokiita wenyewe Mhasibu Mkuu, Mhasibu nani lakini ni mtaalam yule, yule si kama mimi muuza dodo, yule mwenzangu pale kaajiriwa kwa sifa alizonazo.

Lakini utamkuta mtaalam yule anasema kufunga hesabu kwake yeye kunakuwa kishindo. Sasa hapa tunapata shaka kidogo, inakuwaje Mhasibu mzima wewe ushindwe kufunga hesabu, hayo mahesabu unayahifadhi vipi. Sasa hili sisi tumeliona ni tatizo na tatizo hili lipo pale pale la kuoneana haya ambao mtindo huo upo, Mhasibu anachotakiwa ni lazima afunge mahesabu yake lakini unamkuta Mhasibu hata habari hana.

Kama unamuweka Mhasibu hawezi kufunga mahesabu yake sijui Mhe. Waziri wa Fedha unatwambiaje hapa. Maana yake tunachojua Wahasibu wale mnawapa donge nono katika mishahara yao kuliko ninafikiri watendaji wengine, mmewatengea hasa fedha maalum kwamba wanashughulikia fedha hawa kwa

hivyo hata mishahara yao mizito. Lakini kama mtu hawezi kufanya wajibu wake mshahara huo wa nini? Maana haki na wajibu ni watoto pacha asiwe tu mtu anadai haki lakini wajibu wake haujui. Afanye wajibu wake apewe haki yake, hilo hakuna tatizo. Lakini kama mtu hafanyi wajibu wake ile haki ya nini sasa si haki yake.

Sasa hivi nafikiria Mhe. Naibu Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha wakafanya ukaguzi mzuri kwa Wahasibu wao. Namna ambavyo hawafungi mahesabu, utakuwa Mhasibu wanaajiri taasisi nyengine kuja kufunga mahesabu wakati yeye yupo. Unapoajiri taasisi nyengine maana yake unatumia fedha zaidi za walipa kodi na wewe unalipwa mshahara kwa kazi ile. Sasa ningelimuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, kama hawa Wahasibu ambao wapo na hawawezi kufunga mahesabu yao ningeomba ukawaweka kando, ukatuwekea watu ambao wana taaluma ile na wanaweza kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, nasogea kwenye mashirika. Mashirika yetu ya umma haya. Mashirika yetu ya umma haya yanajitahidi kukurupuka, lakini serikali inaonekana kama haiko tayari serikali kuu kuyasaidia mashirika haya ili yaendelee. Mhe. Naibu Spika, nasema hivyo haya mashirika yetu haya, nataka nitoe mfano wa *Zanzibar Insurance* hili Shirika la Bima. Hili ni Shirika ambalo linajitahidi sana na limo katika kupiga hatua kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni tu kama utakumbuka limekamilisha jengo lake jipya pale limehamia. Kwa kweli mimi ninawapa hongera sana watendaji wa Shirika lile kwa kazi nzuri wanayofanya na kuliendeleza lile Shirika. Lakini serikali inawavunja moyo, Mhe. Naibu Spika, Shirika lile lina chombo kinaitwa *regulator* kinachowaweka sawa huko kinachowasimamia katika shughuli zao.

Sasa Serikali wamehama tu kwenye jengo lile la zamani wamehamia jengo jipya serikali imelichukua jengo imewapa Wizara ya Elimu bila ya hata ya kuwataka ushauri wale wenyewe. Wakati wao hawa Shirika hawa ile ni *asset* ambayo inatakiwa kubakia kwenye *record* katika kumbukumbu zao na kuweka kama ni mtaji wa lile Shirika. Yule *regulator* huwa anawakagua kuzitizama zile *asset* walizonazo.

Kwa hiyo, unapoziondosha kuzipeleka katika taasisi nyengine maana yake unawapunguzia mtaji wale na unapowapunguzia mtaji kesho na keshokutwa yule *regulator* anaweza kuwaambia hawafai kuendesha zile shughuli za Bima wafunge. Kwa sababu hawana mtaji wa kutosha kumbe serikali ndio inayowasababishia vile, inachukua tu kwa nguvu zake ilizonazo.

Lakini jambo la kushangaza unachukua jengo lile unawapa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakati Wizara ya Elimu wao wenyewe wana jengo wameliuza kwa Bakhresa lililokuwa Wizara ya Elimu Shangani kule, si la kwao lile kwa nini wasitengeneze kama wanataka kutumia, wao walilipiga mfuko kwa Bakhresa wanakwenda kuomba huko Serikali Kuu wananyang'anywa lile kule. Huu ni uonevu tunayaonea mashirika yetu haya badala ya kwenda mbele yatakuwa hayendi mbele yatarudi nyuma.

Nimetoa mfano wa shirika hili tu laki yako na mengine yanafanyiwa vitu vya namna hiyo na Serikali Kuu. Mimi nafikiri serikali iangalie vizuri kabla ya kutaka kuchukua mali ya shirika lile basi ni vyema wakakaa na wale watendaji wa shirika kwanza waka-*negotiate* wakakubaliana si kutumia nguvu zake tu ikenda ikawapokonya. Kweli serikali ina nguvu na yule ni mtoto wake tu, lakini na yeye ana haki zake, umempeleka pahala kuna chombo kinamsimamia kesho na keshokutwa atapokwamba bwana wee hiki chombo kinanambia mimi nisiendeleze hii biashara utakuja kumwambia mtendaji hafai kumbe serikali ndio iliyosababisha vile.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Vikosi vya SMZ, kuna tatizo kidogo kwenye Vikosi vya SMZ hasa KMKM. Nimepata malalamiko kuna malimbikizo makubwa sana ya fedha za wanajeshi wale za likizo, wana malimbikizo yao ya muda mrefu hawajalipwa fedha zao hizo za likizo.

Mhe. Waziri wa Vikosi yupo hapa mwenyewe atakuja kutueleza tatizo ni nini. Kwa sababu haya malimbikizo wameshakuwa ya muda mrefu. Mwaka jana nakumbuka kwenye bajeti tuliyazungumza haya na alituahidi Mhe. Waziri kwamba haya mambo kama yalikuwepo sasa hivi hamna kitu kila kitu kinamalizwa, bajeti inayokuja hakuna kitu hiki, lakini mpaka juzi nimewasiliana nao baadhi ya maaskari wanachosema fedha zao za malimbikizo ya likizo hawajalipwa. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri tusije tukagongana kwenye bajeti hapa, ayatengeneze mapema hayo ayakamiloisha akija kwenye bajeti na haya bado yapo tutamtolea mafungu tuyapeleke huko wapate kulipwa.

Lakini suala zima kwenye Chuo cha Mafunzo. Mhe. Naibu Spika, kule Chuo cha Mafunzo kuna wanafunzi wanalazwa mana wako kule ndio kama nyumbani wanapata mafunzo, kwa sababu sisi hatuna wafungwa tuna wanafunzi ndio maana tunaita Vyuo vya Mafunzo hatuiti Magereza. Kwa hivyo, mimi nilikuwa nina wazo kidogo hasa kuhusu suala la malazi, tuliwahi kutembelea sisi pale lakini ile hali ya wanafunzi wanavyolala magodoro yale amekwisha kabisa, tukajaribu kuuliza ule uongozi pale wa Chuo cha Mafunzo wakasema kweli hili ni tatizo. Kwa sababu

sisi tunanunua magodoro kila mwaka na magodoro haya tunayaweka chini. Kwa hivyo, saruji hii na haya magodoro hayachukui muda yanamalizika, matokeo yake kama bajeti haijafika pale wanafunzi wale wanalala chini wanatandika shuka tu.

Mimi nafikiri Mhe. Naibu Spika, ningeiomba serikali ikaangalia uwezekano wa kununua vitanda badala ya godoro. Kwa sababu bora kitanda kitapokuwa hakina godoro akitandika shuka atalala vizuri, kwa sababu wale pale ni wanafunzi tu wanajifunza tabia njema walifanya tabia ya uasi basi wanajifunza tabia njema. Kwa hivyo, tusiwape adhabu ya kulala kwenye saruji inawaathiri afya zao.

Lakini vile vile serikali inakula hasara zaidi kila mwaka ina maana iwe na bajeti ya kununua magodoro mapya, lakini ikinunua kitanda leo kinaweza kikakaa miaka mitatu, mine, mitano mpaka kumi hujanunua kitanda chengine. Sasa mimi nafikiri kuwe kuna bajeti maalum ya kununua vitanda kwa ajili ya wanfaunzi wale.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye tatizo la hatimiliki. Tatizo hili Mhe. Naibu Spika, ni kubwa na ukubwa wake unasababishwa, maana yake linatengenezwa liwe kubwa na zito kweli kweli kwa sababu tu ya maslahi. Nasema hivyo kwa makusudi Mhe. Naibu Spika, kwa sababu watu ambao wanakwenda kutafuta hatimiliki hawachukui muda hatimiliki zile hupatikana watu binafsi.

Lakini taasisi za serikali kupata hatimiliki Wizara ya Ardhi kishindo chake kikubwa kweli, ziko taasisi ambazo zishaomba zaidi ya miaka mitatu mpaka mine hazijapatiwa. Sasa hebu tujiulize Mhe. Naibu Spika, kuna nini? Ziko taasisi zinaomba kabisa na hazijapatiuwa na ziko taasisi haziombi wala hazina utaratibu huo kwa sababu tu ya maslahi, ndio yale aliyoyasema Mhe. Abdalla Juma hapa mana unapokuwa huna hatimiliki kesho na keshokutwa anatokea mtu anasema hapa pangu anatengeneza hatimiliki panakuwa pake kweli kwa sababu serikali haina hatimiliki.

Hili tatizo limeshajitokea sana, viko viwanja vingi humu vya serikali sasa hivi vishahodhiwa tena watu wana hati kabisa na vilikuwa vya serikali. Wanazo hati lakini utafanye serikali inabakia kimya, kwa sababu mtapokwenda Mahkamani ukimgusa anakwambia twende Mahkamani yule, mkienda utashindwa wewe ya kwako iko wapi wewe unasema tu hapa pangu manaake niliparithi tangu siku hizo, lakini yule yeye anaonesha hati. Sasa mimi ningeiomba sana serikali kuangalia utaratibu wa utoaji hatimiliki kwa maeneo ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie hapo kwa kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Mkwajuni ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu, mimi, wewe na wajumbe wote kusimama hapoa kufanya shughuli ambayo imetuleta hapa ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na kulinda maslahi yao.

Nikushukuru pia na wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia hoja hii ya Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nianze mchango wangu kwa kupendekeza kwamba Baraza lako tufanye marekebisho ya kanuni zetu na utifute Kanuni ya 106(g) na Kanuni ya 118. Mhe. Naibu Spika, Kanuni ya 106 (g) inaorodhesha zile Kamati za Baraza la Wawakilishi na (g) ni ya Kamati ya *PAC.* Kanuni ya 118 ndio inazungumzia kuwepo kwa Kamati ya *PAC* na majukumu yake. Mimi Mhe. Naibu Spika, niwaombe Wajumbe wenzangu baadae tufanye utaratibu tulete mapendekezo tuzifute kanuni hizi mbili.

Kwa nini nasema hivyo Mhe. Naibu Spika, sioni sababu ya kwenda kuwasumbua kina Mhe. Omar Ali Shehe na kamati yake na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Abdalla Juma wakenda wakafanya kazi nzito wakaja na ripoti kama hii halafu serikali ikenda ikaitia kapuni sioni sababu yake, kuliko hata iliyozungumzwa fedha za walipa kodi pengine wanaweza kufanya kazi kwa wiki ngapi hao, lakini ile nguvu waliyotumia kufanya kazi ile halafu serikali ikaja hapa ikatekeleza sera ya *business is usually*.

Mhe. Naibu Spika, *PAC* katika mfumo wa Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola ni chombo kizito sana na ndio maana katika Kanuni za maulimbile katika Mabunge yote ya Jumuiya ya Madola ikiwa huna mfumo kama wetu wa Serikali yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa ambayo hakuna serikali inayo upinzani, katika Mabunge ya kawaida ambayo kuna serikali ya upinzani ni lazima katika kanuni ya maumbile ni lazima kwama *PAC* iongozwe na Mjumbe kutoka chama cha upinzani. Mantiki yake nini Mhe. Naibu Spika, mantiki yake ni kuichunga serikali, kwa hivyo huwezi kuwa na Mjumbe kutoka upande wa serikali akaichunga serikali katika hali ya kawaida.

Lakini katika hali yetu anaweza kutoka popote, lakini kwa kutambua njama ile bado katika vyama viwili vinavyounda serikali imeonekana kwamba kiongozi wake atoke kwenye Chama kile ambacho ni cha upinzani ili kuichunga serikali kwa sababu bado Rais anatoka katika chama ambacho ni *Majority* katika serikali.

Mhe. Naibu Spika, yamewekwa haya ili kuhakikisha unatunza fedha za walipa kodi. Kwa sababu hata dhana yenyewe ya kuwepo Bunge katika dunia ililetwa kwa kutambua haja ya kuibana serikali katika matumizi. Walioibua dhana ya Bunge Uingereza msingi wake wale *Ma-liberal* waliokuwa matajiri, waliokuwa na viwanda, walimwambia hatuwezi kumlipa kodi mfalme ikiwa sisi hatuna kauli katika uendeshaji wa serikali na matumizi ya fedha ambazo zinaichangia serikali, ndio msingi wa kuja msemo kwamba, "*no taxasion without representation"*, kwamba hatuwezi kulipa kodi ikiwa hakuna uwakilishi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, Bunge na dhana yake limeendelea kuundwa upya na mpaka kuunda taasisi kama hizi ili kulinda ile dhana ya kulinda fedha za walipa kodi.

Mhe. Naibu Spika, ili tuendelee ni lazima tuchunge fedha zetu na uchungaji wa fedha una namna mbili, udhibiti mapato lakini pia uchunge matumizi. Inawezekana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo akafanya kazi kubwa sana katika kuongeza mapato katika serikali na taasisi ambazo zinamsaidia, lakini kama hatuchungi matumizi yatakuwa ndio yale yale kama vile unatia maji kwenye pakacha hayakai.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi wala sitoshughulika kuingia katika kifungu kimoja kimoja humu mana sioni faida yake, lakini mimi naomba ninukuu sehemu ndogo tu ya ripoti hii tena mwanzo kabisa ukurasa wa mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya *PAC* inatwambia, "kibaya zaidi Kamati imegundua kuwepo kwa ubadhirifu wa fedha za serikali na ubadhirifu na ufujaji wa mali za taasisi hizo huku sheria ya fedha na kanuni zake za mwaka 2005 pamoja na sheria ya manunuzi na ugavi wa mali za serikali na kanuni zake zinaendelea kuvunjwa. Hali hii inasikitisha sana kamati ambayo kwa muda mrefu sasa inaendelea kusisitiza haja ya kufuatwa kwa sheria hizo ipasavyo". Hili liko mwanzo kabisa wametuwekea Kamati ya *PAC*.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na *observation* hiyo hatuoni serikali ikijali, mbali ya Ripoti ya *PAC* zimeshaundwa Kamati Teule nne katika Baraza hili zikaleta ripoti zake humu ndani. *PAC* tangu imeingia serikali hii ni ripoti yake ya tatu hii. Mhe. Naibu Spika, tukijitizama tunafanya nini ndio nikasema tuvifute hivi vifungu, tukitaka kupima sera za serikali Mheshimiwa tutizame hii, iko wapi serikali. lakini utizame kule juu Mhe. Naibu Spika, kasema Mhe. Mbarouk Wadi kutupu kabisa, inaonesha dharau ya hali ya juu kabisa serikali na watendaji wake kwa chombo

hiki, haiwezekani mnajadili ripoti muhimu kama ya kamati hii ya kuchunguza hesabu za serikali halafu serikali watendaji hawaonekani.

Mhe. Naibu Spika, ndio nikawa najiuliza kwa kutumia lugha ya Mhe. Rashid Seif Suleiman *are we serious?* Kweli tuko makini? Mhe. Naibu Spika, nilikuwa najiuliza mimi hivyo kweli tukishafanya hivi mimi napata wasiwasi kwa mkabala huu wa serikali *attitude* hii kwamba kweli baada ya hapo zikachukuliwa kwenda kufanhiwa kazi ripoti hizi, mimi napata wasi wasi sana Mhe. Naibu Spika. Najiuliza hivi Mhe. Rais anazipata anazipitia ripoti hizi? Lakini kama anazipitia anazifanyia kazi?

Mhe. Naibu Spika, Katiba yetu kifungu cha 112(5) inazungumzia juu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu sa Serikali kupeleka ripoti yake kwa Rais na Rais baadae ndio kuagiza ripoti ile ipelekwe Baraza la Wawakilishi halafu *PAC* ndio wanfanya kazi yao. Na ile niseme ikiwa Rais hakuleta kwa sababu ya umuhimu wake basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anaweza kumpelekea Spika au Naibu Spika akaleta Baraza la Wawakilishi uzito wa ripoti ile Mhe. Naibu Spika. Lakini sasa uzito huo usiishie hapo tu, tuone utekelezaji wa yale yanayojadiliwa humu ndani.

Sasa leo Mhe. Naibu Spika, najiuliza ripoti zinajadiliwa? Watendaji hatuwaoni juu. Mhe. Naibu Spika, kasema Mhe. Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi katika Baraza hili, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni kwamba, haya mambo pengine wala si makosa ya mawaziri, lakini sasa nasema hawa mawaziri ndio wanaowasimamia watendaji. Sasa hata ile kuhakikisha kwamba wanakuwepo kusikiliza jinsi Wawakilishi wa wananchi wanavyochambua watendaji wao wanashindwa kuwepo hapa.

Mhe. Naibu Spika, Katiba yetu kifungu cha 50(1) kinasema kwamba,

> “Pale Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais au Waziri yeyote mwengine anapokuwa na dhamana ya Wizara yoyote ya Serikali, atakuwa ndiye kiongozi na Msimamizi Mkuu na bila ya kuathiri masharti yoyote ya usimamizi, Katibu Mkuu ambaye ofisi yake itakuwa ni ya utumishi wa Serikali atakuwa ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa Wizara”.

Jukumu la kuwa kiongozi na msimamizi mkuu amepewa Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili anapokuwa anaongoza wizara na Mawaziri. Sasa wanatwambia baadhi ya wengine kwamba huko katika mawizara hata kushirikishwa, hata kujua, hata ile kukaribia wakubwa wanapopanga mambo yao huwa hawatakiwi wawepo. Sasa mimi najiuliza kile kiungo baina ya yule ambaye anakuja hapa Wawakilishi

wa wananchi kuja kuomba fedha kwa niaba ya wizara ambaye baadae ndio tunakuja msulubu sisi humu ndani juu ya matumizi yanapokwenda vibaya, sasa yeye basi hata asiwe na kauli.

Mimi sidhani kwamba tunakuja tu, kwa sababu Katiba imesema kwamba yeye ndiye kiongozi na msumamizi mkuu. Na mimi nakiri nadhani Mheshimiwa na mawaziri wetu tunao katika Baraza hili, wasikubali kwamba wao hawahusiki, kwa Afisa Mtendaji Mkuu ni mbali na kuwa kiongozi na msaidizi mkuu ni vitu viwili tofauti. Maneno yaliyotumika mazito na madhubuti sana matokeo ndio haya Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, jeuri, kibri, dharau, inda ya watendaji wa serikali haiishii kwa muajiri hata chombo hiki. Chombo hiki cha kikatiba wanafika kusema huko aa, waache wapige kelele si kazi yao kupiga kelele tu, wanasema tena mengine yanasemwa katika koridoo zako Mhe. Naibu Spika, hapo nje ata si mbali, aa waache wapige kelele tu wale, matokeo yake tunakidharaulisha chommbo hiki na ndio maana Mhe. Hamza Hassan alisema nadhani jana kwamba palifanywa kipindi katika redio kuulizwa wananchji watoe maoni yao juu ya mjadala unaendelea Baraza la Wawakilishi, wakafika kututukana yale ni matusi Mhe. Naibu Spika, dharau ya mwisho ya wananchi tunaowaongoza kusema aa, ni Baraza la *Comedy*.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ikiwa wenzangu watakubali wao kuwa *comedian* shauri yao mimi wa Mji Mkongwe sitakubali kuona kuwa watu wa Mji Mkongwe walisimama kunipigia kura nikaja nikawa *comedian* katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, tunajua kuna watu walidhani kwamba wataling'oa meno Baraza hili, na kati kati hapa mwaka jana mpaka mwaka huu palipitishwa mambo makusudi kuparaganya ule mshikamano uliokuwemo ndani ya Baraza la Wawakilishi humu ndani. Kwa sababu ilionekana kwamba, mshikamano na *back bencher*s utapelekea madudu mengi kuibuliwa katika serikali hii na kuhakikisha kwamba tunazilinda fedha za walipa kodi ambao wanahangaika usiku na mchana wakachuma serikali ikakata kodi nakuendesha mambo yanayohusu wao kwa ujumla wao.

Mhe. Naibu Spika, Baraza hili likiamua linaweza na lina meno, katika Wajumbe 81 wa Baraza hili serikali ina wajumbe 29 tu humu ndani ndio faida ya ule mfumo aliosema Mhe. Salmin Awadh, kwamba tumetoka katika zama zile za kuwa upande mmoja kulikuwa kuna upande wa serikali likiwa baya likiwa zuri mawaziri na *back bencher* watatetea tu, na upande wa pili kulikuwa kuna upinzani na mawaziri

vivuli wao likiwa baya likiwa zuri watapinga tu, tushatoka kule. Sasa hata kanuni zetu zinatambua kuna mawaziri na kuna *back benchers*.

Nguvu hii Mhe. Naibu Spika, mimi nawaomba wenzangu wala siiambii serikali katika hili, hebu tuamueni, ile heshima ambayo chombo hiki ilipata baada ya uchaguzi na mwaka mzima wa 2011 tuirejesheni wananchi waheshimu chombo hiki na itakuja ikiwa kama alivyosema Mhe. Hija Hassan, itakuja hapa tukionesha mfano tukang'oa angalau waziri mmoja kutoka *CUF* na waziri mmoja kutoka CCM, tukaonesha mfano. Nimesema mapema kwamba mawaziri pengine na wao hawahusiki, lakini ile ya kutokubali kutekeleza wajibu wao katika kifungu kwamba wanawasimamia watendaji wao ndio viongozi na wasimamizi wakuu.

Mhe. Naibu Spika, niliwahi kusema tusidanganye kwamba haiwezi kutokea dunia inabadilika kwa kasi, kwamba pengine hatuna uwezo wa kumchukulia hatua waziri mmoja mmoja kama Baraza, lakini tumepewa meno na katiba hii. Kifungu cha 41 kiazungumzia hoja ya kura ya kutokuwa na imani kwa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili, tukifanya hivi ndio nikasema hebu tutumie meno tuliopewa, tukifanya hivi serikali itabidi iondoke iundwe mpya labda itakuwa fundisho kwa wengine, na sio kwa maana ya mawaziri tu, kwa sababu mawaziri pengine hata hawahusiki hawa, lakini iundwe upya mpaka huko chini kwenye uoza uliokuwa umejaa huko.

Mhe. Naibu Spika, nimesema sitaki kuingia jambo moja moja makusudi kwa sababu naona ni kupoteza muda tu, nikazungumze sijui KMKM na miradi yao ya ujenzi na fedha ambazo tunajua kwamba zimeundiwa mtandao baina yao na watendaji katika Idara ya Mhasibu Mkuu na watendaji katika Ofisi ya Rais yanajulikana Mhe. Naibu Spika haya, kwa nini tuingie huko. Au tukazungumzie kutola kwa *Fixed Asset Register* sijui tukazungumzie nini, tunazungumza kila siku haya.

Mhe. Naibu Spika, leo nasema na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wenzangu tujue nguvu zetu. Mhe. Naibu Spika, hiki ni chombo kikubwa sana hii Katiba, hii ni silaha nzito na mara nyingi tunakuwa wepesi wa kuvisoma vifungu vilivyokuwemo ndani ya katiba, lakini katiba hasa Mhe. Naibu Spika, dhamira ya walioiweka na katiba inawekwa na wananchi inaelezwa na wenye katiba katika utangulizi.

Waingereza wanasema, wananchi ndio *Sponsors of The Constitution*, ndio wadhamini wa katiba. Wadhamini wa Katiba ya Zanzibar wanasema nini katika utangulizi wa katiba, nini malengo yetu kama nchi, kama taasisi za nchi, ikiwemo

serikali, likiwemo Baraza la Wawakilishi, ikiwemo Mahkama na vyombo vyengine vyote vya nchi.

Mimi naisoma, “Na kwa kuwa sisi Wananchi wa Zanzibar tumeamua rasmi na kwa dhati tujenge katika nchi yetu jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na amani na kwa kuwa misingi hiyo yaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia ambayo serikali yake husimamiwa na Baraza la Wawakilishi, ambayo serikali yake husimamiwa na Baraza la Wawakilishi, ambayo serikali yake husimamiwa na Baraza la Wawakilishi!!! Lenye Wajumbe waliochaguliwa na linalowakilisha wananchi na pia yenye Mahkama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo wowote na hivyo kuhakikisha kwamba haki zote za binadamu zinadumishwa na kulindwa na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa ukamilifu”. Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Naibu Spika, katiba hii vile vile katika sehemu inayozungumzia malengo na maamuru muhimu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sura ya Pili kifungu cha 10 Mhe. Naibu Spika, inasema kwamba,

> “Kwa madhumuni ya kuendeleza umoja na maendeleo ya watu na ustawi wa jamii katika nchi, itakuwa ni wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.10 (b) Kuondosha kabisa vitendo vya rushwa na utumiaji mbaya wa cheo dhidi ya umma kwa wale wote walio na madaraka”. Lakini la muhimu Mhe. Naibu Spika, 10(h) “Vyeo vyote vya madaraka ni dhamana na vipo kwa faida na manufaa ya umma na wale wote walio na madaraka watawajibika ama moja kwa moja kwa umma au kupitia kwa vyombo vya uwakilishi”.

Mhe. Naibu Spika, chombo kikuu cha uwakilishi katika nchi ni Baraza la Wawakilishi. Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi niseme, sisi tushasema sana, nimewaambia Wawakilishi wenzangu tufanyeni maamuzi, hii na iliyopita hizi ziwe nondo wakati wa bajeti hapa. Kuna sura nzima ndani ya Katiba hii Mhe. Naibu Spika, inazungumzia masharti ya fedha yahusuyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo anafahamu kwamba chombo hiki ndicho kilichopewa dhamana ya kumuidhinishia yeye fedha halafu yeye akenda akasimamia matumizi yake. Kwa hivyo nasema tujipange, hapana kuidhinisha matumizi mapya ya fedha nyengine ikiwa hakuna maelezo ya fedha hizi za mwaka jana, najua mwaka jana palikuja maneno mengi sana kwamba, kwa mujibu wa katiba msipopitisha Baraza litavunjwa.

Mwanasiasa mmoja wa Zanzibar aliwahi kusema hapa, ‘ukiujua huu, huu huwiji’. Sasa Mhe. Naibu Spika, sawa bajeti yake kubwa tutampitishia Mhe. Waziri wa Fedha, lakini kuna bajeti za wizara moja moja hapa tunao wakati huo.

Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Rais, namalizia namwambia Mhe. Rais, namuomba sana, Mhe. Hija kanukuu hotuba yake alipokuwa analizindua Baraza hili na jinsi alivyosisitiza kwamba msingi wa serikali yake itakuwa ni uwajibikaji leo nasikitika sana kusema kwamba serikali yake inapwaya, inapwaya ndani ya Baraza la Wawakilishi, inapwaya mbele ya macho ya umma.

Mhe. Naibu Spika, tusijidanganye kwamba yaliyotokezea katika nchi za wenzetu kuwa hayawezi kutokea Zanzibar. Dunia inavyokwenda hivi sasa kunazungumzwa dhana ya nguvu ya umma, hakuna mtu aliyefikiria kama watu waliokuwa wakidhaniwa wameridhika wakishapata tende na kahawa wameridhika jamaa zangu wa Mashariki ya Kati, leo kunatetemka kwa sababu watu wamechoka kuendeshwa ovyo ovyo.

Mhe. Naibu Spika, nimevisoma vifungu vingi sana vya katiba ili kukumbushana tu, sisi tutamaliza wajibu wetu kuyajadili leo mpira uko kwa serikali. sisi tumechoka Mhe. Naibu Spika, kasema Mhe. Salmin Awadh na mimi narejea. Tumechoka huko nje tunapotoka tukaambiwa si mshapiga kelele ndo itakuwa nini? Sasa tunamuomba Mhe. Rais asije akalifikisha Baraza hili likaja likatekeleza nguvu yake ya kifungu cha 41 cha Katiba hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mwisho wa yote tutarudi kwa wananchi, nambwambia atazame sana Mhe. Rais serikali yake unapokuwa na mawaziri ambao anazungumza ndani ya Baraza la Wawakilishi na inaingia katika rekodi za *hansard* kwamba kwake yeye dhana nzima ya uwaziri ni kutafuta rizki ni hatari, manaake anakujibu kabisa kwamba kama rizki na wewe utapata, nilitaka kumwambia kwamba mimi nimeonesha mfano Wapemba nilitaka kufanya kazi hii ya kutumikia wananchi nikakataa uwaziri, nilisema katika kikao cha Mhe. Rais na leo naseama ndani ya Baraza nikarikodiwe *hansard* kabisa nitetee wananchi.

Lakini ninachozungumza kwamba lile jibu lake kuwa yeye dhana nzima ya mawaziri wa Serikali ya Dkt. Shein kumbe uwaziri ni kutafuta rizki na kama kutafuta rizki ndio maana zinatafutwa kwa njia za halali na njia zisizokuwa za halali ilimradi rizki ipatikane tu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, sisi tunamaliza kazi yetu leo kwa ripoti hii, lakini mpira uko kwa serikali, mpira uko kwa Rais. Kwa sababu mwisho wa siku namalizia, mwisho wa siku katika katiba hii nafasi zote za utumishi katika nchi ni nafasi za Rais mwenyewe, ipo wazi wazi Mhe. Spika, kifungu cha 51 Mhe. Spika.

Madaraka ya Serikali ya Zanzibar yatakuwa ni mikononi mwa Rais na kwa mujibu wa Katiba hii, anaweza akatekeleza yeye moja kwa moja au kuwapa viongozi waliopo chini yake kutekeleza madaraka hayo. Ifahamike kwamba masharti yaliopo katika kifungu hiki hayazuii sheria kukabidhi madaraka kutekeleza kazi kwa chombo chochote cha umma au mtu mwengine yeyote ambaye si Rais wa Zanzibar lakini madaraka ni yake.

Hawa wote anaowateuwa katika mawaziri, makatibu wakuu, wakurugenzi, mameneja wanafanya kazi kwa niaba yake. Sasa Mhe. Naibu Spika, nadhani madhali yeye ndiye anayewaweka anayo nafasi ya kuwajibisha. Kinyume chake Mhe. Naibu Spika, nimesema kule kwetu Makunduchi kuna ngoma inaitwa Kipwapwe. Waliokuwa wakitizama televisheni miaka ya thamanini ilikuwa ikioneshwa, basi nyimbo yake huwa wanaanzia mule, *"Tuonane mkwaju ngoma tuonane*" na mkwaju ngoma wetu Mhe. Naibu Spika, Juni/Julai tukijaaliwa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naiunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia na nasema tena kwamba tusipoona hatua zikichukuliwa, sisi tutajikosha ndani ya nchi na niwaambie wawakilishi wenzangu tena kwamba sote tutarudi kwa wananchi uwajibikaji wetu ndio utapimwa humo wakati wa Juni/Julai.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi jioni hii kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti hii ya *PAC*. Pia nimshukuru Mwenyekiti wangu wa *PAC* kwa kuwasilisha ripoti hii kwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kumshukuru *CAG* pamoja na Wizara ya Fedha kwa kuiwezesha kamati yangu kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na kufikia leo kuwasilisha ripoti yetu hii. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hii mimi ni kamati yangu, kwa leo mimi nisingekuwa na mengi kwa sababu kamati tumeshawasilisha ripoti hii ambayo wajumbe wameshaichangia na ufanisi wa ripoti hii, kwa kweli umeletwa pamoja na makatibu wetu ambao tumefanya kazi hii ngumu kwa muda ambao ni mrefu sana na tulikuwa tunachukua wakati mkubwa kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti wa kamati asubuhi, tulikuwa hatujali masaa, tulikuwa tunafanya kazi kwa ufanisi kwa kuileta ripoti hii mbele ya Baraza letu tukufu.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kamati hii yenye majukumu ya kuisimamia serikali kwa kupitia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iweze kufanya matumizi ya zile fedha ambazo tunazipitisha hapa kwa kutumia sheria ya manunuzi na vile vile sheria ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, nikianza na ripoti hii ambayo ina mambo mengi lakini kwa kuwa ripoti imeshasema, mimi itakuwa kazi yangu ni kutoa athari ambazo zinajitokeza katika kutokufuata sheria za fedha pamoja na sheria za manunuzi.

Kwanza nianze na kutokuwepo na udhibiti na utunzaji wa mali. Bila ya kutokuwepo udhibiti na utunzaji wa mali, kwa kweli serikali yetu itakuwa na hasara kubwa kwa sababu Waswahili wamesema "Ukitunze ili kudumu". Katika kupita kwenye kazi zetu hizi kwenye mashirika na maeneo mbali mbali kama kamati ilivyosema tumekuta kwamba hakuna udhibiti na utunzaji wa mali za serikali. Hili ni tatizo na kwa sababu serikali inataka ifanikiwe basi ni lazima ripoti hii iifanyie kazi kwa kuona kwamba sasa utunzaji wa mali zetu na udhibiti unafuatwa.

Vile vile athari nyengine ambayo itatokana na kutokuwa na daftari la kutunza mali. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, *mali bila ya daftari hughibu bila ya habari*. Kwa hivyo niseme kwamba kutokuwepo kwa daftari vile vile ni tatizo na inaweza ikai-*cost* serikali yetu mambo mengi na kutokujua mali zake hasa.

Vile vile kwa sababu sisi binadamu tuna mambo mengi na kuna watu wa aina mbali mbali, bila ya kuwa na daftari na daftari lenyewe liwe lenye kukamilika, tunakuta madaftari, kwa vile kwa sababu Kamati ya *PAC* tunakwenda likaekwa pale lile la kusema na kama walivyosema wajumbe wenzangu kuna comedy. Kwa hivyo hapa linakuwepo daftari lakini la kufanya ule mchezo wa kuigiza.

Lazima lile daftari likamilike, liwe na *value*, *cost* ya kile kitu chenyewe. Hili ndio litakuwa limekamilika. Tunajua kulikuwa na tatizo lakini serikali ninafikiri kupitia Wizara ya Fedha imeshaandaa hii format na kuna wizara ambazo zimeanza. Mimi nishukuru serikali kwa kuona kwamba kulikuwa na haja ya kulifanyia kazi hili suala.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, ni lazima taasisi zetu ziwe na mpango kazi, bila ya kuwa na mpango kazi athari yake ni kupangilia ule utaratibu hasa wa manunuzi, bila ya kuwa na mpango kazi basi vile vile mapungufu haya ya mpango wa manunuzi na hii husababisha pale unapotaka kufunga mahesabu, kwa sababu

ulikuwa huna mpango kazi wako na hili tumeliona *physically* kwamba fedha ikifikia muda wa kufunga mahesabu mwezi wa Juni ndio fedha zile zinatiwa na matumizi yake yanayofanyika pale.

Kwa kweli yanakuwa hayafuati ule mpango wa manunuzi, kama ni mikataba inajazwa tu na hii inapelekea zile *goods* ambazo tumezitaka pale hatupati ambazo tumezikusudia. Vile vile na kwa sababu kutakuwa hakuna mkataba mikataba yenyewe haijakamilika, basi pia hapa inaweza ikatokeza athari ambayo ikailisha hasara serikali.

Mhe. Naibu Spika, suala la kutofunga mahesabu ni kweli mahesabu yanakosekana na kwa sababu ya makubaliano bado na hasa mashirika, kuna *list* ile ya *PBZ, ZSSF* na nyengine. Kwa kweli kama mimi ni mhasibu ni aibu kusema kwamba hawakufunga mahesabu, nimeona kama kulikuwa kuna mgongano kwamba serikali inafunga hesabu zake kutoka July to June.

Lakini sasa haya mashirika ni kwamba yanafunga mahesabu zao kupitia *January to December*. Ni kweli kwa sababu *CAG* anafuata *financial year July to June*, kwa kweli akifika pale mahesabu hayajafungwa na inaonekana na kwa mujibu wa sheria au katiba kwamba Mdhibiti na Mkaguzi wetu wa Hesabu ndio anayestahiki kuzikagua hizi hesabu, kwa hivyo anaona pale kuwa hazijafungwa lakini niseme kwamba sasa ni lazima kuwe na mabadiliko ya kwa haya mashirika yetu ya SMZ basi yaweze kubadilisha huu mtizamo na waanze sasa wakubaliane kwamba hesabu zifungwe kama anavyotaka *CAG* wetu.

Vile vile kuna suala la madeni Mhe. Naibu Spika, ni kweli madeni yanadhoofisha. Niseme deni ni kitu muhimu lazima tulipe madeni. Ingawaje ni serikali taasisi zote za serikali lakini madeni kama hayatolipwa basi tunadhoofisha ile taasisi nyengine. Na kama kuna madeni ambayo yanataka kufutwa basi ni lazima ile taarifa ifike hapa Barazani na tuweze kupitisha kwa sote, kwa sababu sisi ni Wawakilishi wa wananchi.

Ukaguzi wa ndani Mhe. Naibu Spika, una athari zake bila ya kutokuwepo na ukaguzi wa ndani, inaweza vile vile yakapita matumizi ambayo si ya haki, yaliyokuwa hayakutizamiwa. Kwa hivyo vile vile nishauri kwamba ni lazima ukaguzi wa ndani uwepo.

Vile vile kitengo cha manunuzi kiwepo katika taasisi zetu ili tuweze kuleta ufanisi katika mambo yetu. Ni lazima kuwe na *collaboration*, tuwe na mashirikiano ya pamoja bila ya kuwa na mashirikiano, kwa kweli tutakuwa na matatizo.

Ningeomba elimu kwa wahasibu na hasa wahasibu wa Halmashauri. Tumepita maeneo mbali mbali tukaona kwamba mahesabu yana matatizo kidogo, unakuta mtu hajui unamwambia nina *reconciliation* anakupa ule muhtasari wa kufunga mahesabu anakwambia *open balance, less revenue less expenditure* ndio anafanya *statement* yake.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, nikienda mbele kwenye miradi ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika 2.

Mhe. Fatma Said Mbarouk: Ahsante sana. Mhe. Naibu Spika, kuhusu miradi ya maendeleo kwa kweli kuna mitazamo tofauti baina ya wananchi na pale inapotokezea kwamba kuna mradi wa maendeleo, serikali inachangia au wananchi wanachangia lakini kunakuwa kidogo hitilafu kwa zile kamati zenyewe kutokufahamiana na haya tumeyaona.

Haya tumeyaona vile vile kwa upande wa wananchi ningetoa ushauri na kuwaambia kwamba ni lazima tuthamini ile miradi ambayo serikali inaileta kwa ajili yetu. Unakuta kama miradi ya *TASAF* mara nyingi tulivyokwenda tumeona kwamba miradi imeanzishwa lakini kuna migongano baina ya wenyeviti na makatibu wao kwamba hawana ushirikiano. Na niseme nitoe wito kwa wananchi sasa hivi kwamba tuondoshe zile itikadi ili ile miradi iweze kuendelea.

Hayo nimeyaona mwenyewe tulipokwenda physically katika maeneo mbali mbali, unakuta kwamba miradi ile na hasa tumekwenda Tundauwa tuliona kuwa mradi umekwisha wa soko lakini bado wananchi wenyewe wanavutana kwa sababu ya itikadi. Kwa hivyo vile vile ningetoa wito kwa wananchi kwamba sasa twendeni kwenye maendeleo, tuondoe zile itikadi hivi sasa ili kuileta ufanisi kwa zile fedha za umma zisipotee.

Kwa sababu unakuta jengo limeshakwisha lakini limekaa halina kazi yoyote. Tumekuta pale soko limekwisha lakini kuna migongano ya wenyewe kwa wenyewe wananchi bado hawajaweza kulifungua na ukitizama zile ni fedha za umma, na kwa sababu ni fedha za umma ni lazima tuzilinde kwa hali yoyote.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Amani.

Mhe. Naibu Spika: Sasa tunakwenda kwa Mhe. Mohammed Mbwana Hamad lakini michango mingi munarudia ile kwa ile.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kuwepo hapa katika hali ya afya njema. Lakini pia nachukua nafasi ya kukupongeza kunipa nafasi hii na mimi kuchangia angalau mawili matatu katika ripoti ya Kamati ya *PAC*, kamati ambayo inafanya kazi katika wizara zote za serikali na mashirika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo niseme kwamba jana Mhe. Spika alisisitiza sana kutokana na umuhimu wa watendaji wakiwemo mawaziri kuwepo katika kusikiliza ripoti hii muhimu ambayo inamgusa kila Waziri wa Nchi katika nchi hii ya Zanzibar, lakini pia inawagusa na watendaji wengine.
Tulifikiria leo kwamba ukumbi wa juu kama walivyosema wenzangu utajaa lakini masikitiko ni kwamba kuna watendaji wachache tu ambao wanatusikiliza katika ukumbi huu. Lakini pamoja na hayo tunasema kuwa wakati umefika wa kubadilika.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze mchango wangu kidogo kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Naibu Spika, ofisi hii ni muhimu sana kwa sababu ndio ofisi ambayo imepewa dhamana ya kuzikagua fedha zote za serikali zinazoingia katika mawizara na taasisi zetu za serikali.

Mhe. Naibu Spika, ofisi hii inahitaji kupewa watumishi ambao watakuwa na taaluma mbali mbali. Kwa mfano ofisi hii inahitaji kuwa na wahandisi, wachumi, wafamasia, wanasheria na wengine ili kuweza kufanya kazi zao vizuri kila kada inayohusika kufanya kazi. Kwa hivyo nimuomba Mhe. Waziri anayehusika na ofisi ile anapaswa ofisi ile kuiboresha ili kufanya kazi kwa ufanisi unaostahiki.

Mhe. Naibu Spika, nikianza na mchango wangu katika ripoti iliyosomwa na Mhe. Omar Ali Shehe ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, niende katika kukosekana kwa hati miliki katika majengo na maeneo mbali mbali ya serikali.

Mhe. Spika, kwa kweli inasikitisha sana kwamba mpaka leo kuna majengo na maeneo mbali mbali ya serikali yamekosa hati miliki. Nataka nitoe mfano wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ambayo kuna majengo kwa mfano jengo la *Karume House* halina hati miliki, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Pemba, Hoteli ya Bwawani haina hati miliki na majengo mengine.

Mhe. Naibu Spika, tumuombe Waziri wa Fedha ahakikishe inshaallah na mali za serikali vikiwemo viwanja vina hati miliki ili wahasibu wetu wanapoweka mahesabu yao yaweke mahesabu sahihi zikiwemo na mali za serikali, tusikae katika majumba ambayo hayana hati miliki au katika ofisi ambazo hazina hati miliki.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niende katika ripoti ya *PAC* kwenye ukurasa wa 8, kuhusu sura ya ukiukwaji wa taratibu za malipo na manunuzi. Mhe. Naibu Spika, ripoti ya Uchunguzi wa Hesabu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka 2010/2011 inaonesha kwamba malipo mbali mbali yalifanywa kwa kukiuka taratibu yalifikia jumla ya shilingi bilioni mbili, milioni mia tatu sabini na saba, laki tatu thamanini na tatu elfu mia tatu na thalathini na tano.

Mhe. Naibu Spika, huu ni ubadhirifu mkubwa. Sasa kutokana na ubadhirifu huu watendaji wanafanyakazi bila ya kujali miko na taratibu zao za kazi. Mhe. Naibu Spika, wahasibu wote wamefundishwa taratibu za kudhibiti mali, kuuza na kununua, kupokea lakini kwa kudharau tu na fedha zinakwenda ovyo.

Sasa nimwambie Mhe. Waziri wa Fedha kuna usemi unaosema, “Dawa ya jino ni kung’oa si vidonge”. Mhe. Naibu Spika, umefika wakati hivi sasa watendaji wote ambao wanafanya kazi zao kwa uzembe wawekwe pembeni, kwa nini nikasema wawekwe pembeni kwa sababu tuna vijana wetu wengi wamesoma wanatafuta ajira hivi sasa. Kuna vijana wamemaliza vyuo vikuu ndani na nje ya nchi hawana ajira, tunang’ang’ania vijana wanafanya kazi kwa mazoea.

Mhe. Naibu Spika, imefika wakati sasa tubadilike. Wananchi wetu wote walidhania kwamba Serikali ya Umoja ya Kitaifa italeta mabadiliko ya uchumi na hali za wananchi wetu zitatononoka. Lakini bado hali ya wananchi wetu ni duni, watu wanatafuta angalau milo miwili kwa siku inashindikana kwa sababu ya utendaji mbaya wa watendaji ambao wanafanya kazi kwa mazoea.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, yeye ndiye mwenye dhamana ya fedha za nchi hii, vitabu vyote vya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali hivi ukivisoma vina mambo mengi ya ubadhirifu wa mali na pesa za nchi yetu hii. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri wa Fedha kila atakapolikutia tatizo la fedha la ubadhirifu wa fedha katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alichukulie hatua. Vyenginevyo tutakuwa tunasomea maiti tunaondoka na ujaka wetu.

Mhe. Naibu Spika, imefika wakati angalau watendaji basi wapewe barua za onyo. Lakini tunasoma ripoti baadae basi tunaweka ripoti chini hakuna kinachoendelea. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hili aliangalie kwa kina watendaji wasifike wakati wakajenga kibri, wakajiona kwamba wao ndio wao, wajue kwamba kuna wenziwao tele wamesoma na kazi hiyo wanayoifanya wao basi wapo watendaji ambao wanaweza kuifanya kwa uzuri zaidi. Mhe. Naibu Spika, umefika wakati wa kubadilika ni lazima twende na mabadiliko yalivyo, tuache kufanya kazi kwa mawazo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 9 na 10 wa ripoti ya Mwenyekiti wa *PAC*. Ukurasa wa 10 unahusiana na ufungaji wa hesabu. Kwa kweli kuna taasisi nyingi hazifungi mahesabu. Ripoti inasema hapa kwamba uchunguzi wa kamati kwa hoja hii umebainika kwamba kuna baadhi ya wahasibu kutokuwa na uwezo wa kufunga hesabu.

Sasa hili ni tatizo, kuna taasisi hazifungi hesabu na wanapobidi kufunga hesabu wanatafuta wataalamu kutoka nje, yaani kutoka labda Tanzania Bara kuja kuwafungia hesabu hapa. Tunasema hivi kwamba tulitembelea Chuo cha Fedha pale Chwaka, wametueleza vizuri wana utaalamu mzuri sana wa ufungaji wa mahesabu. Kwa hivyo, kwa nini taasisi ambazo hazina uwezo wa kufunga mahesabu wasikitumie Chuo cha Chwaka na badala yake wakatafuta wataalamu upande mwengine. Upande huu nakusudia kwamba gharama za kuwalipa wale ni kubwa zaidi kuliko kuwalipa wale vijana wetu pale Chwaka.

Kwa hivyo kile chuo kinawafundisha wataalamu na wapo wataalamu wazuri ambao wana uwezo wa kufunga hesabu. Kwa hivyo, taasisi hizi zinapaswa kuwatumia vijana wetu ili na wao hawa ambao hawawezi kufunga hesabu wapate ule uelewa kupitia kwa wataalamu wetu hawa.

Mhe. Naibu Spika, kwa haraka haraka niende katika ukurasa wa 12 wa ripoti. Hii ni miradi ya *TASAF*. Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Waziri wa Fedha kwamba miradi ya *TASAF* kwa kiwango kikubwa inajengwa haifikii kiwango. Jengo la *TASAF* linajengwa kwa gharama kubwa lakini baada ya miaka miwili mitatu jengo lote limepasuka, linahitaji ukarabati wa gharama mpya. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri wa Fedha suala hili aliangalie kwa kina na wanapokwenda wataalamu basi lile jengo husika na taasisi husika ilisimamie jengo lile kwa umakini wa hali ya juu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kuna mengi ambayo labda tungeyazungumza lakini miongoni mwao yameshazungumzwa na wasemaji waliopita na ulisema kwamba

tusirudie, lakini kuna mambo lazima yarudiwe kutokana na umakini wake kama kuyatilia nguvu.

Niseme kwamba nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, taa yako naheshimu uliokwisha iwasha. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*).

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba Baraza lako tukufu liweke kanuni kando ya muda badala ya kumaliza kama kawaida yetu saa mbili kasorobo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tuliruhusu liendelee na shughuli zake na ili tumruhusu Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, ili kufanya majumuisho ya michango muhimu sana ambayo imetolewa na Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi, ili waweze kutoa ufafanuzi mzuri na halafu wananchi wasikie nini viongozi hawa wawili wamesema juu ya yale yaliyosemwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri kuhusu kuongeza muda wa Baraza wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka na mimi niungane na wenzangu kumpongeza sana Mwenyekiti wa *PAC* pamoja na wajumbe wako. Pia nataka na mimi niunge mkono taarifa hii ya Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli sijawahi kuyaona, leo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, ingawa baadhi yetu akiwemo Mwakilishi wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe, alithubutu kusema heshima ya Baraza inashuka, lakini mimi naona leo imepaa na wala haiwezi kushuka. Baraza letu litaendelea kuwa na heshima na

wananchi wetu wataliheshimu Baraza hili. Kwa sababu moja tu ile aliyoisoma Mhe. Ismail Jussa katika Katiba, kwamba Baraza ndilo linalosimamia serikali.

Kwa hivyo kwa upande wangu mimi Wajumbe waliochangia hoja iliyotolewa na Mwenyekiti walikuwa ni 9, akiwemo pamoja na Mwenyekiti mwenyewe. Lakini Mhe. Naibu Spika, hoja nilizozinukuu ni 87. Ninapata faraja kanuni 108(15) kinamtaka kila Waziri aje atoe taarifa ya utekelezaji kwa maagizo haya ya Kamati mwezi wa Machi. Isipokuwa *PAC* inamtaka Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aje atoe taarifa ya utekelezaji. Imenipa faraja sana kanuni ile na mimi Mhe. Naibu Spika, nasema nayaandaa haya yote kuja kuyatolea taarifa kwa ukamilifu, panapo uhai na majaaliwa mwezi wa Machi, 2014 kama kanuni inavyonitaka.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nisiwatoe raha Wajumbe wa Baraza lako tukufu, nitaomba zile hoja muhimu na za msingi na kwa kunusuru muda nizitolee basi ufafanuzi kidogo.

La kwanza Mhe. Mwenyekiti na baadhi ya Wajumbe walitamka wazi kwamba serikali yetu hii inafanya biashara na wafanyabiashara ambao hawalipi kodi. Nataka niseme kwamba zoezi hilo la kuwatambua hao wafanyabiashara wanaofanya biashara na serikali ambao hawalipi kodi, basi bodi yetu ya mapato imeanza kulifanyia kazi na tutakaowabaini watapaswa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria na taratibu zetu. Hilo zoezi na sisi tumeshaliona na tumeshaanza kulifanyia kazi.

Vile vile nataka niwaambie wenzangu Wajumbe wa Baraza lako tukufu wamesema sisi Mawaziri sio watendaji, lakini ni wasimamizi, tusimpe mfanyabiashara kazi asiyelipa kodi. Tuwaambie watendaji wetu kama huyo mfanyabiashara hana *tin* namba yake tukafuatilia na sisi tukaona kwamba ni mlipaji kodi mzuri, kwa nini tunampa biashara, tusimpe na sisi biashara basi. Kwa hivyo, hili nawaomba sana Mawaziri wenzangu tulisimamie.

Pia limezungumzwa suala la udhibiti wa risiti na matumizi holela ya risiti. Wazo lililotolewa mimi nakubaliana nalo kabisa. Nitazungumza na wenzangu wa *ZRB*, tuone basi ni kwa kiasi gani wafanyabiashara tuliowasajili watatengenezewa risiti zenye *tin* namba zao na wao watakwenda kuzinunua kule. Wazo ni zuri tu, kwa sababu ya kudhibiti zile risiti, risiti *fake* ndio tutaweza kuzidhibiti. Nitazungumza na wenzangu wa *ZRB* tuone urahisi wake, wepesi wake na uzito wake katika kulitekeleza suala hili.

Mhe. Naibu Spika, limezungumzwa suala zima hapa la ulipaji wa kodi kwa wajenzi wa majengo. Nataka niseme ndugu zetu hawa wanaojenga ni wengi mno, lakini ndio wengi ambao hawalipi kodi na hawalipi kodi kwa sababu hakuna chombo wala sheria ambayo inawaandaa wao kuweza kulipa kodi. Wazo lililotolewa la kuandaa utaratibu wa kuweka sheria na mimi naliwafiki. Kila penye pesa basi mimi nitaliafiki tuparekebishe ili pesa iweze kupatikana.

Mashirika ya Umma kutolipa kodi. Nataka niseme kwamba kwanza tulipoyaanzisha haya Mashirika ya Umma serikali imechukua. Nataka niunganishe na ile hoja ambayo Mhe. Mtando ndugu yangu pale alisema kuwa hatuko tayari serikali kuyasaidia mashirika. Kwa kweli tunayasaidia sana. Nataka niseme kwamba tulipoyaanzisha haya mashirika, tuliwaambia kwamba kila watakapotengeneza faida, wasilete gawio serikalini, wachukue lile gawio kama kujenga mtaji, tuliwaambia wajenge mtaji na wakafanya hivyo. Tukawaambia tena kuna baadhi ya kodi wasilipe ili wajenge mtaji, katika lengo la kuwasaidia.

Mhe. Naibu Spika, lakini lazima tukubali kuwa kuna mashirika mengine yameshindwa kufanya biashara na kuna mashirika mengine yamefanya biashara vizuri sana, *performance* zao ni nzuri na sasa hivi wameshaanza kutoa gawio kwa serikali. Wamelitaja Shirika la Bima. Shirika la Bima ni *one of the best.* Benki ya Watu wa Zanzibar, Shirika la Bandari nalo sio shirika baya, Shirika la Umeme nalo sio shirika baya kama litafanyiwa kazi ile mliyoitoa katika Kamati Teule, sio shirika baya. Kuna mashirika ambayo unaweza ukayaona hasa, kwamba haya yakifanyiwa kazi kidogo yanaweza yakasaidia bajeti ya serikali. Lengo letu ni kwamba haya mashirika yaweze kutoa gawio na kuna zile kodi ndogo ndogo basi waweze kulipia wenyewe ndipo watakapoweza kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu taasisi zinazojitegemea kuendelea kupata ruzuku. Jamani mimi nataka niseme kitu kimoja tu ndugu zangu, tunapitisha sheria hapa kwa taasisi, tunaunda taasisi sisi wenyewe hapa kisheria, lakini hatuziangalii zile taasisi tunazoziunda miundombinu yake. Unapokuja sasa kuunda taasisi haina miundombinu basi inabidi uipe ruzuku tu ili ijenge miundombinu, lakini tunapaswa kuziangalia mpaka muda gani utazijengea hiyo ruzuku. Ukiona miaka mingi inakwenda taasisi hizi bado hazijaweza kujenga miundombinu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niishauri serikali na mwenzangu hapa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo hapa ni Kiongozi wetu. Taasisi hizo tuzigeuze ziwe idara za kawaida tu, kwa sababu zinashindwa. Sasa lengo ni kwamba tunawapa ruzuku wajenge miundombinu halafu wajitegemee, waondoke kabisa kuwa ni tegemezi katika serikali. Lakini unaikuta taasisi miaka 20 au 25.

Mhe. Naibu Spika, mfano mzuri naweza kusema Chuo cha Chwaka. Chuo hiki kinafanya vizuri sana na katika muda mfupi kile Chuo kitakuwa hakitegemei tena ruzuku, kitafanya vizuri sana. Ni lazima niwape *credit* yao.

Suala jengine ambalo Mwenyekiti umelizungumzia sana ni kama tuta-*cover* kidogo basi tunaweza tukafika bilioni 30 mapato yetu kwa mwezi. Mimi nataka nikuambie kwamba muono wangu ni huo, na nikiangalia kodi ambayo tukiweza kuifanyia kazi vizuri sana VIP, basi tunaweza tukafika bilioni 30 kwa mwezi. Sasa hivi tunazungumzia bilioni 22 na tulipoingia hapa tulikuwa tunazungumzia bilioni 13 miaka minne na nusu tumefika bilioni 22. Lakini juhudi hizi mmoja wenu humu ndani alisema Waziri wa fedha peke yake hawezi, ni lazima tushirikiane sote jamii nzima ikerwe na watu ambao hawataki kulipa kodi. Sisi wengine hatukerwi, kama hulipi kodi hukerwi. Kwa hivyo, mimi nakubaliana nalo kabisa wazo la Kamati, tutalifanyia kazi tuone hali yetu itakwendaje.

Mhe. Naibu Spika, kuanzishwe miradi ambayo ina lengo la kuimarisha mfumo wa ulipaji kodi, uanzishwe mradi huo. Hili wazo ni zuri sana na tutajaribu kuliangalia kwamba tukianzisha mradi ambao una lengo la kuimarisha mfumo wa ulipaji kodi, basi utaweza kusaidia kupata kodi zaidi.

Taasisi za umma kukopa na kushindwa kulipa. Kifungu nambari 16(3) cha sheria ya fedha kinakataza, huwezi ukakopa bila idhini ya Waziri wa fedha. Wamekopa nyumba huko na wameshindwa kulipa, mataasisi yameshindwa kulipa. Hazina ikasema mwisho mwaka 2006 tunapiga mstari, deni la chini ya mwaka 2006 Hazina inabeba inalipa. Lakini hapo tena hakuna. Sasa kama taasisi itakopa halafu inashindwa kulipa huyo asimlilie mtu, atafute vyanzo vyake alipe mwenyewe, zaidi ni agizo lipo tayari. Sisi tumeingia awamu ya saba tumelikuta na tunalisimamia.

Mhe. Naibu Spika, juzi ndugu zetu wa uwanja wa ndege pale sehemu ya *fire* wanataka kukopa kwa ajili ya kuongeza magari ya Zimamoto walikuja kutuona, kwa sababu wanalielewa hili. Kwa hivyo, mimi nasema kifungu cha 16(3) cha sheria ya fedha kimesimama na kiko safi sana. Mchakato wa kufuta madeni umekwama.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimwambie somo yangu Mhe. Omar Ali Shehe kwamba hatujakwama, tunachokifanya hapa tunalipitia deni moja baada ya moja, mengine yale yanaweza yakalipwa.

Mhe. Naibu Spika, leo mchana nimezungumza na watendaji wangu, nadhani tuko karibu sana. Bahati nzuri Naibu Katibu Mkuu wangu, ameweza kuiona mpaka ile *text* niliyoiwasilisha mimi Bungeni ya kufuta madeni ya Muungano, kaiona. Kwa hivyo, jitihada tunaendelea nazo na nitawataka wenzangu hawa, nafikiri katika kipindi hiki tukimaliza Baraza hilo la bajeti, basi Baraza linalokuja tulete hilo azimio la kufuta hayo madeni ambayo hayawezi kulipika.

Mhe. Naibu Spika, ukiukwaji wa taratibu za malipo ya manunuzi. Ukikiuka taratibu za malipo ya manunuzi maana yake umekiuka sheria ya manunuzi na sheria ya manunuzi ina adhabu zake. Mimi nasema kwamba kila mmoja hii sheria anapaswa kuisimamia, kila Wizara na kila taasisi kuna *procurement unit*, kile kitengo ndio kinapaswa kuzisimamia hizo taratibu.

Mimi nasema kwamba mwaka jana nilizungumza na Wahasibu wote, nikawaambia kwamba hesabu inayokuja nitaifuata wizara moja moja, nikiona kwamba kuna taasisi ambayo imefanya upotevu mkubwa zaidi, basi nitawataka wajieleze na nitafanya hivyo, wajieleze tu kwa nini wamefanya hivyo na wakati tumeshazungumza. Bilioni 2, imeelezwa hapa katika ripoti.

Udhaifu wa Udhibiti wa Mkaguzi wa ndani. Nataka niseme kwamba Mhe. Naibu Spika, suala hili tunaliangalia kwa kina sisi, kama ni sawa kwa wakati huu kuwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa ndani, tunaliangalia kwa kina na tutalifanyia kazi. Tutashirikiana na Mwanasheria Mkuu ili kuweza kuona tutafanya nini.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Wahasibu na maafisa manunuzi tuwaajiri na wawe na sifa. Nataka niseme Mhe. Nabu Spika, hivi sasa ndani ya serikali tuna upungufu wa wahasibu 100. Imezungumzwa sana kwamba Pemba wamewakuta hawana sifa Wahasibu na kadhalika. Tuna upungufu wa Wahasibu wenye sifa 100 na sifa inaanzia diploma na tumeomba utumishi tupate angalau nafasi basi tuajiri. Mwaka 2012/13 tumepewa nafasi 10 tu. Sio kuwa hatuyaoni haya tunayaona. Lakini na yeye kwa mujibu wa bajeti yake aliyowekewa, akinipa mimi 100 maana yake hana kitu kanipa 10 tu. Lakini wazo lililotolewa kwamba kuwafunza hawa vijana maafisa manunuzi. Ni wazo zuri, tutaendelea kuwafunza.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba tulipofanya tathmini baada ya ile miaka 10 ya *vision*, tukabaini kwamba tuna mapungufu sana katika utaalamu wa Uhasibu na *procurement officers*. Kada tulizobaini tuna mapungufu nchini tumebaini hizo na sasa hivi tunawa-*train* wengi zaidi ili waje kutusaidia zaidi.

Mapato ya vikosi yanapaswa kuingizwa kama ni mapato ya serikali. Mimi nakubaliana naye mia kwa mia. Hili kwa sababu Mhe. Waziri mwenzangu ni kamati yangu na tuko karibu sana, tutalisimamia kwa pamoja. Wao wanapofanya kazi wanapopata mapato, wanatakiwa kuingiza kama ni mapato ya kuanzia shughuli zao za mwaka, kama hawafanyi hivyo basi watakuwa wanafanya makosa. Tutazungumza na viongozi wa vikosi na tutazungumza na Wahasibu ili suala hili tulitekeleze kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa kukagua hesabu za mashirika ya umma haupaswi kwenda tofauti na Katiba. Katiba yetu ya Zanzibar, kifungu cha 112(3) (c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Shughuli za Serikali ndiye aliyepewa mamlaka ya kukagua taasisi yoyote ya serikali. Sasa kama mashirika yana sheria zao, sheria haiwezi kuwa juu ya Katiba. Mimi mwanzo sikujua kama tatizo ni kubwa kiasi hiki.

Utakumbuka Mhe. Omar Ali Shehe Mwenyekiti wa *PAC*. Mwaka jana ulipokuja na taarifa basi alitoa taarifa ya hizi taasisi tatu, Bima, *ZSSF* na *PBZ*. Nikaziita mimi hizi, nikamuita na *CAG* tukafanya kikao cha pamoja, tukaja na *conclusion* nzuri sana. Sasa hivi nadhani ile *conclusion* itafuatwa kwa taasisi hizi pamoja na *CAG*. Kumbe tatizo ni kubwa, taasisi 12.

Mhe. Naibu Spika, taasisi hizi nitaziita zote, ili tuje tuelewane na tufahamishane, kila mmoja atabeba jukumu lake kama hawasilishi ripoti kwa *CAG*. Nitawaomba waandike kwa maandishi wampelekee *CAG* kuahidi kwamba watapeleka hizo hesabu zao na nakala wailete kwenye ofisi yangu.

Chuo cha Fedha kitumike kwa kusaidia kufunga hesabu za serikali kwa taasisi zetu. Lengo letu ndio hilo kwamba jamani kama hizi fedha za serikali na kuna taasisi ya serikali ambayo inaweza ikafanya kazi ile, basi ipewe kipaumbele kwanza hiyo taasisi ya serikali ifanye kazi hiyo. Tutazishajihisha hizi taasisi zinazo *outsource*.

Mhe. Naibu Spika, orodha ya mashirika yaliyowasilisha hesabu zao wa *CAG*. Nimeshaichukua hiyo orodha nimeiona. Fedha za kutekeleza miradi ya *TASAF* na ile ya wananchi hazikufuatiliwa kwa ukamilifu. Nataka niseme kwamba mimi nilikuwepo hapa kama ni mtendaji, baadae nikaondoka, nimerudi tena kama mwanasiasa. Nilikuwa nikiangalia sana muongozo wa miradi ya wananchi haukuwa mzuri. *My person opinion*, inawezekana kwamba wengine wakawa na *opinion* tofauti, ndio waliotufikisha hapa. Miradi ya wananchi alikuwa anakuja tu

mtu Kamati hivi au kamati hivi. Kamati ya Sheha yenyewe tulikuwa tukiipelekea kusimamia, ilikuwa uwezo wa kusimamia hawana ni mdogo, sasa tumefika hapa.

Mhe. Naibu Spika, jambo zuri ni kwamba hakuna tena miradi ya wananchi, sasa hivi kuna mfuko wa jimbo, ambao mwenyewe Mheshimiwa Mwakilishi atakuwa ni msimamizi. Miradi ya *TASAF* nayo ni hivyo hivyo. Lakini haya maelezo ambayo tumeyapata sasa hivi, kwa sababu *TASAF* inaendelea na iko chini ya Mhe. Makamu wa Pili Rais, nitamuona Waziri mwenzangu tutakaa na tutaanza kuutizama huu muongozo wa *TASAF*. *TASAF* ina muongozo wake, kama kuna utata kidogo basi tunaweza tukau- *customize* kwa mujibu wa hali yetu ya Kizanzibari, tutafanya hivyo na tutatoa maelezo zaidi.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, imeelezwa hapa mgao wa *TASAF* kwa Zanzibar uwe angalau ile asilimia 4.5. Tutaitazama na tutaongea na wenzetu, hili ni jambo la kukaa tukaongea nao tu, kwa sababu huu ni mkopo unaokuja kwa Serikali ya Tanzania.

Halafu iliulizwa kiwango cha asilimia 10, ndugu yangu Mbarouk Wadi Mussa Mtando vile vile aliuliza kiwango cha asilimia 10. Hiki kiwango cha asilimia 10 kipo kulingana na utaratibu wao, kwa ajili ya kuwasaidia wale viongozi kuweza kufuatilia hii miradi. Kama hawafuatilii, hapo ndio pahala pa kuuliza, kwamba hizi pesa mlizopewa kwa ajili ya kufuatilia mnazifanyia nini sasa. Lakini ilitoka hoja kwamba tui-*review* tuitizame upya kwa sababu hii ni asilimia kubwa kidogo, basi nitakaa na Mhe. Mohamed Aboud ili tuitizame upya, tutashirikiana na ofisi inayosimamia miradi ya *TASAF* kwa Zanzibar na ile ya Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kusimamia utekelezaji wa sheria ya fedha na manunuzi. Hili nakubaliana na nyinyi moja kwa moja kwamba ni lazima sheria za fedha na manunuzi zisimamiwe ili tuweze kufanikisha utekelezaji wa sheria hii. Bila ya kuzisimamia hizi sheria ndio hapa mapotezi ya fedha nyingi sana yanatokea.

Kuhusu uandaaji wa mikataba ushirikishe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Hili ndio elekezo na siku zote Makamu wa Pili wa Rais anatushauri na kutuuliza sisi Mawaziri, kuhusu mikataba hii Mwanasheria ameiona. Sijui wenzangu hapa, lakini mimi nafanya naye kazi kwa karibu sana. Mikataba ya meli aliniuliza mara nyingi sana, Mwanasheria kaiona. Kwa sababu katika meli kuna mikataba miwili. Kuna mkataba wa ujenzi na kuna mkataba wa *finance* yote Mwanasheria kaiona. Kwa hivyo, hatuwezi tukasema tunatengeneza mikataba halafu Mwanasheria haioni. Ndio pale uliposema kwamba ukifanya kitu hicho maana yake una lako jambo,

usije tena ukalia na hoja alizotueleza Mhe. Ismail Jussa hapa, unaweza ukajikuta ndio wanakuondoa hao.

Utaratibu wa uuzwaji wa vitu chakavu. Kuna taratibu tatu zimewekwa katika sheria ya uuzwaji vitu chakavu.

(1) Taratibu ya kuuza kwa *tender*,

(2) Taratibu ya kuuza kwa mnada,

(3) Taratibu ya *Single Source*

Mhe. Naibu Spika, inawezekana kitu unachotaka kukiuza hakiwezi kutumika popote pale isipokuwa kikatumiwe na Kiwanda cha Sukari tu, kwa hivyo inabidi ukakiuze kwenye Kiwanda cha Sukari tu basi, hiyo ndio *single source*. Lakini sisi tunasema kwamba tutaangalia *the best option* ili tuweze kufuata ile sheria ya uuzwaji wa vitu chakavu.

Vile vile imezungumziwa sera ya mfumo wa ushukaji wa thamani ama upandaji wa thamani. Mhe. Naibu Spika, maandalizi yanakwenda vizuri na tunategemea vijana hawa tutawapa muda zaidi ili waweze kuikamilisha kwa wakati muafaka. Hii sera ni muhimu sana utunzaji na matengenezo ya mali za serikali hasa vyombo vya moto, hili ndio tatizo tulilonalo. Unaweza kusema kwamba tuna tatizo hili serikalini, tuna tatizo la *maintenance culture* ndani ya *society* yetu ya Kiafrika. Kwa hivyo, ile *society* inatunyemelea mpaka kwenye maofisi yetu nayo ndio hivyo hivyo.

Mhe. Naibu Spika, unaweza kukuta kitu kinataka spana au *fuse* ndogo tu basi kikawekwa hapo wee mpaka kikaja kuhitajia zaidi *more than one hundred, or two hundred million shillings* kwa kutengeneza. Nadhani hili itabidi maafisa wetu ambao wanalisimamia hili tukae nao na tuzungumze nao, Bima hasa kwa vyombo vya moto vya serikali, muongozo upo kwamba vyombo vyote vya moto vya serikali ni lazima viwe na Bima tena Bima yenyewe ikatwe kwa *Zanzibar Insurance,* sio uende kukata Bima kwengineko.

Sasa kama kuna mtu anapanda chombo kwenda Bima ya Serikali, aah mimi nasema *traffic* wanawajibu wa kuwasimamisha njiani, lakini muongozo upo na hata mwaka jana nakumbuka tulitoa toleo la kuwakumbusha vile vile. Tutatoa toleo zaidi la kuwakumbusha.

Kuhusu daftari la kudumu, karibu wote waliochangia Mhe. Naibu Spika, wamezungumzia daftari la kudumu. Nataka hapa mnisikilize kidogo. Nikimaliza matatu manne nitafunga mjadala

Mhe. Naibu Spika, ni kweli tulitoa fomu kwa taasisi zote kuorodhesha mali ambazo ziko chini ya taasisi hizo, kwa bahati nzuri na wote wakaorodhesha na wakarudisha, baadae tukaja kujikuta kwamba walivyoorodhesha wengi wameorodhesha sivyo. Namwambia kwamba nataka kuorodhesha kompyuta, anachukua kompyuta.

Kwa mfano wa kompyuta, anaichukua kompyuta kama kompyuta na kuiorodhesha kompyuta moja. Lakini ukweli ni kwamba ile *monitor* inaweza kuibiwa peke yake, *UPS* inaweza kuibiwa peke yake, *stabilizer* inaweza kuibiwa peke yake. Sasa ile yote ni kompyuta yeye kaorodhesha kompyuta tu moja. Tukasema kwa utaratibu huu bado mali ya serikali inaweza kuibiwa kwa sababu mtu anaweza kuja kuchukua *stabilizer* akenda zake, tukasema hapana

Sasa hivi tumeshaorodhesha wizara tano pamoja na thamani yake, lakini kuna gharama kubwa sana ya zoezi hili. Mwaka huu wa bajeti unaoanza tutaorodhesha tena wizara tatu, naomba nizitaje tena kabisa zijiandae. Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, na Wizara ya Katiba na Sheria.

Hili zoezi linataka pesa nyingi sana na linataka muda, kwa sababu kuorodhesha idadi tu ya vitu haitakusaidia kuweka katika *asset register,* ni lazima uweke na thamani, lakini wizara tano tayari na thamani zake tayari na tumechelewa, kwa sababu katika zile tano za mwanzo tulifanya kosa hatukuchukua *giant* mbili tukazitia pamoja Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafuzo ya Amali. Hizi ni *giant ministry* tumezitia pamoja katika kundi la kwanza imetuchelewesha kumaliza. Lakini nawaambieni Waheshimwa kwamba hoja yenu ni muhimu na sisi kama serikali tunaiona ni muhimu na tunataka tuimalize.

Hivi sasa tunajaribu kutafuta *other donors* wa kuweza kusaidia katika ku-*finance* hii tukishapata kutakuwa kuna *consultant* wengi zaidi wataifanya hiyo kazi katika kipindi kimoja, tunaweza kumaliza katika kipindi kifupi. Lakini kwa kweli na sisi tumeona na tunalifanyia kazi vizuri tu. Umuhimu wa kujenga majengo mapya, hili ni muhimu sana. Waheshimiwa Mawaziri wanalielewa sana, kwa sababu naweza kuthubutu kusema kwamba hapa Mawaziri ambao wanakaa katika majengo mazuri labda ni watatu au wanne tu, Mhe. Haroun Ali Suleiman, Mhe. Ali Juma Shamuhuna, Mhe. Juma Duni Haji na Mhe Abdillahi Jihad Hassan basi. Wengine

sisi majengo yetu ni yale tuliyorithi ya zamani, lakini sasa tunaandaa utaratibu wa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya. Tumeanza majengo mengine mmeona lile la Wizara ya Katiba na Sheria, lina ghorofa ngapi sijui sita au nane linakwenda.

Umetoa pendekezo zito Mhe Omar Ali Shehe, kwamba kikao cha bajeti kiwe kabla ya Juni na kimalizike kabla ya Julai. Mimi nataka nikuombe kwa kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, na hii Ofisi ya Katibu wa Baraza la Wawakilishi, iandike rasmi hoja hii kwa Mhe Makamu wa Pili wa Rais Serikalini, ili kuipa uzito serikali ikae na kuangalia faida na hasara zake, halafu na wao wataona nini cha kufanya. Mimi nasema hoja hii tuiandikie rasmi serikali ili tuone tutafanya nini.

Mhe. Naibu Spika, hoja kama nilivyosema ziko nyingi, lakini naomba nijibu hoja mbili za mwisho kwa uzito wake. Niliulizwa hapa na Mhe. Hija Hassan Hija kuhusu deni la taifa. Nataka nimwambie kufikia mwezi Machi mwaka 2013 deni la taifa ni 252.28 bilioni, za nje ni bilioni 203.77 za ndani ni bilioni 48.51 hilo ndio deni letu la taifa. Hoja ya kwanza ndio hiyo.

Hoja ya mwisho Mhe. Naibu Spika, hoja zote nimezichukua pamoja na haya niliyoyatolea maelezo tutaziandikia rasmi ili nitakapokuja tena Mwenyezi Mungu akitujaalia uhai na uzima mwezi wa Aprili, kwa mujibu wa kanuni 108(15) ya Baraza la Wawakilishi nitakuja tena kuzitolea maelezo zaidi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, na mimi namalizia kwa kuunga mkono hoja hii ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika): Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru tena kwa mara nyengine kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako kwa ajili ya kufanya majumuisho au ya kuhitimisha hoja iliomo kwenye ripoti yetu.

Naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Omar Yussuf Mzee (Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa ufafanuzi wake mzuri sana alioutoa. Kwanza kwa namna alivyojibu hoja za utekelezaji wa ripoti ya mwaka jana. Pili kwa jinsi alivyoanza kutoa ufafanuzi wa ripoti ya mwaka huu kama ni Mwenyekiti wa Kamati naridhika sana na maelezo aliyoyatoa. *(Makofi)*

Vile vile yanaonesha kwamba kwa vyovyote vile maana yake mtu anapokuzungumzia unajua maana hisia unaweza kujua namna gani yuko *serious*.

Kwa hivyo, naamini *seriousness* aliyoionesha mbele ya kikao hichi ndivyo itakavyokuwa utekelezaji ukijaaliwa mwaka 2014. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Mawaziri wote kwa namna walivyokuja mbele ya Baraza hili na kueleza namna walivyotekeleza ripoti ya mwaka uliopita. Katika hili naomba niseme kwamba hoja yetu ilikuwa hasa ijibiwe na watu wawili.

Kwanza ni Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu yeye ndiye Msimamizi wa Sera za Fedha na ndiye mwenye Ripoti ya Kamati ya *PAC* kama wenzetu duniani wanavyofanya. Vile vile na Mawaziri nao kwa sababu kama ilivyoelezwa kwamba wao ndio wasimamizi wakuu wa wizara, ingawa nasikitika kwamba mawaziri wengine hawakuwepo tofauti na alivyoeleza Mhe. Spika jana kuwataka wote wawepo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tulifurahi zaidi kwa sababu jambo hili halifanywi na Mawaziri tu, wanaomba ni mawaziri, lakini wanaotumia ni Makatibu Wakuu na mchakato huu wa fedha unakwenda katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ni ya bajeti ambapo hulazimika *Accounting Officers* kuja mbele ya Baraza hili kuomba na katika kipindi kile tunashuhudia namna walivyogangamaa katika kutaka tuwaidhinishie fedha. *(Makofi)*

Lakini ilipaswa pia katika awamu hii ya kuangalia namna ya walivyozitumia fedha tulitarajia na wao wawepo pale, ili tuone na wasikie namna gani walivyozitumia fedha, kwa sababu unavyoomba ndivyo namna unavyotakiwa ueleze namna ulivyozitumia.

Kwa hivyo, tulitaraji leo kule juu kule Makatibu wetu ambao ndio *Accounting Officers*, yaani maafisa wahasibu wa wizara zote 16 wawepo, ili waone namna ambavyo mawaziri wao na jinsi ripoti ilivyogusa utendaji wao katika suala zima la fedha wakiongozwa na *Pay Master General* (*PMG*). *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, *Pay Master General* ndiye yeye mwenye kuwateua wale, yaani uteuzi wa Makatibu Wakuu wanateuliwa na Mhe. Rais, lakini kuteuliwa kuwa Afisa Mhasibu unateuliwa na Katibu Mkuu. Kwa hiyo, dhamana yote ya Makatibu Wakuu kama *Accounting Officers*, basi anayo Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, sasa na yeye tulitegemea aongoze jopo la Makatibu Wakuu kuwepo pale. Sasa kama Mwenyekiti wa Kamati kwa kweli nasikitika sana na tabia inayooneshwa na Makatibu Wakuu kudharau chombo cha wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tabia hii napenda nikuhakikishie kwamba hatutaendelea kuivumilia zaidi ya hapa tulipofikia. Kwa kweli sisi humu ndani ni Wawakilishi halali wa wananchi na wala hakuna mtu aliyejileta humu ndani, na sote tumechaguliwa na watu wazima, vijana, mawalii, walevi pamoja na kila aina ya watu katika jamii. Kwa hivyo, haiwezekani kutudharau tunayo mamlaka makubwa sana. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, Makatibu Wakuu leo wanapokosa pale na *Accounting Officers* wote, kwa kweli tutakuja kuwa na hoja ngumu sana katika hoja ya bajeti, kwa nini tuwaidhinishie fedha ambazo kwamba hawataki kuja mbele yetu kuangalia namna gani fedha zile wamezitumia. Mhe. Naibu Spika, uvumilivu wetu sasa unakaribia mwisho. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba niwataje Waheshimiwa Mawaziri waliokuja mbele ya Baraza lako tukufu hili na kutoa hoja, ambao ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.
2. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.
3. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
4. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
5. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
6. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, ambaye hakuwepo.
   Mhe. Naibu Spika, baadaye naomba muongozo wako, kwamba wizara ambazo hazikuwasilisha utekelezaji wake Wawakilishi tutapata fursa gani ya kujua utekelezaji wa ripoti iliyopita.
7. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.
8. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ambaye hakuwepo katika kikao.
9. Mhe. Waziri wa Afya.
10. Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.
11. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.
12. Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ambaye hakuwepo katika kikao hichi.
13. Waziri wa Kilimo na Maliasili, ambaye hakuwepo katika kikao hichi.
14. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, yeye tunashukuru Kaimu aliwasilisha na ndio utaratibu tuliokubaliana, kwamba Waziri akiwa hayupo, basi aje Kaimu Waziri na huu ndio utaratibu unavyokwenda, sasa leo mratibu wa Serikali anasema sijui waziri huyu na serikali inaendeshwa vipi

sasa. Kwa hivyo, tunamshukuru Waziri wa Biashara kwamba ameleta Kaimu wake.

15. Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi na
16. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, tunamshukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waliochangia kwa hisia kali sana mjadala wetu, wao napenda niwataje kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Hija Hassan Hija
3. Mhe. Salmin Awadh Salmin
4. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
5. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
6. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
7. Mhe. Fatma Mbarouk Said na
8. Mhe Mohammed Mbwana Hamad.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru wote kwa kuunga mkono Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba niupongeze utaratibu huu tuliojiwekea, kwa sababu utaratibu huu ndio mara ya kwanza kufanywa na hii ndio inavyoonesha *accountability* ya serikali mbele ya chombo hichi, kwamba tunaagiza lakini mwisho wa siku mawaziri wanapata fursa ya kuja kueleza nini walichotekeleza.

Kutokana na hali hiyo, naomba nieleze masikitiko yangu, kwamba baadhi ya mawaziri badala ya kuja kueleza utekelezaji wa ripoti zilizopita baadhi ya mawaziri wamejibu ripoti hizi, ambapo tunataraji ripoti hizi jawabu lake lije mwakani tukijaaliwa ni katika kujifunza. *(Makofi)*

Katika hili Mhe. Naibu Spika, kwa uzito wa kikao hichi ambapo huu ni wakati pekee tunapoangalia utendaji wa serikali. Kwa hivyo, ninapendekeza kwamba kikao hichi basi kiwe ni maalum kwa ajili ya kupitia ripoti za serikali na tuache vikao vyengine vya Baraza tujadili mambo mengine ya miswada na mambo mengine ya kiserikali, lakini kikao hichi tukitenge maalum, ili Wawakilishi tupate nafasi pana ya kuihoji pamoja na kuiuliza serikali, kwa mantiki ile ile kwamba tunayo mamlaka Kikatiba ya kuisimamia serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, michango ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi imekwenda katika kusisitiza uwajibikaji, pia imekwenda katika kuona kwamba kunachukuliwa hatua kwa wale wote waliofanya matata katika fedha za umma. Vile vile michango ya Wajumbe imekwenda katika uchukuliwaji wa hatua madhubuti katika mapendekezo yaliomo katika ripoti.

Kwa hivyo, kwa ujumla michango yote ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi imekwenda katika kuunga mkono hoja na kusisitiza kwamba serikali lazima iwajibike, katika kuwawajibisha wale wanaokiuka sheria pamoja na kuhakikisha kama mapendekezo yaliomo kwenye ripoti yanafanyiwa kazi kwa ujumla wake.

Kwa mantiki hiyo, basi naomba Mhe. Naibu Spika uniruhusu niende kwenye mchangio wa ujumla. Kwanza naomba niseme kwamba ripoti tuliyoiwasilisha mbele yetu hapa ni ripoti ya mwaka 2009/2010 kwa ripoti tatu na ripoti ya mwaka 2010/2011 kwa Ripoti ya *Financial Auditing*. Sasa kazi ya leo hapa pamoja na kupata majibu ya utekelezaji, lakini kazi yetu kubwa ilikuwa ni kuwasilisha ripoti mpya itokanayo na ripoti tulizokabidhiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mashirika.

Wakati mwengine Waheshimiwa Wajumbe tunazungumzia kwamba hoja zinajirudia. Kwa mfano, hoja ya mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu na pengine mwakani, kwa hiyo tusishangae kwamba hoja hizi tunaweza kuzikuta. Jambo la msingi ni kwamba hoja isipojibiwa basi inaendelea kujitokeza katika ripoti zinazofuata.

Kwa maana hiyo, mara kwa mara kama ikiwa *Fixed Asset Register* pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri, kwa sababu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu amepewa mamlaka ya sheria kwamba aangalie, akague aone nini kilichopo, kwa hiyo yeye hajui hili liko kwenye mchakato au watu wanakwenda mbio ama hili vipi, yeye akiona buku halipo basi kazi yake ni kuandika tu katika ripoti. Kwa hivyo, kujirejea kwa hoja ni kutokana na kwamba hoja iliyohojiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu haikupata majibu katika wakati unaostahiki na hilo ni moja.

Jambo la pili Mhe. Naibu Spika, kuna uwezekano mkubwa kama ikiwa watendaji watakuwa wako makini katika kujibu *query*, kwa sababu nataka niseme kwamba, ili *query* iingie katika kitabu basi haingii tu kirahisi ni mchakato mrefu hupita. Mdhibiti huja katika taasisi anafanya *auditing* na pale anapokuja kuna *enter meeting* na *exit meeting*, maana yake *enter meeting* ni ile anayokwambia sasa hodi naingia kufanyakazi zake.

Lakini mwisho anapotoka kuna ile *exit meeting* jamani kwaherini natoka, lakini kwaherini natoka hukueleza kwamba nilichokikutia ni kadhaa kadhaa, na pale pale kwenye meza kama unacho basi unatakiwa umpe pale pale na unapompa maana yake hoja hiyo haiingii katika kitabu.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukimwambia karibu baada ya kukueleza ni kwamba huenda ofisini kwake na baadaye hukuandikia na kukukumbusha bwana nilikuja ofisini kwako na kasoro zilizopo ni moja, mbili, tatu na hukuandikia, maana yake nini? Wakati huo mtendaji anayo nafasi ya kujibu kama kweli ulipokuja kitu hichi hapana, lakini kitu hichi hivi sasa kimepatikana. Kwa hivyo, katika nafasi hiyo bado kuna nafasi ya kukifanya kitu kile kisiingie katika hoja ya Mdhibiti.

Lakini inapotokea katika hatua ile Mdhibiti akishaondoka katika ofisi ni kwamba anapokwenda zake anapoandika watendaji hawa-*respond* mpaka dakika ya mwisho Mdhibiti anaandika ripoti hakuna mawasiliano yoyote anayopata. Mhe. Naibu Spika, katika hatua hiyo Mdhibiti hulazimika kuandika ripoti na akishaandika ripoti basi suala hilo Mdhibiti halimuhusu tena, yaani kitu kikishaingia kwenye Ripoti ya Mdhibiti basi hakiko tena katika mamlaka ya Mdhibiti.

Mhe. Naibu Spika, naomba hiyo ieleweke kwamba kama ikiwa watendaji watakuwa wako makini, basi kuna uwezekano mkubwa kwa taasisi nyingi kuepuka *query*, lakini *query* zinakuwemo kwa sababu watendaji wetu takriban hawako makini. *(Makofi)*

Kuhusiana na suala la mapato Mhe. Naibu Spika nataka nieleze tu kwamba mapato yanayo *formula* yake, ambayo ni moja tu ni kuongeza mapato na ukapunguza matumizi, utakapoongeza mapato na kupunguza matumizi basi *automatically* mapato yatapanda, lakini utakapoongeza mapato na ukaongeza matumizi maana yake mapato hayatapanda.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana tukasema tufanye kitu hichi, yaani *simultaneous* tuongeze mapato na wakati huo huo tupunguze matumizi. Nashukuru Baraza lako mwaka jana lilifanya kazi nzuri sana na Kamati imekuja na *concern* hii, kwamba matumizi kama tukifanya utafiti matumizi ya serikali sehemu kubwa sana yanakwenda kwenye matumizi ya mafuta pamoja na vipuri.

Kwa hiyo, ndipo tukaja na hoja hii tukasema basi ikiwezekana na inawezekana kwa sababu hakuna lisilowezekana ni maamuzi tu, huwezi kusema kwamba tuna

tabia za Kiswahili hapana, tufike pahala siku moja tabia za Kiswahili tuache na tuseme tunasimamia hili na lazima tusimamie hili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tumependekeza hili kwamba matumizi ya vyombo vyote vya moto vya serikali viwe na utaratibu maalum. Naomba niseme kwamba kama nitarudi tena katika Kamati kwenye kila wizara nitakayotembelea basi kitu cha kwanza namkamata dereva wa Waziri lazima anioneshe *Log Book* nitaanza na yeye.

Kwa hivyo, kama dereva hakutuonesha *Log Book* alililolijaza basi tutamnyang'anya ufunguo, lazima twende hivyo tufike pahala tuamue na wala hatuwezi kwenda kwenye *business as usual* ikawa ndio *formula* yetu, kwa sababu tunazungumza *business as usual*, lakini sisi ndio wa kwanza tunafanya *business as usual*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tumelipendekeza hivyo kwa sababu tunataka tuanze suala hilo katika hilo. Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi nakumbuka katika hili kwamba baba yangu alikuwa ni dereva wa serikali na kipindi kile nilikuwa mdogo lakini nilikuwa nikimuona kwamba kila anapoondoka hujaza kwenye buku na sijui maana yake nini, lakini kila anaposimama kurudi ofisini huwa akijaribu kuandika na nilikuwa sijui maana yake nini, kumbe leo nakuja kujua aa! Ndio lile *Log Book*, ambalo tunasema tumeliachia na mambo yamekwenda na hivi sasa kila kitu ni mkorogo vyogo.

Mhe. Naibu Spika, mambo huharibika na msingi mkubwa wa kuharibika kwa mambo mimi nataka niwaambie ni kutokana na kutofuata Sheria za Manunuzi ndio msingi mkubwa. Kwa hivyo, kama mtafanya utafiti sehemu zote zenye mambo ambayo yamefeli, basi ukichunguza na kupeleleza utakuta kwamba sheria imekiukwa.

Kwa mfano, unapokwenda kwenye jengo lile la Wizara ya Fedha semeni mutakavyosema lakini Sheria za Manunuzi zimekiukwa na hata zile skuli tatu ambazo yule mkandarasi amekimbia kwenye Mradi wa Elimu ya Lazima Mtule Paje, Dimani mkandarasi amekimbia kabisa. Lakini ukifuatilia amekimbiaje mkandarasi, yaani ukifuata utaratibu wa kumpata huyu na wala hatujafanyia kazi, lakini tutalifanyia kazi na ninawahakikishieni mtakapofuatilia utaratibu wa kumpata mkandarasi basi mtakuta kuna pahala mme-*skip* ndio siri kubwa iliopo.

Mhe. Naibu Spika, leo mkandarasi yule akitaka kutiliwa fedha anakwambia aa! Usinilitie benki, mkandarasi huyu, yaani ukitaka kumfanyia malipo anasema aa!

Usinitilie, kwa sababu anachotiliwa chochote benki wanakata maana yake nini, maana yake mumechagua mtu ambaye hana uwezo ni *bankrupt* na wala sheria haikubali hili.

Mhe. Naibu Spika, mtindo huu wa kuwachagua watu ambao tunawapa kazi lakini kumbe vile tunawapa watu ulaji tu. Kwa mfano, anakuja mtu anataka kazi lakini hana shilingi hohe hahe, maana yake serikali mumlipe kwanza na hilo tulilikutia katika Wizara ya Afya, kwamba alipewa mtu tenda na mkataba unasema kwamba utamlipa asilimia hii kabla ya kazi na baada ya kazi utamlipa asilimia hii, lakini asilimia mia moja amelipwa kabla ya kufanya kazi.

Hali hii ina maana kwamba yeye mwenyewe alikuwa hana shilingi ya kuifanya hiyo kazi, lakini kumbe vile tenda zenu zote munawapa watu ambao wao wenyewe ni wakandarasi wa kuganga njaa tu na wala hawana chochote walichonacho.

Kwa kweli sheria inasema kabisa kwamba muwape watu ambao wanao uwezo, ili mtakachowalipa lakini kazi yenu waikamilishe na baadaye ndio muje mumaliziane, lakini leo mtu hana shilingi anakuja kuomba kazi serikalini, na kile unachompa wewe ndio mtaji wake wa kazi na hakuna utaratibu huo na sheria haijataka hivyo.

Sasa kama tukifanya vizuri tukiangalia Sheria ile ya Manunuzi utakuta kwamba kwanza ukiifuata vizuri ina kitu uwazi, kwamba watu wote iwe ni wazi wanakuja pale wana-*compete* katika tenda, lakini kuna kitu uwezo ndani yake. Kwa hiyo, ukisema sheria ile huifuati maana yake itakuwa hakuna uwazi wala uwezo na vitu kama hivyo ambavyo tunavizungumza.

Mhe. Naibu Spika, kitu chengine ni matumzi ovyo katika serikali. Kwa kweli matumizi ovyo tunajua kwamba kila mwaka Baraza lako hili linapitisha Bajeti ya Serikali, lakini tujiulize ule msingi wa taasisi kutayarisha Bajeti ya Serikali *base* yake huwa ni kitu gani.

Tunavyojua ni kwamba taasisi yoyote inakuwa na kitu Mpango Kazi, yaani kabla hamjaenda kufanya kazi basi mnakuwa na mpango kazi, kwamba tunakusudia kwa mwaka huu wa fedha kufanya kazi moja, mbili, tatu na huo ndio mpango kazi wetu huu tutahitaji nini na nini kukinunua ndio hiyo *Procurement Plan*, yaani Mpango wa Manunuzi.

Sasa unaposema kwamba taasisi haina Mpango wa Manunuzi *base* yako ya kuweka bajeti ilikuwa ni kitu gani ndipo pale tunapofikia pahala Mhe. Naibu Spika

kumbe bajeti zote tunazozipitisha hapa ni bajeti hewa tu, tulilishuhudia hilo katika Wizara.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kuna taasisi moja, maana wanatufanya sisi Kamati kama vile mbumbumbu hatufahamu kitu, haya tupeni Mpango Kazi wenu, wakasema Mpango Kazi tunao, haya leteni, basi wakatupa Mpango Kazi wa mwaka huu sijui 2013 unaanza tangu Juni ya mwaka jana mpaka Septemba ya mwaka huu, mbona tunadanganyana.

Kwa kweli, Mpango Kazi ni mpango wa mwaka na maana yake mwaka ni kuanzia Juni Julai na leo ukituambia Juni mpaka Septemba ya mwaka huu maana yake umekusudia kuidanganya kamati, kweli tunauza dodo lakini akili tunazo tunaweza tukasoma. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tunasema kwamba kuna matumizi ovyo kwa sababu hakuna Mpango Kazi katika taasisi nyingi za umma.

Katika hili Mhe. Naibu Spika kwa heshima kubwa naomba wizara ziandae Mpango Kazi kwa sababu kama hatuna Mpango Kazi, maana yake ni kusema kwamba hata hii bajeti na ndio ile inayokuja kwamba kuna hoja za watendaji hutwambia kwamba fedha zile hazitolewi katika wakati muafaka na husubiriwa katika kipindi cha Mei na Juni Wizara ya Fedha hawana cha kufanya kuhusu fedha basi hututilia tu fedha na hilo ni tatizo Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo, naomba matumizi ovyo yote yaondoshwe na msingi wa kuondosha matumzi ovyo ni kuwa na Mpango Kazi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika Serikali za Mitaa lilizungumzwa sana suala hili kwa maana ya Manispaa, Halmashauri pamoja na Mabaraza ya Miji. Kwa kweli tunayo matatizo makubwa. Kamati yangu kwa kujua uzito wa suala hili kwa mara ya kwanza tumeanza sasa kuwashirikisha Waheshimiwa Madiwani, kwa sababu Sheria ile ya Serikali za Mitaa Mabaraza yale ndiyo yenye mamlaka ya kuandaa bajeti.

Kwa maana hiyo, kamati yangu kila mara kwa kweli hushirikiana na Waheshimiwa Madiwani kuwaambia pamoja na kazi yao ya kupitisha bajeti, pia wanayo kazi ya kuhakikisha kwamba matumizi ya fedha yanakwenda kama yalivyopangwa.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumzie kwa ufupi sana ni kuhusu ufungaji wa mahesabu. Mhe. Naibu Spika, katika suala hili naomba niseme hivi katika kosa baya sana ni kosa la taasisi kutofunga mahesabu, ni afadhali ufunge mahesabu na

ionekane kuna *lose* ya milioni 1 au 10 ama 20 au 100, kulikoni taasisi kuwa haifungi mahesabu, maana yake taasisi isipofunga mahesabu inakufanya usijue chochote kinachoendelea ndani yake.

Katika hili Mhe. Naibu Spika, tuliona Mhe. Waziri alipokuja alisema kwamba mwaka jana alipata hoja tatu tu, yaani taasisi tatu, lakini mara hii kuna hoja kumi na mbili, yaani taasisi kumi na mbili, maana yake nini? Kwa kweli maana hii ni kwamba kuna utaratibu siku hizi, mwaka huu taasisi haina uwezo wa kufunga mahesabu basi huenda kukodi watu kwa ajili ya kuzuia ile *query*, basi huwakodi wale watu popote pale kwa ajili ya kuwafungia mahesabu, lakini mwaka huu ukishamaliza wao hujiona kama wameshamaliza kazi, kumbe vile hawajui na mwaka unaofuatia wanatakiwa wafunge hesabu na kila mwaka wafunge hesabu.

Sasa kinachotokea utakuja kukuta taasisi hii kufunga hesabu mwaka huu, lakini mwakani haifungi hesabu na ndipo pale *query* zinapokuja. Kwa hivyo, unaweza kwenda katika taasisi ukakuta mwaka huu wamefunga hesabu na mwengine hawakufunga, kwa sababu takriban kama walivyoeleza Waheshimiwa Wajumbe kwamba wahasibu wetu wengi hawana uwezo wa kufunga hesabu.

Mhe. Naibu Spika, katika hili niseme tukitumie Chuo chetu cha Uongozi wa Fedha Chwaka na wao walitupa *offer* kwamba pamoja na kufunga hesabu, lakini watatoa *training* maalum kwa ajili ya wahasibu katika kufunga mahesabu. Kwa hivyo, tunaomba tukitumie Chuo chetu cha Uongozi wa Fedha Chwaka.

Kwa kweli ripoti yetu imeeleza mapendekezo mengi na mara hii tumekuja na *style* mpya na wala hatukuja na maneno mengi tumekuja na *observation* na *recommendation* na hii ni *style* mpya na ndio matokeo ya mafunzo tuliyopata. Kwa hiyo, naamini kwamba Mhe. Naibu Spika, itamrahisishia Mhe. Waziri pamoja na Waheshimiwa wengine kuweza kutekeleza mapendekezo ya kamati kwa urahisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba kelele zetu tunazozifanya Waheshimiwa Wawakilishi tuna lengo moja tu, ni kwamba tunaitaka serikali yetu tukufu iliopo madarakani iwajibike basi. Kwa kweli katika sisi na mimi binafsi sitaki uwaziri na ninaamini baadhi ya wenzangu nao itakuwa ni hivyo hivyo na wala sina hakika siwezi kusoma moyo wa mtu, lakini fakhari yangu mimi binafsi ni kuona Serikali yetu hii ya Umoja wa Kitaifa inachapa kazi na kujenga imani pamoja na matumaini kwa wananchi, mwisho wa siku, ili wananchi waone kwamba huu ndio mfumo pekee unaofaa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Rais ambaye yupo madarakani kweli ni mchapakazi, Makamu wa Kwanza na wa Pili ni wachapa kazi na kweli ameteua kikosi kazi cha mawaziri na hiyo ndiyo fakhari yetu tu, sisi kule nyuma kunatutosha na kutaendelea kututosha. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wataalamu husema kwamba "Bunge goigoi huzaa serikali goigoi! Ama Bunge dhaifu huzaa serikali dhaifu!"

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumsikilize Mhe. Mwenyekiti anamalizia majumuisho yake.

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika): Mhe. Naibu Spika, nasema tunasema hivi kwa sababu tunaamini kwamba umakini wetu ndio utaifanya serikali iwe makini zaidi, kwa sababu kadri sisi tutakavyokuwa makini na serikali nayo itakuwa makini. Kwa hivyo, kuna siku tutakuja na plasta za midomo humu na tunao uwezo wa kujitia plasta za midomo humu na tukaja tusiseme chochote na tukamaliza tukaenda zetu, lakini athari itakuwa kwa nini, itakuwa hatuwafanyii wananchi haki. *(Makofi)*

Kwa mfano, jana nilikuwa nazungumza na Mhe. Hija Hassan Hija aliniambia ah! Madamu ukisema au usiseme unapata posho, kwa hiyo tusiseme, basi nilimwambia tutakuwa hatuwafanyii haki wananchi na tuache tuwafanyie wananchi haki.

Mhe. Naibu Spika, niwezalo kulifanya ni kusema, na kusema nimeshasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, tumalizie hoja niwahoji wale wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujamaliza kwanza niwashukuru kwa kazi nzuri tuliyofanya tangu asubuhi hadi hivi sasa na kuweza kumaliza hoja nzito sana kwa siku ya leo. Kwanza nimuahidi Mhe. Mwenyekiti maombi yake mawili aliyoyatoa kwa Spika, kwamba moja tufuate utaratibu mpya

wa mambo ya bajeti, tutakaa na Kamati ya Uongozi na tutaiandikia serikali, hilo ninamuahidi.

Pili kwamba kipindi kama hiki tufanye kazi moja tu kupitisha Kamati za Kudumu, ili twende mbali zaidi. Tatu kusikitika kwamba mawaziri watatu hawakuwasilisha ripoti zao, nadhani serikali imesikia lakini na sisi kama Baraza tutachukua jitihada.

Baada ya hayo, niwashukuru tena kwamba kazi tumefanya vizuri na naomba niakhirishe kikao hiki hadi tarehe 19/04/2013 saa 3.00 za asubuhi.

(Saa 2:40 Usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 19/04/2013 saa 3.00 asubuhi)